# URUDIAJI NA UWASILISHAJI WA MAANA KATIKA USHAIRI WA KISASA

UNIVERSITY OF NAIROBI LIBRARY
EAST AFRICANA

NA

OIRO GEORGE OMONDI

C50/76789/2014

CHUO KIKUU CHA NAIROBI

IDARA YA KISWAHILI

TASNIFU HII IMETOLEWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI (M.A.) KATIKA CHUO KIKUU CHA NAIROBI.

NOVEMBA, 2017

A1701625A
University of Nairobi Library Thesis
2016

# UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu binafsi na haijatolewa kwa mahitaji ya shahada ya uzamili katika chuo chochote kingine.

---------------------------------- 3/11/2017

Oiro George Omondi Tarehe

Mtahiniwa

Tasnifu hii imeandikwa na kutolewa kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi walioteuliwa na Chuo Kikuu cha Nairobi.

---------------------------------- 3/11/2017

Prof. Kyallo Wadi Wamitila Tarehe

---------------------------------- 3/11/2017

Mwl. Leonard Sanja Leo Tarehe

# TABARUKU

Tasnifu hii naitabaruku kwa mke wangu mpendwa, nana Lucy Omondi na mtoto wangu Cedric Caeser Omondi, kwa uvumilivu wenu ambao umenisaidia kuzamia na kuibukia kazi hii. Mwenyezi Mungu awajazie rehema na awalinde dhidi ya ovu lolote.

Kwa wazazi wangu, Musa na Jane Oiro pamoja na ndugu zangu Jacky, Doro, Vin, Anny, Willy na Wicky, mlinipa msukumo chanya wa kulisukuma gurudumu la kazi hii. Mola awape nguvu na uwezo wa kutimiza malengo ya mustakabali wenu.

# SHUKURANI

Awali ya yote, naichukua fursa hii adimu kumshukuru Maulana kwa uhai, nguvu, baraka na uwezo wa kuiwazia na kuishughulikia tasnifu hii nzima. Pili, maadamu ulimwengu umenitia darasani, ukanifundisha maana ya kurudisha wema kulikotokea wema, ama hisani kulikojiri hisani, sina budi kulipa deni hili la wema japo kwa heko na asante.

Ulumbi ambao umeniongoza maishani tangu nikiwa mdogo ni kuwa ukiujua huu, huu huujui. Hakika nitakuwa mwingi wa makosa nisipowashukuru wasimamizi wangu farisi wenye tajiriba pana katika lugha ashirafu ya Kiswahili, ambao wamenijenga kwa kunijuza nisiyoyajua na kunielekeza ipasavyo ili kuikamilisha tasnifu hii. Profesa Kyallo Wadi Wamitila na Mwalimu Leonard Sanja Leo, nawavulia kofia.

Ni kweli kwamba barabara nyoofu na laini hujengwa na wengi. Hii ndiyo maana nawashukuru kwa dhati ya moyo wahadhiri wangu walioniongoza katika kozi hii. Hawa ni: Prof. John Habwe, Prof. Iribe Mwangi, Prof. Kineene wa Mutiso, Prof. Mwenda Mbatiah, Prof. Rayyah Timammy, Dkt. Zaja Omboga, Dkt. Jefwa Mweri, Dkt. Evans Mbuthia, Dkt. Prisca Jerono na Mwalimu Mary Ndung'u. Mola awazidishie nguvu za kitaaluma ili kuzidi kukuza na kunoa bongo za wengine.

Chango ni kuchangizana. Hakika, wanafunzi wenzangu wamekuwa nguzo muhimu sana katika kutimiza lengo langu. Ushirikianao na mchango wao usiomithilika umenifaa pakubwa hivyo siwezi kuwapuuza kwa vovyote vile. Hawa ni: Jackline, Lilian, Veronica, Nancy, Rose, Pauline, Musamali, Okello, Raymond, Silas, Florence, Naisimoi, Githinji, Victor, Peter, Claris, Christine, Shem na Domnic. Asanteni na Maulana awaongoze mnapoendelea kulisukuma gurudumu la maisha.

Kimsingi, tasnifu hii ni tokeo la umoja ambao umenihakikishia nguvu za kujenga mustakabali wangu kiusomi. Taibu! Kidole kimoja hakivunji chawa. Alhamdulilahi!

# IKISIRI

Tasnifu hii imeshughulikia urudiaji na uwasilishaji wa maana katika diwani ya *Dhifa* na *Vifaru Weusi.* Tumeangazia mambo yafuatayo: usuli, suala la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, sababu za kuchagua mada, upeo na mipaka ya utafiti, yaliyoandikwa kuhusu mada, msingi wa kinadharia na mbinu tulizotumia kufanya utafiti. Tumeeleza aina mbalimbali za urudiaji kama sehemu ya kimsingi ya ubainishaji wa viwango vya urudiaji. Tumetoa maana za aina za urudiaji na kuzigawa katika vitengo vitatu vikuu ambavyo ni: urudiaji sahili, urudiaji wa kimaumbo na urudiaji wa kimuundo. Tumechunguza aina za urudiaji kama zinavyojitokeza katika diwani ya *Dhifa* na *Vifaru Weusi* kwa kutoa mifano mwafaka ili kudhihirisha namna ambavyo washairi wametumia urudiaji kuwasilisha maana na kuendeleza dhamira. Tumeangazia dhima na athari ya urudiaji kama mbinu ya kipekee inayotumiwa na washairi kuwasilisha maana na kuthibitisha namna urudiaji unavyomwathiri mpokeaji kwa kuelezea dhima zifuatazo: usisitizaji wa maana, uelewekaji, upigaji mwangwi, suala la wizani, ukumbukaji, suala la ujumi na uziada. Tumehitimisha kwa kutoa muhtasari wa utafiti na mapendekezo ya tafiti nyinginezo.

YALIYOMO

Mada....i
Ungamo....ii
Tabaruku....iii
Shukurani....iv
Ikisiri....v
**SURA YA KWANZA:UTANGULIZI....1**
1.1 Usuli....1
1.2 Suala la utafiti....3
1.3 Malengo ya utafiti....3
1.4 Maswali ya utafiti....3
1.5 Sababu za kuchagua mada....4
1.6 Upeo na mipaka....4
1.7 Yaliyoandikwa kuhusu mada....4
1.8 Msingi wa kinadharia....8
1.8.1 Viwango vya ukiushi katika nadharia ya umitindo....11
1.8.2 Kiwango cha ukiushi wa kisarufi....12
1.8.3 Kiwango cha semantiki....13
1.8.4 Kiwango cha kimaandishi au grafolojia....14
1.8.5 Kiwango cha kileksia....14
1.8.6 Kiwango cha kihistoria....15
1.9 Mbinu za utafiti....16
1.9.1 Sampuli....16
1.9.2 Ukusanyaji wa data....16
1.9.3 Uchanganuzi wa data....16
1.9.4 Uwasilishaji wa matokeo....16
1.10 Hitimisho....17
**SURA YA PILI:MSINGI WA URUDIAJI....18**
2.1 Utangulizi....18
2.2 Dhana ya urudiaji....18

2.3 Aina za urudiaji ........................................................ 19
2.3.1Urudiaji sahili ........................................................ 19
2.3.2 Urudiaji wa irabu na konsonanti ........................................................ 20
2.3.3 Urudiaji wa silabi ........................................................ 20
2.3.4 Urudiaji wa neno ........................................................ 20
2.4 Urudiaji wa kimaumbo ........................................................ 21
2.5 Urudiaji wa kimuundo ........................................................ 21
2.6 Aina za usambamba ........................................................ 22
2.6.1 Usambamba wa kisintaksia ........................................................ 22
2.6.2 Usambamba wa kivisawe ........................................................ 23
2.6.3 Usambamba wa kitanakuzi ........................................................ 23
2.6.4 Usambamba wa kisemantiki ........................................................ 24
2.6.5 Usambamba wa kifahiwa ........................................................ 24
2.6.6 Usambamba wa kidhamira ........................................................ 25
2.6.7 Usambamba wa kimuundo ........................................................ 25
2.6.8 Usambamba wa kiwizani ........................................................ 25
2.7 Urudiaji wa kibalagha ........................................................ 26
2.7.1 Anafora ........................................................ 26
2.7.2 Epifora ........................................................ 27
2.7.3 Mrejeokuwili ........................................................ 27
2.7.4 Anadiplosia ........................................................ 27
2.7.5 Epanalepsia ........................................................ 28
2.8 Hitimisho ........................................................ 28
**SURA YA TATU:URUDIAJI KATIKA DIWANI YA *DHIFA*** ........................................................ **29**
3.1 Utangulizi ........................................................ 29
3.2 Urudiaji wa irabu na konsonanti ........................................................ 29
3.3 Urudiaji wa silabi ........................................................ 30
3.4 Urudiaji neno ........................................................ 32
3.5 Urudiaji wa kimaumbo ........................................................ 34
3.6 Urudiaji wa kimuundo ........................................................ 36

3.6.1 Usambamba wa kimuundo ........ 36
3.6.2 Usambamba wa kisintaksia ........ 37
3.6.3 Usambamba wa kivisawe ........ 38
3.6.4 Usambamba wa kitanakuzi ........ 39
3.6.5 Usambamba wa kisemantiki ........ 40
3.6.6 Usambamba wa kidhamira ........ 42
3.6.7 Usambamba wa kiwizani ........ 43
3.7 Urudiaji wa kibalagha ........ 44
3.7.1 Anafora ........ 45
3.7.2 Epifora ........ 45
3.7.3 Anadiplosia ........ 46
3.7.4 Epanalepsia ........ 47
3.8 Hitimisho ........ 48
**SURA YA NNE:URUDIAJI KATIKA DIWANI YA *VI FARU WEUSI* ........ 49**
4.1 Utangulizi ........ 49
4.2 Urudiaji wa irabu na konsonanti ........ 49
4.3 Urudiaji wa silabi ........ 50
4.4 Urudiaji neno ........ 51
4.5 Urudiaji wa kimaumbo ........ 53
4.6 Urudiaji wa kimuundo ........ 55
4.6.1Usambamba wa kimuundo ........ 55
4.6.2 Usambamba wa kisintaksia ........ 57
4.6.3 Usambamba wa kivisawe ........ 59
4.6.4 Usambamba wa kifahiwa ........ 60
4.6.5 Usambamba wa kitanakuzi ........ 62
4.6.5 Usambamba wa kisemantiki ........ 63
4.6.7 Usambamba wa kidhamira ........ 65
4.6.8 Usambamba wa kiwizani ........ 67
.7 Urudiaji wa kibalagha ........ 68
4.7.1 Anafora ........ 68
4.7.2 Anadiplosia ........ 69

4.7.3 Epifora....70
4.8 Hitimisho....71
**SURA YA TANO:DHIMA NA ATHARI ZA URUDIAJI KATIKA DIWANI ZA *DHIFA* NA *VIFARU WEUSI*....72**
5.1 Utangulizi....72
5.2 Usisitizaji wa maana....72
5.3 Uelewekaji wa ujumbe....74
5.4 Upigaji mwangwi....75
5.5 Kujenga wizani....76
5.6 Dhima ya ukumbukaji....77
5.7 Suala la ujumi....79
5.8 Suala la uziada....81
5.9 Hitimisho....83
**SURA YA SITA:HITIMISHO....84**
6.1 Utangulizi....84
6.2 Muhtasari wa utafiti....84
6.3 Mapendekezo....86
**MAREJELEO....87**

# SURA YA KWANZA
# UTANGULIZI

## 1.1 Usuli

Urudiaji ni dhana pana na ya kimsingi kabisa ambayo msanii hutumia kuwasilisha maana katika kazi ya fasihi. Urudiaji ni fani ambayo inajihusisha na matumizi ya sauti, silabi, maneno na ruwaza za sentensi, zaidi ya mara moja katika kazi ya fasihi ili kuleta msisitizo wa maana hivyo kuikuza dhamira. Kuna aina mbalimbali za urudiaji ambazo mshairi anaweza kutumia kuwasilisha maana kama vile: urudiaji sahili, urudiaji wa kimaumbo na urudiaji wa kimuundo ambao unahusisha sifa ya usambamba. Leech (1969:62) anasema kwamba urudiaji ni njia mojawapo ya kimtindo inayoweza kutumika kuleta uziada. Dhana hii ya uziada aghalabu hutumika kama sifa inayochangia uwasilishaji wa maana. Uziada huu unaweza kupatikana au kutopatikana katika ushairi kwa kutegemea lengo na mtindo wa mshairi mwenyewe.

Katika ushairi sauti, silabi, maneno au vifungu vya maneno vinaweza kurudiwarudiwa kama njia ya kukuza dhamira yake. Sifa hizi za urudiaji zinaweza kuzua hisia za mpokeaji na kusisitiza suala linalozungumziwa ama zikatumiwa kwa minajili ya kuleta urari wa vina hasa katika mashairi ya kiarudhi.

Urudiaji unaweza kujitokeza katika mashairi ya kisasa. Kutokana na kubadilika kwa mitazamo ya washairi kuhusu sheria za utunzi, ushairi wa aina yoyote, wa kufuata arudhi au wa kutofuata arudhi unaweza kuwa wa kisasa. Haimaanishi kwamba ushairi usiofuata arudhi kabisa ndio wa kisasa pekee. Hata mashairi ambayo yametungwa kufuata sheria lakini hayajafuata sheria hizo kikamilifu pia ni ya kisasa. Kimsingi, ushairi wa kisasa ni ule ulioanza kutungwa katika miaka ya mwanzo wa karne ishirini na ambao una mabadiliko ya kimuundo japo unaweza kuwa huru au wa kimapokeo.

Kulingana na Yeats na wenzake (1976), washairi wa kisasa wanaweza kutumia mistari mifupi katika utunzi wao badala ya kutumia koma na kikomo. Hufanya hivyo ili utunzi wao uwe unaovutia kimtindo na usioweza kutabirika kimuundo. Ushairi wa kiarudhi huweza kutabirika kutokana na sheria zinazozingatiwa. Mpokeaji wa mashairi anapaswa kuhusisha fikira zaidi kuliko hisia zake ikizingatiwa kwamba ujumbe wa shairi unapaswa kufikiriwa kwanza kabla ya muundo wake. Washairi wa kisasa hutilia maanani sana athari inayoletwa na neno katika shairi kuliko namna shairi hilo linavyoundwa. Hii ni kutokana na haja ya kuwasilisha ujumbe kwa

jamii, jambo ambalo wanaliona kuwa muhimu zaidi kuliko muundo wa shairi lenyewe. Ujumbe hubebwa katika neno na ruwaza za sentensi ambazo mshairi hutumia kwa mtindo wake mwenyewe.

Mtindo wa mshairi huweza kutokana na mbinu anazotumia kama vile urudiaji na namna anavyofinyanga lugha kutokana na uhuru alio nao. Washairi wawili wanaweza kutumia mbinu hii ya urudiaji kwa njia na viwango vinavyotofautiana. Hali hii inategemea mtindo binafsi wa mshairi na namna anavyotaka kuwasilisha maana kwa njia inayomtambulisha. Anaweza kutumia urudiaji kwa kuchimuza maneno au akakosa kutumia uziada huu kwa kuhofia kudhoofisha maana katika kazi yake. Kwa kuwa fasihi hulenga masuala ya kijamii, mshairi anapaswa kuimarisha maana hasa anapomulika masuala yanayohusu jamii moja kwa moja hususan masuala ibuka. Katika uchanganuzi wetu wa diwani husika, tumejaribu kubainisha athari za urudiaji wa aina mbalimbali.

Katika kazi hii, mbali na kutilia mkazo sifa za urudiaji wa maneno, tumeangazia namna urudiaji wa virai na vishazi unavyojitokeza. Kwa mujibu wa Wamitila (2008:309), urudiaji wa kimuundo unatokea pale ambapo muundo fulani umerudiwa. Muundo huo unaweza kuwa wa kishazi au sentensi. Urudiaji unahusishwa sana na ushairi na ukitokea katika kazi ya kinathari basi huingiza sifa za kishairi katika kazi hiyo. Anataja namna mbalimbali ambavyo urudiaji wa kimuundo unaweza kujitokeza katika ushairi. Katika kazi hii tumeangazia urudiaji na jinsi unavyodhihirisha mtindo wa mwandishi katika diwani za *Dhifa* na *Vifaru Weusi* mbali na kulinganisha sifa hii ya urudiaji katika diwani hizi mbili.

Msanii anapoitumia lugha katika kazi yake huwa anaazimia kuwasilisha mawazo yenye maana na kuyafikisha kwa jamii inayomiliki lugha yenyewe kwa njia ya ubunifu. Urudiaji ni mfano wa mbinu ya kutumia lugha kwa ubunifu na hutofautisha pakubwa lugha ya maongezi ya kawaida na lugha ya kisanii katika ushairi. Aghalabu katika shairi, vifungu vya maneno kama vile virai, vishazi na sentensi huweza kurudiwarudiwa ili kusisitiza maana.

Washairi, Kezilahabi na Muhammed Khatib wameandika diwani nyingi ambazo zinazungumzia masuala mbalimbali ya kijamii. Hata hivyo, diwani hizi za ushairi wa kisasa tulizoteua zinakisiwa kuwa na upeo zaidi kimbinu na kimaudhui. Zinahusisha masuala ibuka kama vile mapenzi, uongozi mbaya, ufisadi na mengineyo ambayo yanaathiri moja kwa moja maisha ya

binadamu. Kazi zilizopo kama vile kazi ya Mwania (2007) haijabainisha aina mbalimbali za urudiaji katika ushairi wa kisasa. Huu ulikuwa msukumo tuliokuwa nao ili kuliziba pengo hili la kiusomi hivyo kupanua mielekeo ya uhakiki wa ushairi wa kisasa. Aidha, mapendekezo yaliyotolewa na Mwania (2007) kuhusu haja ya tafiti zaidi kufanywa kuhusu fani katika ushairi huru kutokana na upana wake, yametuchochea kuchunguza urudiaji kama mbinu ya kimuundo na kimtindo kwa kubainisha aina zake mbalimbali.

Wamitila (2008:233) anaeleza kwamba urudiaji ni muhimu sana katika fasihi. Hii ni kwa sababu dhana ya mwigo au muhakati inayohusishwa na Plato na Aristotle, na ambayo ndiyo dhana ya kimsingi katika uchanganuzi wa matini ya kifasihi imejengwa katika msingi wa urudiaji. Katika uhalisia wa jamii, kinachowasilishwa katika kazi ya fasihi, kimsingi huwa kimerudiwa. Hii ndiyo maana uchanganuzi wa mbinu hii ya urudiaji ni muhimu sana si katika ushairi pekee bali pia fasihi kwa jumla.

## 1.2 Suala la utafiti

Utafiti huu umechunguza urudiaji katika diwani za *Dhifa* na *Vifaru Weusi* na kubainisha umuhimu wa mbinu hii katika uwasilishaji wa maana na ukuzaji wa dhamira katika ushairi. Tumeangazia urudiaji, ulivyo katika diwani husika na kubainisha namna washairi wanavyoutumia kutimiza malengo yao.

## 1.3 Malengo ya utafiti

Utafiti huu umetimiza malengo yafuatayo:

i. Kueleza aina mbalimbali za urudiaji katika ushairi.
ii. Kubainisha matumizi ya urudiaji katika diwani ya *Dhifa.*
iii. Kubainisha matumizi ya urudiaji katika diwani ya *Vifaru Weusi.*
iv. Kubainisha dhima na athari za urudiaji katika diwani za *Dhifa* na *Vifaru Weusi.*

## 1.4 Maswali ya Utafiti

i. Je, kuna aina zipi za urudiaji katika ushairi?
ii. Je, urudiaji umejibainisha vipi katika diwani ya *Dhifa*?
iii. Je, urudiaji umejibainisha vipi katika diwani ya *Vifaru Weusi*?
iv. Je, urudiaji una dhima na athari gani katika diwani teule za *Dhifa* na *Vifaru Weusi*?

## 1.5 Sababu za kuchagua mada

Katika utafiti huu, tumeziteua diwani za *Dhifa* na *Vifaru Weusi* ili kuchunguza namna washairi wanavyotumia urudiaji kuwasilisha maana. *Dhifa* ni diwani iliyoandikwa miaka mingi baada ya *Kichomi* hivyo tunahisi kwamba ni ya kisasa na kama ilivyo *Vifaru Weusi*, ambayo imeandikwa hivi majuzi, inaangazia masuala yanayoibuka na yanayoathiri jamii ya kisasa kama vile ufisadi, mapenzi, suala la utawala mbaya, utabaka na mengineyo. Kwa hivyo, kwa kuchagua kuchanganua urudiaji, msomaji wa kazi hizi ataelewa vyema masuala yanayozungumziwa kimtindo katika diwani hizi. Kila mtunzi na mwandishi wa fasihi huwa na mtindo wake unaomtambulisha kama msanii fulani. Urudiaji ni muhimu sana katika uwasilishaji wa maana kwani husaidia katika kusisitiza na kutilia maanani ujumbe katika shairi. Tumechagua kuchanganua urudiaji katika diwani hizi ili kuwasaidia wasomaji wa mashairi kuzielewa kazi hizi barabara na kuwasaidia watafiti wa baadaye kuweza kuchanganua vipengele vingine vya kimtindo katika kazi hizi.

Tumeziteua diwani za *Dhifa na Vifaru Weusi* kutokana na kukosekana kwa kazi zinazochanganua urudiaji katika diwani hizi. Aidha, udurusu wetu wa kimbele umedokeza kwamba kazi tulizoteua hazijawahi kuchunguzwa kinadharia. Hivyo, utafiti huu ni mwafaka kujaza pengo lililopo ili washairi na wasomaji wengineo waweze kubainisha namna urudiaji unavyotumika kuwasilisha maana katika diwani husika.

## 1.6 Upeo na mipaka

Utafiti huu umejikita katika uchanganuzi wa kimtindo wa diwani za *Dhifa* na *Vifaru Weusi*. Katika kazi hii, tumeangazia aina mbalimbali za urudiaji ambazo washairi wametumia kuwasilisha maana na kukuza dhamira. Tumejibana katika aina za urudiaji ambazo zinadhihirika katika diwani hizi kwa kutoa mifano mahususi na kueleza athari za urudiaji huo na dhima yake kwa mpokeaji.

## 1.7 Yaliyoandikwa kuhusu mada

Mwania (2007) alifanya utafiti kuhusu usambamba katika ushairi huru. Alijaribu kudhihirisha namna washairi huru wanavyotumia usambamba katika kazi zao kuibua msuala mbalimbali katika jamii. Uchanganuzi wake ulilenga kuonyesha namna washairi wanavyotumia uhuru wao

wa kutamba na kueleza mchango wa usambamba katika utoaji wa ujumbe kwa jamii lengwa. Alitafiti namna usambamba unavyodhihirika katika ushairi huru kwa kuzingatia misimbo ya kiheminitiki, kiseme, matukio, kiishara na kirejelezi kwa kujibana katika nadharia ya semiotiki inayohusu ishara na uashiriaji.

Alidhihirisha namna ambavyo washairi wa kisasa wanavyotumia uhuru wao kumulika masuala ya jamii. Katika kazi yake, alibainisha namna usambamba unavyojitokeza katika diwani za: Kichomi ya Kezilahabi (1974), Mchezo wa Karata ya Mberia (1997) na Chembe cha Moyo ya Mazrui (1988). Alijadili misimbo mbalimbali na mifano iliyopo katika mashairi huru teule mbali na kueleza kuhusu usambamba kwa jumla bila kujikita katika aina yoyote ya usambamba.

Kuhusu diwani alizochagua hasa Kichomi ya Kezilahabi, masuala yanayoikumba jamii hubadilika kadiri ya mpito wa wakati hivyo mielekeo ya kuyatazama masuala haya pia huweza kubadilika ikizingatiwa kwamba lugha kama njia ya uwasilishaji ni sayansi na huweza kubadilika jinsi wakati unavyobadilika. Diwani ya *Dhifa* iliandikwa miaka thelathini na minne baada ya *Kichomi* hivyo uwezekano wa kuibua masuala yale yale kwa mtindo ule ule ni finyu. Utafiti wetu unahusu viwango vyote vya urudiaji. Tumeangazia aina tofautitofauti za ruwaza za sentensi na namna ambavyo zimetumika na washairi kuwasilisha maana.

Mwelekeo aliotumia Mwania ni tofauti sana na wetu. Katika kazi hii, tumeshughulikia urudiaji kwa kujikita katika aina zake mbalimbali kwa kutumia nadharia ya umitindo na kubainisha namna urudiaji huu unavyowasilisha maana katika diwani husika. Mwania hakueleza aina tofauti za muundo huu wa urudiaji wala dhima na athari za usambamba katika uwasilishaji wa maana, suala ambalo tumejikita katika kuchanganua. Aidha, hakubainisha aina mbalimbali za muundo huu wa urudiaji. Utafiti wetu umejumuisha uchanganuzi wa viwango mbalimbali vya urudiaji wa maneno na ruwaza za sentensi katika diwani husika.

Mnenuke (2010) aliichanganua dhima ya urudiaji katika mawasiliano akibainisha kwamba urudiaji unaweza kuimarisha au kudhoofisha maana au kupunguza na kuongeza msisitizo wa dhana inayozungumziwa. Anadhihirisha kwamba dhana hii ya urudiaji hujitokeza zaidi katika mazungumzo ambapo wazungumzaji wanakuwa na uhuru wa kutumia mbinu zozote wanazozijua ili kuwezesha mawasiliano yafanikiwe kwa kiwango kinachostahili. Uchunguzi wake umejikita katika namna lugha inavyotumika katika mazungumzo. Hakujikita katika

uchanganuzi wa kazi yoyote ya fasihi bali alibainisha umuhimu na uamilifu wa urudiaji katika mawasiliano kwa jumla. Utafiti wetu umechunguza namna urudiaji na aina zake mbalimbali unavyotumika na washairi wa kisasa kuwasilisha maana kwa kujikita katika diwani ya *Dhifa* na *Vifaru Weusi.* Utafiti huu umebainisha urudiaji kama mbinu ya kimtindo ambayo mshairi yeyote anaweza kutumia kwa uhuru na upekee wake katika uwasilishaji wa maana na ukuzaji wa dhamira.

Kundi la ' Migrant Education Program Consortium Incentive' (2012) lilizungumzia vipengele vya urudiaji kama vile urudiaji wa irabu, vokali na maneno katika mashairi matatu teule ya Kiingereza. Lilibainisha jinsi vipengele hivi vinavyojitokeza katika mashairi hayo bila kushughulikia maana zinazowasilishwa na maneno hayo. Aidha, lilijikita katika viwango vichache tu vya urudiaji na kuacha vipengele muhimu kama vile urudiaji wa ruwaza za maneno. Ni kazi ambayo haikuonyesha dhima na athari za maneno yaliyorudiwa katika uwasilishaji wa maana wala haikuchanganuliwa kinadharia. Hata hivyo, ina uhusiano wa karibu na utafiti wetu ambao unajihusisha na urudiaji wa viwango vyote kwa kujikita katika diwani mbili kuu. Tofauti na kazi ya kundi hili, utafiti wetu umechanganua namna urudiaji na aina mbalimbali za urudiaji zinavyotumika kuwasilisha maana. Tumevibainisha viwango hivyo na kueleza dhima zao katika ukuzaji wa dhamira katika diwani teule. Katika uchanganuzi wa kazi za fasihi, ubainishaji wa mbinu ya kimtindo iliyotumiwa na mshairi haitoshi kudhihirisha lengo la mwandishi bali dhima na athari ya mbinu hiyo ni muhimu katika kuielewa dhamira.

Manjavidze (2013) anazungumzia suala la urudiaji akilizingatia kama suala muhimu sana la kimtindo katika matini ya fasihi. Katika makala yake, anaeleza aina tofauti tofauti za urudiaji na kutoa mifano ya kijumla bila kujikita katika diwani yoyote. Hajabainisha ni matini gani ambayo urudiaji huo unajitokeza wala uchanganuzi wake haujatumia msingi wowote wa kinadharia. Katika kazi yake, ametoa mifano na kueleza namna urudiaji wa ziada unavyoweza kudhoofisha maana unapotumika katika matini. Anaeleza urudiaji kama mbinu ya kipekee kabisa ambayo mwandishi anaweza kutumia kuwasilisha maana. Anasisitiza kwamba sio maneno wala ruwaza za sentensi pekee zinazorudiwa bali pia sauti. Kwa kuthibitisha hali hii, anatoa mifano ya sauti zinazorudiwa katika sentensi. Kazi hii ina uhusiano mkubwa na utafiti ambao tumefanya ijapokuwa haijajikita katika uchanganuzi wa diwani yoyote kinadharia, jambo ambalo utafiti wetu umechunguza na kueleza athari ya urudiaji katika diwani husika.

Ndumbu (2013) alizungumzia takriri na sitiari katika Utenzi wa Rasi'lghuli katika kufanikisha kazi ya mshairi kifani akitumia uhakiki wa kimuundo. Alieleza na kufafanua dhana za istiara na takriri pamoja na aina za kila moja huku akitoa mifano. Uchanganuzi wake ulijikita katika ushairi wa kijadi ambapo ameeleza namna mshairi alivyotumia mbinu hizi kufanikisha kazi yake. Hakueleza namna mtindo wa mshairi unavyoathiri maana katika shairi hilo la kimapokeo bali alijikita katika kubainisha jinsi ambavyo mbinu hizo zinatumika kuunda kazi nzima. Hata hivyo, katika utafiti wetu tumeangazia ushairi huru tukichunguza urudiaji kama suala la kimtindo na namna urudiaji huu, kupitia katika aina zake, unavyotumiwa na washairi kuwasilisha maana na kukuza dhamira. Uchanganuzi wetu ni wa kimitindo ili kubainisha namna mshairi anavyotumia lugha kwa upekee hivyo kudhihirisha ubunifu wake.

Tafiti na makala yaliyoandikwa kuhusu ushairi wa kisasa kama vile uhakiki wa diwani ya *Fungate ya Uhuru* iliyoandikwa na Venance (2013), yaliangazia mashairi ya kisasa yenye urudiaji na kubainisha namna maneno yalivyorudiwa. Alijikita katika kiwango cha neno pekee bila kutazama urudiaji wa ruwaza mbalimbali za sentensi. Aidha, alibainisha baadhi ya maneno yaliyorudiwa bila kuchunguza wala kutathmini jinsi urudiaji wa maneno hayo unavyowasilisha maana katika mashairi hayo. Hakushughulikia uwasilishaji wa maana ya maneno yaliyorudiwa. Utafiti wetu umelenga kueleza vipengele vya urudiaji na kubainisha namna vinavyotumika katika uwasilishaji wa maana. Tumedhihirisha dhima na athari ya urudiaji kwa kujikita katika diwani za *Dhifa* na *Vifaru Weusi*. Uchanganuzi wetu ni wa kinadharia, tofauti na wake ambao haujatumia msingi wowote wa kinadharia.

Mueller (2015) alifanya uchunguzi wa kimitindo wa matumizi ya urudiaji katika mashairi ya lugha ya Kiestonia ( Estoniana poetry). Katika utafiti wake, alibainisha urudiaji kama dhana inayotumiwa na mshairi kuleta athari ya kimvuto. Alionyesha kwamba mshairi anapopanga silabi, maneno na sentensi kwa kuzirudiarudia huwa ana kusudi la kuleta mvuto fulani wakati shairi linapowasilishwa kwa mpokeaji kwa kuimbwa au kukaririwa. Mvuto huu unatokana na mapigo ya sauti yenye kuleta mahadhi fulani.

Mueller anadhihirisha kwamba ubunifu wa mshairi na urudiaji ni mambo mawili ambayo hayawezi kutenganishwa. Hii ni kwa sababu urudiaji ni dhana ya kimtindo ambayo mshairi huweza kutumia kuonyesha upekee wake katika ubunifu ili kuwasilisha maana kwa njia inayovutia hadhira. Hivyo basi anauona urudiaji kama chombo halisi cha kuleta mvuto

unaohitajika na mpokeaji wa shairi. Mtazamo wake ni tofauti sana na wetu katika utafiti huu kwani tumechunguza urudiaji kama dhana ya uwasilishaji wa maana na namna maana hiyo inavyosisitizwa katika viwango mbalimbali vya urudiaji. Utafiti wetu umeutazama urudiaji kama mbinu ya kimtindo ambayo mshairi hutumia kuwasilisha maana na kwamba kilicho muhimu katika urudiaji ni athari ya kimaana inayojitokeza katika kazi husika.

## 1.8 Msingi wa kinadharia

Katika uchanganuzi wetu, tumetumia Nadharia ya Umitindo iliyoasisiwa na Leech (1969). Alishughulikia mtindo kama njia mojawapo ya kutathmini kazi za fasihi. Leech (1969: 2) anasema kwamba umitindo ni uchanganuzi wa mtindo katika kazi ya fasihi au namna lugha inavyotumika katika fasihi. Anasisitiza kwamba uchanganuzi wa kimitindo unahusisha muktadha; kipindi fulani cha utunzi, mtindo fulani na shairi fulani. Mtunzi wa shairi lolote huwa na mtindo wake wa kipekee. Katika fasihi andishi, mtindo ni mazoea ya mwandishi: namna mwandishi anavyoeleza masuala na changamoto za jamii kwa kutumia lugha kwa upekee ambao unamtambulisha kama mwandishi fulani na kumtofautisha na mwandishi mwengine. Mtindo wa mwandishi ni yeye mwenyewe na jinsi anavyojieleza katika kazi nzima ya fasihi. Mashairi yanayotungwa huweza kuchunguzwa kimtindo kwa kuangazia muktadha wa utunzi wa mashairi hayo.

Leech ( 1969: 5-6) anasisitiza kwamba mambo mengi yanayozingatiwa katika fasihi yanatokana na masuala ya matumizi ya vinyume, taswira na jazanda ambazo asili yao ni lugha ya nyongeza ya kawaida na huweza kuhakikiwa kutokana na namna mtunzi mwenyewe anavyozitumia. Istilahi ambazo hutumika katika kuchanganua na kuzihakiki kazi za fasihi kama vile istiara, taswira, kinaya, usambamba na jazanda haziwezi kutazamwa wala kufafanuliwa bila kuingilia masuala ya isimu.

Kulingana na Leech, kanuni za lugha ndizo zinazotumiwa kimtindo kuendeleza istilahi hizi katika utunzi ikizingatiwa kwamba wasanii wawili wanaweza kutumia taratibu moja ya lugha ile ile lakini mitindo yao ya kujiendeleza ikawa tofauti. Anasema kwamba umitindo au elimumitindo ni uhakiki na ufasiri wa matini katika mitazamo ya kiisimu. Ni taaluma inayofungamanisha uhakiki wa kazi za fasihi na isimu.

Sifa nyingine anayotoa Leech kuhusu nadharia hii ni kwamba umitindo pia unahusu matumizi ya dayolojia, mazungumzo ambayo yanahusisha lafudhi, lahaja, rejista au sajili, lugha elezi na masuala ya sarufi kama vile sauti na urefu wa sentensi. Baadhi ya masuala haya hujitokeza katika usemaji. Umitindo, kama mkabala wa kuchanganua matini ya fasihi unategemea msingi wa usemaji kwa kuchukulia kwamba matini ya fasihi ni kama sauti ya binadamu ambayo hutumika katika ushawishi wa jamii kwa mtindo fulani.

Kulingana na Leech, umitindo, hauhusu matini ya fasihi tu, bali pia kazi zozote zilizoandikwa kama vile katika nyanja za siasa, biashara, dini na tamaduni. Anaeleza kwamba umitindo pia hujaribu kubainisha kanuni ambazo zinatumika katika kueleza namna wahusika wanavyotumia lugha kuibua masuala ya jamii, utoaji na upokeaji wa maana, uhakiki wa kidiskosi na wa kifasihi.

Umitindo, kama nadharia inayotumiwa kuchanganua mtindo katika kazi za fasihi inajikita kati ya isimu na fasihi kwani sheria na taratibu za lugha ndizo zinazowekwa katika matumizi ya kifasihi ili kuibua masuala ya jamii. Msanii hutumia njia mbalimbali kuelezea matukio na njia hizi ndizo mtindo wa msanii huyo. Sifa za kimtindo katika matini ya kifasihi huchanganuliwa kwa kuongozwa na nadharia hii.

Kazi yoyote ya fasihi huwa na umbo lake na umbo hili aghalabu huwa na athari katika kiwango fulani cha lugha kwa wapokeaji wa kazi ile. Umitindo basi hujikita katika kubainisha uhusiano uliopo kati ya umbo na athari inayosababishwa na umbo hili. Akizungumzia lugha ya fasihi, Leech anasema kwamba mtindo ndicho kipengele kinachoweza kuamua athari ya matini yoyote: athari ya matini ya fasihi hupatikana kutokana na mtindo anaotumia mwandishi katika kujieleza. Anasisitiza kwamba mtindo ni jinsi mtu anavyotumia lugha, hali ambayo haijajibana tu katika fasihi bali pia kujitokeza katika usemi wowote wa kawaida ambapo mtu huweza kuchagua namna ya kuzungumza mbali na kwamba watu hawawasiliani tu katika maandishi. Hata hivyo utafiti huu haujikiti katika mtazamo wa kiusemaji.

Crystal na Davy (1969:10) wanachangia suala la lugha wakisema kwamba nadharia hii inachanganua tabia za lugha kwa lengo la kubainisha sifa maalum zinazobanwa katika muktadha maalum kutoka katika zile sifa za kijumla za kiisimu zinazotumika katika lugha. Lugha huwa na kanuni na taratibu zake na kanuni hizi za kiisimu ndizo zinazowekwa katika matumizi ya

kawaida. Hivyo basi nadharia hii huchunguza namna taratibu hizi za lugha zinavyotumika katika ushairi. Kaida za lugha zinazozungumziwa katika isimu ndizo zinazotumiwa na msanii katika kujieleza. Mawazo haya yanafungamanisha 'parole' na mtindo wa kutumia lugha kwani sheria za lugha ndizo ambazo mshairi hutumia katika utunzi kwa mtindo wake mwenyewe. Parole ni matumizi ya taratibu hizi za lugha, iwe katika usemaji au katika uandishi. Hivyo basi mtindo unahusishwa na mkabala huu wa parole kwani ni namna mtu yeyote anavyoitumia lugha yake katika mazingira fulani kuwasilisha maana.

Bradford (1997: 2) anaunga mkono wazo kwamba lugha inayotumika katika matini ya fasihi na matini ambayo si ya fasihi huweza kuwa na vipengele vinavyolingana kimtindo ila tofauti inajitokeza katika uamilifu wa matini haya. Matini ya fasihi huandikwa na msanii ambaye hufinyanga lugha kwa njia ya ubunifu ili kuteka mawazo na hisia za msomaji kuhusu masuala ya jamii. Anaitazama lugha kama njia inayotumika na wengi kutangamana na kuelezeana tajiriba zao katika mazingira mbalimbali na kwamba bila lugha, tajiriba zetu kuhusu jambo lolote huwa tuli na zenye ubinafsi katika akili zetu. Msanii anakuwa na ushawishi tu pale anapoamua kuweka lugha katika matumizi kwa mtindo wake mwenyewe. Ijapokuwa tunaweza kutumia ishara, haiwezi kuwa na athari kubwa ya kiushawishi katika miktadha mipana kama ilivyo sauti na maandishi.

Wamitila (2003:39) anachangia mawazo haya ya Leech akisema kwamba Elimu-mitindo hutumiwa kurejelea taaluma inayohusu uchunguzi na uchanganuzi wa jinsi mbalimbali za kuelezea matukio katika kazi ya fasihi. Kutokana na kijelezi hiki, matukio katika kazi ya fasihi huelezwa kwa kutumia lugha hivyo basi nadharia ya umitindo ndiyo inayotumika kuchanganua namna mshairi anavyotumia lugha ili kuwasilisha maana.

Simpson (2004: 2) kwa upande wake anasema kwamba umitindo ndicho kiini cha uhakiki wa kazi ya fasihi kwani inahusu uchanganuzi wa mtindo na mbinu za ubunifu katika uandishi. Ni njia ya uchanganuzi ambapo matumizi ya lugha hupewa uzito. Anasisitiza sana matumizi ya lugha kama namna maalum ambayo mwandishi hutumia kudhihirisha mtindo wake wa utunzi. Wanaumitindo huiona lugha kama ala muhimu na ya kipekee kutokana na uamilifu wake wa kuibua maana kimtindo.

Kimsingi wazo kuu linalojitokeza kutokana na tathmini ya wataalam hawa ni kwamba, lugha ndiyo njia ya kipekee ya kuwasilisha masuala ya jamii kwa mtindo wa msanii. Lugha huwa na kanuni na mshairi huzitumia kanuni hizo kuikuza dhamira yake. Mshairi hutumia kanuni hizi kwa upekee unaomtambulisha kama mtunzi wa aina fulani. Hivyo basi nadharia inayoweza kuchunguza namna mtunzi anavyotumia lugha kuwasilisha maana ni nadharia ya umitindo. Mshairi anaweza kufuata kanuni za lugha au asifuate kutokana na namna anavyotaka kufinyanga kazi yake. Mojawapo ya dhana muhimu katika nadharia ya umitindo ni ukiushi. Ukiushi hutumiwa kudhihirisha uhuru wa mshairi wa kuchagua kutumia lugha kwa mtindo wake mwenyewe ili kuwasilisha maana katika kazi.

Nguzo zinazozungumziwa na Leech ndizo ambazo tumetumia kama mihimili ya nadharia hii katika utafiti wetu. Kwa mujibu wa Leech, nguzo hizo zinadhihirika katika viwango vya ukiushi.

### 1.8.1 Viwango vya ukiushi katika nadharia ya umitindo

Kwa mujibu wa Leech (1969:42) lugha ya shairi huweza kukiuka sheria za lugha kwa njia nyingi. Makusudi haya yanapaswa kuchunguzwa na kutathminiwa ipasavyo. Ukiushi huu unatokana na dhana kwamba mwandishi wa kazi za kubuni ana uhuru mwingi hasa katika ushairi kuliko watumizi wengine wa lugha.

Kuna viwango tofauti tofauti vya ukuishi wa kaida za matumizi ya lugha ambavyo mhakiki sharti azingatie katika uchanganuzi wa kimitindo wa kazi ya fasihi. Anaorodhesha viwango vifuatavyo: ukiushi wa kileksia au kimsamiati, kisarufi, kilahaja, kisajili au rejista, kifonolojia, kigrafolojia au kimaandishi, kihistoria au kimapisi na ukiushi wa kisemantiki.

Msanii huweza kuchagua namna ya kutumia lugha kwa mtindo wake muradi akuze dhamira yake. Ukiushi ni kipengele kimojawapo cha mtindo ambacho msanii fulani huweza kutumia katika kazi yake. Huu ni uhuru alio nao mshairi yeyote. Katika utafiti huu tumejikita tu katika viwango ambavyo vinahusika na uchanganuzi wa dhana ya urudiaji katika ushairi huru kama vile kiwango cha ukiushi wa kisarufi, kisemantiki, kimaandishi, kileksia na kihistoria.

Katika utafiti wetu, tumetumia nguzo hizi kubainisha viwango mbalimbali vya urudiaji vinavyojitokeza katika diwani za *Dhifa* na *Vifaru Weusi*. Aidha, tumezitumia kubainisha dhima na athari za urudiaji katika diwani husika. Viwango hivyo ni kama ifuatavyo:

## 1.8.2 Kiwango cha ukiushi wa kisarufi

Kiwango hiki ni msingi katika udhibiti wa matumizi ya lugha hasa kupitia kwa matamshi, mofonolojia na sintaksia. Mofolojia ni kiwango cha lugha ambacho kinajihusisha na miundo ya maneno ilhali sintaksia inashughulikia mipangilio na ruwaza za sentensi huku ikibainisha umuhimu wao katika kueleza maana. Leech anaeleza kuwepo kwa miundo nje na miundo ndani ya mipangilio ya lugha. Ijapokuwa haangazii tofauti iliyopo kati ya vijenzi hivi viwili vya maana, anasema kwamba umbo ndani linahusu maana ya sentensi ilhali umbo nje huhusiana na jinsi sentensi inavyotamkwa.

Kazi ya fasihi hujikita katika maana ambayo hujitokeza tu baada ya kuisoma kazi fulani. Maana hiyo inajitokeza kutokana na namna mtunzi anavyotumia lugha kwa ubunifu. Umbo ndani huweza kuhusishwa na semantiki kutokana na uwakilishaji wake wa maana katika shairi. Utafiti wetu unahusu umbo ndani ambalo linasheheni mtindo wa kutumia lugha kuibua maana.

Kiwango hiki kinahusisha matumizi ya lugha kwa kukiuka kanuni za sarufi katika kile kinachotajwa kuwa ni kubananga sarufi, huhusisha pia dhana ya anafora ambayo ni urudiaji wa neno moja katika kila mwanzo wa mstari. Hata hivyo, Leech anadai kwamba ukiushi wa miundo ya sentensi haina athari yoyote katika namna sentensi inavyoeleweka. Muundo katika shairi unaweza kubadilishwa lakini maana ikabaki ile ile. Aidha kiwango hiki hujumuisha urudiaji wa sentensi au vifungu vya sentensi kama ilivyo aghalabu katika ushairi. Ukiushi wa kilahaja na sajili au rejista pia huhusishwa katika kiwango hiki. Mshairi huweza kuchagua kutumia lahaja yake kuwasilisha maana au akatumia maneno ambayo yanazua maana kwa kutegemea muktadha fulani. Kiwango hiki pia hujumuisha matumizi ya sentensi fupi na ndefu ambazo mshairi anaweza kurudia katika kazi yake ili kuwasilisha maana anayokusudia.

Urudiaji, kama njia mojawapo ya mitindo hubainika kutokana na namna mshairi anavyotumia maneno na ruwaza za sentensi ambazo ni sehemu ya sarufi. Tumetumia nguzo hii kubainisha viwango vya urudiaji wa maneno na miundo mbalimbali ya kisintaksia kama vile virai na vishazi. Nguzo hii imetusaidia kutambua maneno yaliyorudiwa na ruwaza za sentensi

zilizorudiwa katika diwani za *Dhifa* na *Vifaru Weusi*. Kwa kuwa nguzo hii pia inahusisha matumizi ya sentensi fupi na ndefu, tumebainisha sentensi hizi na kutambua namna zinavyorudiwa katika diwani hizi.

### 1.8.3 Kiwango cha semantiki

Kiwango hiki ni cha maana ambacho kinahusishwa na matumizi ya lugha kitamathali. Ni matumizi ya lugha kwa njia inayoathiri maana kwa namna fulani hasa kutokana na maneno au vifungu ambavyo si vya maana ya kawaida. Mtunzi huweza kutumia maneno ambayo maana yao hayapatikani moja kwa moja katika kamusi ila mpokeaji anapaswa kufikiria zaidi ili kuelewa maana iliyokusudiwa. Hii inaweza kutokana na uhusiano uliopo kati ya neno fulani na mazingira yanapotumiwa neno hilo.

Sentensi yenye maana inaundwa kutokana na maneno mbalimbali na maana ya kila neno huchangia katika maana nzima ya sentensi. Tunapozungumzia urudiaji tunafikiria kuhusu maneno na vifungu vya maneno kama vile virai na vishazi. Kila neno huwa na uamilifu wake katika kirai au kishazi fulani kinachotumika katika shairi. Maana fiche inadhihirika kutokana na matumizi ya tamathali za usemi, kejeli, ukweli- kinzani na istiara. Mbinu hizi huvutia mpokeaji mbali na kuonesha ubunifu uliopo katika kazi ya sanaa. Katika uchanganuzi wa kimitindo, matumizi ya lugha hupewa uzito zaidi ili kudhihirisha ubunifu wa mshairi.

Vilevile kiwango hiki kinahusisha matumizi ya jazanda na taswira kama mbinu za kimtindo katika uandishi ambayo msanii hutumia kuibua masuala ya jamii kwa namna inayomtambulisha kama mwandishi wa kipekee. Umitindo hujikita katika kubainisha uhusiano uliopo kati ya umbo na athari inayosababishwa na umbo hili. Kila mtindo ambao mshairi hutumia huleta athari ya kimaana kwa mpokeaji.

Hivyo, urudiaji una athari za kimaana ambazo nguzo hii ya nadharia ya umitindo umetusaidia kubainisha. Maana inayopatikana katika umbo la ndani la shairi hutokana na jinsi mshairi mwenyewe anavyotumia ubunifu wake wa lugha. Maana ya kitamathali au maana ya ndani hutokana na namna mshairi anavyoteua tamathali zenyewe kwani kila mshairi huwa na mtindo wake wa kuteua tamathali. Maana hizi zinaweza kurudiwa katika shairi hata kwa kutumia visawe vyao. Nguzo hii imetusaidia kubainisha maana za kitamathali zinazorudiwa na athari zao katika kuwasilisha maana katika diwani teule.

### 1.8.4 Kiwango cha kimaandishi au grafolojia

Hiki ni kiwango ambacho kinahusisha lugha inavyotamkwa na kuandikwa katika viwango vya fonetiki, fonolojia na grafolojia. Kila kazi ya fasihi andishi huwa katika maandishi yenye mipangilio mahususi ya abjadi ili yaweze kueleweka vyema na wanaolengwa. Katika shairi sauti, silabi na maneno yanaweza kuchimuzwa kwa kiwango fulani na kwa kutegemea mtindo anaoegemea msanii ili aweze kukuza dhamira yake. Kiwango hiki huhusisha ukiushi wa matamshi ya maneno, matumizi ya herufi kubwa au ndogo, matumizi ya maandishi ya mlazo na alama za uakifishaji.

Ijapokuwa grafolojia ina uhusiano na fonolojia kutokana na masuala haya ya kisauti, ina kanuni na ruwaza zake ambazo zinajisimamia katika maandishi. Hii haimaanishi kwamba ushairi andishi hauna umuhimu katika uwasilishaji wa ujumbe kimatamshi kutokana na kile anachosema Leech (1969: 39) kwamba athari za kisauti zinaweza kudhihirika katika akili ya msomaji kwa njia sawa anaposoma shairi kimoyomoyo au anapolisoma kwa sauti.

Washairi huweza kutumia urudiaji sahili katika kazi zao. Urudiaji huu unajumuisha sauti za lugha kama vile irabu na konsonanti na mifumo ya vina katika ushairi wa kimapokeo au ushairi wa kisasa. Kwa mujibu wa Wamitila (2008: 486) urudiaji wa mfumo wa vina haupatikani tu katika ushairi wa kimapokeo bali hata katika mashairi huru. Urudiaji wa vina ni muhimu sana kwani huweza kujenga wizani katika shairi.

Kutokana na uhuru alio nao mshairi, anaweza kubadilisha mipangilio ya silabi au sauti katika neno kimakusudi na akaurudia mpangilio huo katika shairi. Nguzo hii imetusaidia kubainisha namna mabadiliko haya ya kisauti yalivyorudiwa na dhima yake katika uwasilishaji wa maana. Aidha nguzo hii imetusaidia kubainisha maneno yaliyochimuzwa au yaliyo na uziada katika diwani za *Dhifa* na *Vifaru Weusi.*

### 1.8.5 Kiwango cha kileksia

Hiki ni kiwango cha ubunaji ambapo mshairi anaweza kubuni maneno akayatumia kuwasilisha ujumbe kwa mtindo anaotaka. Hali hii ni uamuzi wa kipekee wa mshairi katika kuteua maneno kutokana na uwezo wake wa kubuni na tajiriba yake katika usanii. Maneno haya hutumika tu katika miktadha ya shairi fulani. Sifa ya lugha ambayo ni muhimu katika kiwango hiki ni kwamba maneno fulani yanaweza kubuniwa na kadiri yanavyotumika na wengi na kuzoeleka

katika jamii basi hukua hivyo kukiuka ule ubinafsi wa ubunaji. Huu ni mkabala wa isimu ya jamii ambayo ni matumizi ya lugha kwa kutegemea jamii na muktadha. Fasihi vilevile ni kioo cha jamii na lugha inayotumika kuakisi masuala ya jamii inapaswa kueleweka vyema na wanajamii ambao ndio wamiliki wa lugha yenyewe.

Leech anasema kwamba katika shairi kuna maneno (hasa yanayotokana na unyambuaji) yanayoundwa ambayo yamezoeleka sana kiasi kwamba yanaweza kuzingatiwa tu kama maneno ya kawaida na hata yakitumika katika kuzua taswira hayawezi kumtia mpokeaji wasiwasi wowote wa kutoelewa maana kikamilifu. Maneno haya huweza kutumika katika virai na vishazi yakarudiwa kimuundo ili kuzua maana. Tumetumia nguzo hii kubainisha maneno yaliyobuniwa na washairi wakayarudia katika kazi zao na athari ya maneno hayo katika kuwasilisha maana katika diwani teule.

**1.8.6 Kiwango cha kihistoria**

Uhuru wa utunzi wa mashairi huweza kwenda hata zaidi ya mipaka ya lahaja na sajili. Jinsi msanii alivyo na uhuru wa kutumia lugha ndivyo alivyo na uhuru wa kutumia lugha bila kufungwa katika kipindi chake cha kihistoria. Hii inamaanisha kwamba anaweza kuzungumzia masuala ya zamani au ya kisasa ila jambo la muhimu ni kufahamu fika historia ya lugha yake anayotumia kuwasilisha ujumbe na kwamba lazima awe mwanafilolojia ( philologist) na anayeweza kupata mwamko kutokana na watunzi waliotangulia.

Kwa mujibu wa Leech, uchanganuzi wa kimtindo wa kazi husika hufanywa kwa njia yenye utaratibu wa kitaalamu kwa kuangazia lugha ya mtunzi, kipindi fulani cha utunzi, mtindo fulani na shairi fulani. Mara nyingi mshairi anapotumia lugha hujikita katika kipindi fulani cha kihistoria au kipindi cha mabadiliko ya kimtazamo.ya mshairi. Nguzo hii itatusaidia kutambua historia ya washairi husika kwani huweza kusaidia kufahamu mitindo yao ya kutumia lugha na dhamira ambayo aghalabu huibuliwa katika kazi zao. Kuna washairi ambao hutambulika kutokana na namna wanavyotumia lugha au dhamira wanazoibua katika kazi zao. Aidha, mabadiliko ya kimtazamo humfanya mshairi kutambulika kama mwanamapokeo au mwanamapinduzi kwa kuzingatia arudhi au la. Nguzo hii pia imetusaidia kuchunguza mtindo wa shairi husika na kutambua ikiwa mshairi ameathirika na kipindi cha kihistoria au mabadiliko ya kimtazamo.

## 1.9 Mbinu za utafiti

### 1.9.1 Sampuli

Tumeviteua vipengele vyote vya urudiaji kutokana na yale ambayo tumesoma katika diwani za *Dhifa* na *Vifaru Weusi*. Vipengele hivyo ni kama vile urudiaji sahili, urudiaji wa kimaumbo na urudiaji wa kimuundo. Tumetumia hivi kupata data muhimu.

### 1.9.2 Ukusanyaji wa data

Tumezisoma tasnifu, vitabu na majarida mbalimbali yanayohusiana na urudiaji katika ushairi ili kupata data ya kimsingi. Tumepata data kuu kwa kuzisoma diwani za *Dhifa* na *Vifaru Weusi*.

### 1.9.3 Uchanganuzi wa data

Katika utafiti huu wa kimaktaba, data ambayo tumekusanya imechanganuliwa kulingana na malengo ya utafiti kwa kuongozwa na nadharia.

### 1.9.4 Uwasilishaji wa matokeo

Matokeo ya data yamewasilishwa katika sura sita zifuatazo: sura ya kwanza inahusu usuli, sura ya pili inaeleza aina mbalimbali za urudiaji kwa kuweka msingi wa urudiaji kama mbinu, sura ya tatu imebainisha aina za urudiaji katika diwani ya *Dhifa*, sura ya nne imebainisha aina za urudiaji katika diwani ya *Vifaru Weusi*, sura ya tano imebainisha dhima na athari za urudiaji katika diwani zote mbili na sura ya sita ambayo ni sehemu ya hitimisho.

## 1.10 Hitimisho

Sura hii inahusu masuala ambayo yanajenga mada tuliyodhamiria chini ya mipaka na upeo wa nadharia ya umitindo na mashairi katika diwani za *Vifaru Weusi* na *Dhifa*. Tumeainisha madhumuni wazi ya utafiti huu na kutoa maelezo kuhusu kilichotuchochea kuchanganua urudiaji katika mashairi ya kisasa. Tumetambua mbinu ya uruduaji kama suala muhimu la kimtindo linalotumika kuwasilisha maana na kukuza dhamira. Kwa kuangazia urudiaji na aina zake mbalimbali, tumeliziba pengo la kitaaluma katika uchanganuzi wa ushairi. Katika pendekezo hili tumedhihirisha namna tulivyoteua vipengele vya urudiaji na kukusanya data kutokana na usomaji wa diwani tulizoteua, vitabu, tasnifu na majarida yaliyo na uhusiano na urudiaji katika ushairi. Tumeeleza namna ambavyo tumechanganua data hizo, kuzifafanua na kuzitolea mifano mwafaka na hatimaye kuwasilisha matokeo kimaelezo. Pendekezo hili ndilo linalojenga msingi uliotusaidia pakubwa kufaulu katika utafiti huu.

# SURA YA PILI

# MSINGI WA URUDIAJI

## 2.1 Utangulizi

Katika sura hii, tutaweka msingi wa dhana nzima ya urudiaji kama sehemu ya kimsingi kabisa ya uchanganuzi wetu. Katika kazi za fasihi, kuna vipengele vingi vya urudiaji ambavyo msanii anaweza kutumia kuikuza dhamira yake. Tumetoa maelezo kuhusu aina mbalimbali za urudiaji kwa kujibana katika vipengele ambavyo tumetumia katika uchanganuzi wa diwani za *Dhifa* na *Vifaru Weusi.*

## 2.2 Dhana ya urudiaji

Wataalam mbalimbali wametoa maelezo kuhusu maana ya urudiaji. Kwa mujibu wa Galperin (1971: 211), urudiaji ni dhana inayolenga msisitizo wa kimantiki ambao ni muhimu katika kuvuta umakinifu na hisia za msomaji kuhusu neno linalorudiwa. Mtaalamu huyu anaibua wazo la umantiki akidai kwamba ruwaza zozote zinazorudiwa katika shairi lazima ziwe na mantiki ili msisitizo uweze kujitokeza kwa njia inayoeleweka barabara kwa msomaji. Umakinifu na hisia za msomaji unavutwa tu ikiwa viwango vinavyorudiwa vina maana zinazoeleweka.

Msokile (1993: 60) anatoa maelezo ya kijumla kuhusu urudiaji akisema kwamba takriri ni marudiorudio ya sauti, silabi, neno, sentensi, wazo au ridhimu ili kuleta athari kwa msomaji wa shairi linalohusika. Anasema kwamba hii ni njia ya kuonyesha hisia nzito katika shairi. Mawazo haya yanachukulia kuwa urudiaji na takriri ni visawe kwa sababu kukariri jambo ni kulirudia jambo hilo. Anasisitiza kwamba mshairi anapotumia takriri, hudhamiria kuleta athari kwa msomaji kuhusu masuala yanayozungumziwa.

Kulingana na Mclin (1996: 293), urudiaji ni kutumia neno, ruwaza za sentensi au wazo lile lile zaidi ya mara moja ili kuleta msisitizo ama athari fulani mahususi. Kutokana na maelezo haya, viwango vinavyohusika katika urudiaji ni neno, ruwaza za sentensi na maana. Hata hivyo, kijelezi chake hakitoi maelezo kuhusu sauti na silabi ambazo pia ni muhimu sana katika kuibua hisia za msomaji wa shairi.

Kwa mujibu wa Wamitila (2003: 307), urudiaji ni hali ya kusema jambo mara kadha wa kadha na kimsingi hukusudiwa kuhakikisha kwamba msomaji ameyakumbuka mambo fulani. Anasema kwamba urudiaji hutumika katika kazi bunilizi kuviunga vipengele muhimu vya msuko kuleta ruwaza fulani. Kutokana na maelezo yake, mshairi anapolirudia jambo fulani mara kadhaa huwa anamlenga msomaji aweze kukumbuka mambo ambayo yanazungumziwa. Anasisitiza kwamba urudiaji huu hufanywa kwa makusudi ya mshairi ili kuleta ruwaza ya kipekee ambayo inaweza kusaidia kulisisitiza na kuliweka jambo fulani wazi. Katika uhariri wake, Wamitila (2005:18) anayakuza mawazo haya akisema kwamba urudiaji huibua hisia fulani katika akili ya msomaji mbali na kusaidia sana katika kuimarisha kumbukiko na kujenga wizani.

Kutokana na uchunguzi wa maelezo ya wataalam hawa, hivyo basi, urudiaji ni dhana katika ushairi ambayo huleta msisitizo wa kimantiki inayohusisha matumizi ya sauti, silabi, neno na ruwaza za sentensi zaidi ya mara moja kimakusudi ili kuibua hisia, kuleta umakinifu na athari ambayo msomaji anaweza kukumbuka. Urudiaji hutilia mkazo masuala yanayozungumziwa katika shairi.

## 2.3 Aina za urudiaji

Kuna aina mbalimbali za urudiaji katika kazi za kibunilizi. Hata hivyo, katika ushairi, urudiaji hutokea kwa njia maalum ambapo baadhi ya urudiaji unaweza kuchimuzwa tofauti na kazi nyinginezo za kifasihi. Kuna urudiaji wa sauti, silabi, neno, vifungu na miundo. Aina hizi za urudiaji zinaweza kuwekwa katika kategoria nne kuu ambazo ni urudiaji sahili, urudiaji wa kimaumbo, urudiaji wa kimuundo na urudiaji wa kibalagha.

### 2.3.1Urudiaji sahili

Kwa mujibu wa Wamitila (2008: 486), urudiaji sahili ni urudiaji ambao unaweza kuelezwa kuwa ni mwepesi au ulio rahisi kutambulikana. Urudiaji huu unaweza kujumuisha sauti, silabi au maneno. Urudiaji sahili unajitokeza katika maneno mengi na matini nyingi hivyo kuweza kutambulika kwa urahisi. Mshairi huweza kutumia urudiaji huu kuonyesha mtindo wa kipekee wa kuwasilisha maana katika ushairi. Usahili wa urudiaji unatokana na uwezo wa mpokeaji kutambua kwa urahisi, ishara za lugha zinazoradidiwa hata kwa kutazama tu umbo la nje la shairi husika. Kwa mfano, mpokeaji huweza kutambua moja kwa moja, neno au sauti

zinazoradidiwa katika kifungu cha shairi na hana haja ya kuchunguza kwa undani ili kutambua sehemu iliyotokea urudiaji huo. Aidha, urudiaji huu ni sahili kwa kuwa unatokea katika maeneo mengi na matini za kila aina.

### 2.3.2 Urudiaji wa irabu na konsonanti

Urudiaji huu ni wa kisauti ambapo irabu na konsonanti hutumiwa zaidi ya mara moja katika neno. Hiki ni kiwango cha kifonolojia ambapo sauti za lugha hurudiwa au hukaririwa ili kuleta hisia fulani. Huu ndio msingi wa kuwepo kwa *takriri irabu* na *takriri konsonanti*. Takriri irabu inatokea pale ambapo sauti inayorudiwa ni irabu ilhali takriri konsonanti hutokea pale ambapo sauti inayorudiwa ni konsonanti. Urudiaji wa aina hii unapotokea katika ushairi huleta athari kubwa katika kusisitiza maana na kuikuza dhamira ya mshairi.

### 2.3.3 Urudiaji wa silabi

Silabi ni sehemu ya neno inayoundwa na konsonanti na irabu au irabu peke yake na kutamkwa pamoja kama fungu moja la sauti. Kwa mfano, *' i'* na *' ba'* ni silabi mbili tofauti ambazo zinaunda neno *'iba'*. Urudiaji huu unapatikana katika ushairi pale ambapo silabi imerudiwa katika maneno. Silabi zinaweza kurudiwa mwanzoni au mwishoni mwa kila mstari hasa ikiwa shairi ni la kimapokeo. Hata hivyo, mashairi huru pia huweza kuwa na silabi ambazo zinarudiwa katika mistari na vifungu.

### 2.3.4 Urudiaji wa neno

Urudiaji huu hutokea pale ambapo msamiati au neno fulani limerudiwa katika kifungu. Aidha, badala ya kutumia neno hilo maalum zaidi ya mara moja, kisawe chake kinaweza kutumika hivyo tukawa na urudiaji wa visawe. Maclin (1996: 147) anasema kwamba urudiaji wa neno lile lile unaweza kudhoofisha maana na hivyo basi visawe vyake vinaweza kutumika wakati mwingine. Urudiaji huu wa visawe vya maneno ni wa kimakusudi ili kupunguza uziada mwingi katika shairi. Urudiaji wa maneno ni njia maalum ambayo mshairi hutumia kuwasilisha maana ikizingatiwa kwamba kila neno linalotumiwa katika tungo hubeba maana.

## 2.4 Urudiaji wa kimaumbo

Urudiaji huu ni wa kiwango cha kimofolojia ambapo mzizi wa neno fulani ndio unaorudiwa. Neno linaponyambuliwa au kuambishwa, viambishi huongezwa katika mzizi wa neno. Sehemu hii ya kimofolojia ambayo huongezewa viambishi ndiyo inayoradidiwa katika minyambuliko tofautitofauti. Urudiaji huu pia unahusisha takriri ya neno kwa kulenga fahiwa za neno hilo. Kiwango hiki hujumuisha pia urudiaji wa viunganishi na virai au vishazi ambavyo vina urefu sana hasa katika vipande vya shairi vinavyopatikana katika mashairi ya kimapokeo. Katika mashairi haya, kibwagizo huchukuliwa kama umbo linalirudiwa. Hata hivyo mashairi huru hayana vibwagizo bali yanaweza kuwa na umbo linalorudiwa mwishoni mwa vifungu kwa njia isiyotabirika kwa urahisi kama ilivyo katika mashairi ya kiarudhi. Maumbo hayo yanaporadidiwa katika ushairi, maana katika umbo lenyewe husisitizwa ili mpokeaji aweze kuelewa uzito uliopo katika suala linalozungumziwa.

## 2.5 Urudiaji wa kimuundo

Urudiaji huu hutokea pale ambapo muundo fulani wa kirai, kishazi au sentensi umerudiwa. Urudiaji wa aina hii ndio unaoitwa usambamba. Ni urudiaji ambapo jambo moja hurudiwa kwa maneno tofauti. Katika ushairi, lugha huweza kutumiwa kuleta uziada ambao unaweza kudhoofisha maana. Hivyo basi njia mojawapo ya kuuondoa uziada huu ni kutumia miundo tofautitofauti ya urudiaji. Dhana ambayo hutumiwa kuelezea urudiaji huu wa kimuundo ni usambamba.

Wamitila (2003:309) anasema kwamba usambamba ni mbinu ambapo msanii anayarudia maneno fulani au maana fulani kwa muundo mwingine tofauti. Anasisitiza kuwa urudiaji huu huweza kujitokeza katika viwango tofauti kama vya vipashio vya kisintaksia, virai, vishazi na sentensi. Viwango hivi huweza kupangwa kwa namna ambavyo inaleta maana sawa. Hii ina maana kwamba urudiaji huu unalenga kurudia maana kwa kutumia miundo tofauti.

Wales (2011:302) naye anadokeza kwamba usambamba ni urudiaji wa ruwaza sawa za sentensi ambao mara nyingi unahusisha virai na vishazi. Anasema kwamba, kawaida kuna uhusiano wa kimaana katika ruwaza zinazorudiwa. Hata hivyo si lazima ruwaza hizo ziwe na muundo sawa au usinonimia bali zinaweza hata kuwa na uantonimia au kauli zinazokinzana.

Kimsingi, usambamba ni aina ya urudiaji wa kimuundo ambapo ruwaza za sentensi zinazohusisha virai na vishazi hurudiwa kwa kutumia miundo tofauti ili kusisitiza maana. Unahusisha vishazi au sentensi ambazo zina ruwaza sawa na hutokea pale ambapo ruwaza za sentensi zimerudiwa katika shairi.

Kwa kutumia miundo tofauti, mshairi anaweza kupunguza uziada kama Leech anavyonukuliwa na Wales (2011: 302) akisema kwamba usambamba ni uchimuzi uliodhibitiwa kimuundo. Hii ina maana kwamba usambamba hutumia miundo ya vifungu vya maneno kuunganisha mawazo yanayofanana hivyo kupunguza uchimuzi wa mawazo hayo. Miundo hii tofautitofauti hudhihirika kutokana na aina za usambamba. Usambamba ni dhana muhimu sana katika uwasilishaji wa maana kwa kuwa, mbali na kuisisitiza na kuhakikisha uwazi wa maana, ni njia bora sana ya kuendeleza masuala yanayokinzana. Mshairi hutumia usambamba kupanga mawazo na kuonyesha namna mawazo hayo yanavyohusiana kwa muwala mzuri hivyo kuleta uelewekaji na ukumbukaji wa maana ambao huchangia pakubwa katika kuendeleza dhamira. Kuna aina mbalimbali za usambamba ambazo mshairi anaweza kutumia katika utunzi wake.

## 2.6 Aina za usambamba

Kuna aina tofauti za usambamba ambazo tumejadili katika sehemu hii kama vile usambamba wa kisintaksia, kivisawe, kitanakuzi, kisemantiki au kimaana, kifahiwa, kidhamira, kimuundo na kiwizani.Wamitila (2008:490 - 494) anaeleza aina hizi za usambamba.

### 2.6.1 Usambamba wa kisintaksia

Sintaksia ni kiwango cha lugha ambacho kinashughulikia muundo wa sentensi na elementi nyingine zinazounda sentensi kama vile kategoria za maneno, vikundi na vishazi. Kwa kujikita katika sheria za uundaji wa sentensi, kiwango hiki cha lugha huchunguza namna sentensi zinavyoundwa. Sheria hizi ndizo zinazotumika katika utungaji wa sentensi za kazi bunilizi. Hata hivyo, sheria hizi zinaweza kukiukwa na mshairi kimtindo kutokana na uhuru walio nao washairi katika kutumia lugha. Miundo ya kisintaksia inaweza kukiukwa kwa kutegemea mtindo ambao mshairi anadhamiria kutumia kuwasilisha maana na kuikuza dhamira yake.

Usambamba wa kisintaksia ni urudiaji wa muundo wa kisintaksia. Hali hii hutokea pale ambapo vipashio vya kisintaksia kama vile virai na vishazi vinarudiwa kwa kutokea pale pale. Hii inamaanisha kwamba muundo fulani wa kisintaksia huweza kutokea katika mstari fulani wa shairi na likarudiwa katika mstari mwingine au katika mstari huo huo kwa kuchukua nafasi ile ile. Aidha, mahali ambapo muundo fulani umedondolewa, mpokeaji huweza kuutia akilini katika usomaji wake. Muundo uliodondolewa ndio ambao aghalabu hurudiwa katika nafasi ile ile ili kuepusha uziada mwingi. Mshairi anapoutumia usambamba huu, huwa analenga kusisitiza maana fulani kwa njia ya kipekee bila kutokea kwa uziada wa muundo husika. Kwa kufanya hivyo, maana inayowasilishwa huwa imesisitizwa.

### 2.6.2 Usambamba wa kivisawe

Usambamba wa aina hii hutokea pale ambapo wazo au jambo lile lile limerudiwa kwa maneno mengine. Usambamba huu ni urudiaji wa wazo ambalo limekwisha kutajwa katika sehemu fulani ya mstari wa shairi kwa kutumia maneno mengine yaliyo na maana sawa na wazo la kwanza. Kwa mfano, 'hakuna tajiri kwenye sherehe' kisha mstari wa pili ukawa, 'hakuna mkwasi kwenye hafla.' Kutokana na mfano huu, kirai, 'tajiri kwenye sherehe' ni sawa na 'mkwasi kwenye hafla.' Wazo linalojitokeza katika mstari wa kwanza wa mfano huu ndilo lile lile linaloangaziwa katika mstari unaofuata japo kwa maneno mengine tofauti. Mshairi hutumia usambamba huu kuwasilisha maana sawa inayojitokeza katika vifungu viwili vyenye miundo tofauti.

### 2.6.3 Usambamba wa kitanakuzi

Katika aina hii ya usambamba wazo ambalo linaelezwa katika mstari uliotangulia linapingana na wazo katika mstari unaofuata. Hapa, mstari wa pili unapinga mstari wa kwanza. Mawazo mawili katika shairi hulinganishwa kwa namna ambavyo wazo moja linapinga jingine. Kwa mfano, 'msimu wenye baridi kali' na 'msimu wenye joto kali' ni miundo ya maneno ambayo yanakinzana. Katika mfano huu, wazo katika mstari wa kwanza linapinga lile la mstari wa pili. Vile vile, 'mchoyo kero kwa jamii' na 'karimu kipenzi cha wote.' Mistari hii miwili ina mawazo ambayo yanapingana hivyo kudhihirisha usambamba wa kitanakuzi kutokana na namna mawazo yanavyopingana. Kimsingi, mshairi anapotoa kauli fulani ambayo ni kinyume cha kauli ya

kwanza, huwa anaisisitiza tu kauli ile ya mwanzo kwa namna inavyopingana. Hii ni njia ya kipekee ambayo mshairi hutumia kurudia maana fulani katika mashairi ya kisasa.

### 2.6.4 Usambamba wa kisemantiki

Kwa mujibu wa Leech (1981: ix), semantiki ni taaluma inayochunguza maana. Anasema kwamba uchanganuzi wa maana ni muhimu sana katika mawasiliano. Hii ni kwa sababu, binadamu anapotangamana katika jamii, huwasiliana kwa kutumia lugha hivyo pana haja ya kuelewana katika mawasiliano. Katika fasihi, msanii huwasilisha maana kwa mtindo wake. Urudiaji ni moja kati ya mitindo ambayo msanii hutumia katika uwasilishaji wa maana kwa mpokeaji. Mshairi huweza kurudia maana kutumia muundo wa kisemantiki. Hivyo, usambamba wa kisemantiki hutokea pale ambapo muundo unaorudiwa unakuza maana ile ile. Hapa, mshairi hutumia muundo tofauti ambao una maana ile ile inayojitokeza katika muundo unaotangulia. Kimsingi, katika usambamba huu maana ndiyo inayorudiwa kwa kutumia miundo tofauti ya kubadilisha maneno. Usambamba huu pia huitwa *usambamba wa kimaana.* Katika usambamba huu, ruwaza za sentensi zinaweza kuwa tofauti lakini zinakuza maana moja sawa. Ruwaza hizi zinaweza kutokea katika vifungu tofauti tofauti katika shairi. Kukuzwa kwa maana moja huleta msisitizo wa suala linalozungumziwa hivyo kumfanya mpokeaji kuelewa umuhimu wa suala lenyewe. Kwa mfano, 'madhara ya dawa za kulevya yanatambulika kote' na 'madhara ya dawa za kulevya yanajulikana wazi na watu wote.' Sentensi hizi zinawasilisha maana sawa, hivyo zina muundo wa kisemantiki.

### 2.6.5 Usambamba wa kifahiwa

Katika lugha, neno fulani huweza kuwa na uhusiano wa kimaana na maneno mengine. Maana ya maneno haya huwa zinatokana na neno asili au neno linalorejelewa. Hivyo tukawa na maneno yanayokaribiana kabisa kimaana na kirejelewa kutokana na uhusiano uliopo. Maneno haya yanayokaribiana sana kimaana na kirejelewa chao ndiyo yanayoitwa fahiwa. Neno moja huweza kuwa na fahiwa moja au zaidi. Kwa mfano, neno baba linamaanisha mzazi wa kiume na lina fahiwa ya kiongozi.

Katika ushairi, usambamba wa kifahiwa hutokea pale ambapo fahiwa ile ile hurudiwa kwa muundo unaofanana. Fahiwa hii inayorudiwa huwa muhimu sana katika kuikuza dhamira ya

mshairi. Mshairi anapotumia maneno ambayo yana uhusiano wa kifahiwa na kirejelewa chao basi huwa anatilia mkazo maana ya kirejelewa hicho kilichotumika katika kuwasilisha maana.

### 2.6.6 Usambamba wa kidhamira

Katika usambamba huu, dhamira ya mshairi au wazo kuu ndilo linalorudiwa. Mshairi huweza kutumia muundo fulani mahususi kuikariri dhamira yake katika vifungu vya shairi. Wazo lile lile ambalo linajitokeza katika kifungu kimoja ndilo linalorudiwa katika kifungu au vifungu vinavyofuatia. Hivyo basi usambamba wa kidhamira hutokea pale ambapo wazo kuu linaradidiwa katika vifungu vya shairi. Aghalabu lengo kuu la mshairi yeyote ni kuhakikisha kwamba ameikuza dhamira yake kwa mtindo maalum ambao unadhihirisha upekee wake. Mshairi anapotumia usambamba wa kidhamira katika utungo wake anapania kusisitiza dhamira yenyewe. Urudiaji huu wa kimuundo hutumiwa kuwasilisha maana kwa kutilia mkazo wazo kuu katika shairi.

### 2.6.7 Usambamba wa kimuundo

Usambamba unaotokea hapa ni ule wa kurudia muundo sawa au ruwaza ya kimuundo. Kategoria fulani za maneno katika lugha zinaweza kurudiwa kwa kufuata ruwaza fulani. Hali hii inaweza kutokea katika mistari ya vifungu vya shairi. Hapa, muundo au ruwaza yenyewe ndiyo inayokaririwa wala si neno la kategoria hiyo. Kategoria mahususi ya maneno ndiyo inayorudiwa katika mistari ya shairi bila kuzichanganya. Kwa mfano, ikiwa mshairi ameamua kutumia muundo wa kurudiwa vivumishi basi anaweza kutumia aina tofauti za vivumishi. Lazima pawe na ruwaza maalum ya vivumishi katika kila mstari wa shairi.

### 2.6.8 Usambamba wa kiwizani

Msokile (1993: 120) anaueleza wizani kama mapigo maalum ambayo husaidia kujenga uzuri wa kazi ya ushairi. Wamitila (2003:352) kwa upande wake, anasema kwamba istilahi hii hutumiwa kuelezea ruwaza fulani inayorudiwa na ambayo inaakisi mwendo wa usimulizi. Hivyo, wizani ni mapigo maalum yanayoletwa na matumizi ya ruwaza fulani katika shairi.

Usambamba wa kiwizani huhusishwa na shairi la kiarudhi ambalo huzingatia mapigo ya sauti baada ya kipindi fulani. Hutokea sana katika mashairi ya kimapokeo ambayo yana mpangilio

maalum wa vina na mizani katika vipande vya shairi. Hata hivyo, hii haimaanishi kwamba mashairi huru hayana mapigo haya. Urudiaji hujenga wizani pale ambapo ruwaza fulani imekaririwa kimabadilishano ya sentensi fupi na ndefu au kifungu kirefu na kifupi au kupitia kwa ruwaza za sauti. Wizani pia huweza kupatikana kutokana na mipangilio ya kisintaksia katika shairi. Mpangilio huu maalum unaorudiwa ndio unaoleta mapigo. Kwa mfano, 'Talanta nyingi zimo'. 'Zimepita ya kipimo'. 'Hawaziki kwenye shimo'. 'Kuzikuza ndo mfumo'. Vifungu hivi vinne vina urefu na mpangilio maalum wa mizani unaoishia silabi,'mo' ambayo katika usomaji na uwasilishaji husababisha mapigo ya sauti.

## 2.7 Urudiaji wa kibalagha

Urudiaji huu unahusishwa na sanaa ya usemaji na uzungumzaji. Urudiaji ni mbinu mojawapo ambayo sanaa ya balagha hutumia kufanikisha uwasilishaji wa ujumbe. Urudiaji wa kibalagha hupatikana hasa katika ushairi. Hata hivyo, unahusishwa na ubalagha hasa kutokana na istilahi za usemaji zinazotumika. Sanaa ya ubalagha ina uhusiano mkubwa na uandishi kwani kinachondikwa katika matini huwa kinawakilisha kilichosemwa au kuzungumziwa; yaani kilichoandikwa huchukuliwa kama sauti za binadamu. Maneno ambayo yanahusishwa na ubalagha ndiyo yanayotumiwa kuelezea urudiaji huu.

### 2.7.1 Anafora

Kwa mujibu wa Wales (2011: 20), anafora ni aina ya urudiaji ambapo neno lile lile hukaririwa katika mwanzo wa kila mstari wa shairi. Anasema kuwa aina hii ya urudiaji hupatikana katika mashairi ya aina zote na huweza kutumika kuzua athari za kihisia. Si neno pekee linalorudiwa mwanzoni mwa kila mstari bali pia virai. Pia huitwa epanafora au mrejeosabiki, kama anavyotaja Wamitila (2008:494). Kwa mfano, 'Yeye ni rafiki wa dhati'. 'Yeye ni mpenzi wangu'. 'Yeye ni mama wa mtoto.' Katika mfano huu, kifungu, 'yeye ni' kimerudiwa katika mwanzo wa kila mstari.

### 2.7.2 Epifora

Urudiaji huu ni wa kinyume cha anafora ambapo neno au kirai cha mwisho wa mstari hurudiwa mwishoni wa kila mstari au kishazi au sentensi. Kirai au neno lile lile ndilo linalokaririwa katika mwisho wa kila mstari au sentensi. Epifora au mrejeotamati ni urudiaji tofauti na anafora ambayo hutokea mwishoni mwa mstari au sentensi. Kwa mfano, 'Unapokula fikiria mazingira'. 'Unapocheza fikiria mazingira'. 'Utembeapo fikiria mazingira'. Kishazi, 'fikiria mazingira' kimerudiwa mwishoni mwa kila mstari unaofuata. Urudiaji huu ni muhimu kwa kuwa vifungu vilivyoradidiwa mwishoni mwa mistari hujenga msingi wa suala linalozungumziwa. Aghalabu, maneno au vifungu ambavyo mshairi hurudia huwa ndiyo dhamira inayosisitizwa katika shairi husika hivyo kuhakikisha ukumbukaji wa suala hilo kuu.

### 2.7.3 Mrejeokuwili

Wamitila (2008: 494) anaitumia istilahi hii kuelezea urudiaji ambao unahusisha matumizi ya anafora (mrejeosabiki) na epifora (mrejeotamati). Katika urudiaji huu, aina hizi mbili za urudiaji huwa zimetumika. Ni urudiaji ambao unajumuisha ukariri wa neno au kirai fulani maalum mwanzoni mwa mstari kwa upande mmoja na ukariri wa neno au kirai kingine maalum mwishoni mwa mstari kwa upande mwingine. Hii haimaanishi kwamba neno lile lile linalorudiwa mwanzoni ndilo linalorudiwa mwishoni bali neno linalorudiwa mwanzoni ni tofauti na lile linalorudiwa mwishoni. Anafora inapotokea upande mmoja nayo epifora inatokea upande mwingine hivyo kuleta uwili. Urudiaji huu wa kuwili hutokea katika shairi moja hivyo kuitwa mrejeokuwili.

### 2.7.4 Anadiplosia

Kwa mujibu wa Cuddon (1998: 34), urudiaji huu hutokea pale ambapo neno au kirai cha mwisho wa mstari kinarudiwa mwanzoni mwa mstari unaofuatia ili kuleta athari ya kipekee. Wales (2011:18 -19) anasema kwamba urudiaji huu huweza kutumika kama kiungo maalum cha vifungu vya shairi ikitokea kwamba neno au kirai hicho cha mwisho wa mstari wa kifungu fulani kimetumika mwanzoni mwa kifungu kingine. Kimsingi, urudiaji unaotokea hapa ni ule ambao neno la mwisho au kirai cha mwisho katika sentensi ndicho kinachotumiwa kuanzia mstari au kifungu cha shairi kinachofuata.

### 2.7.5 Epanalepsia

Kulingana na Cuddon (1998:264), epanalepsia ni urudiaji ambapo neno au maneno hutokea baada ya maneno mengine kujitokeza katikati yao. Hii ina maana kwamba neno au kirai kilichojitokeza katika mwanzo wa mstari hurudiwa tu baada ya maneno mengine kutoka katika sentensi hiyo. Aidha, ni sawa kusema kuwa maneno yanayojitokeza mwanzoni mwa mstari hukaririwa mwishoni mwa mstari huo. Wales (2011: 139), ambaye pia anamnukuu Puttenham (1958) anasema kwamba epanalepsia ni mwangwi wa sauti. Hii ni kwa sababu maneno yaliyotumika mwanzoni mwa mstari hurejelewa jinsi yalivyo na kutumiwa mwishoni mwa mstari huo. Kulingana na Wales, epanadiplosia ni istilahi ambayo pia huweza kutumiwa kama kisawe cha epanalepsia.

## 2.8 Hitimisho

Katika sehemu hii tumechunguza istilahi mbalimbali zinazotumika katika dhana ya urudiaji. Istilahi hizi zinaeleza aina za urudiaji na jinsi zinavyojitokeza katika viwango tofauti kama vile kiwango cha sauti, irabu na konsonanti, neno, virai, vishazi na ruwaza za sentensi. Aina hizi za urudiaji tulizozieleza ndizo tutakazobainisha katika sura ya tatu na sura ya nne mtawalia kwa kujikita katika diwani za *Dhifa* na *Vifaru Weusi*. Tumeangazia na kuweka vigezo vya namna aina mbalimbali za urudiaji zinavyoweza kubainishwa na athari ambazo urudiaji unaweza kuibua kwa mpokeaji wa mashairi husika. Masuala ya kinadharia ambayo tumezungumzia katika sura hii ndiyo msingi wa urudiaji ambao tumechunguza katika sura zinazofuata.

# SURA YA TATU

# URUDIAJI KATIKA DIWANI YA *DHIFA*

## 3.1 Utangulizi

Katika sura hii, tumedhamiria kubainisha aina mbalimbali za urudiaji ambazo mwandishi Kezilahabi ametumia kuwasilisha maana na kuikuza dhamira yake. Viwango vya urudiaji ambavyo tumebainisha na kuonyesha jinsi vinavyojitokeza katika diwani ya *Dhifa* ni kama vile: urudiaji sahili, urudiaji wa kimaumbo, urudiaji wa kimuundo na urudiaji wa kibalagha. Tumetoa mifano mwafaka inayodhihirisha mtindo wa kipekee ambao mshairi ametumia katika kazi yake.

## 3.2 Urudiaji wa irabu na konsonanti

Fonetiki kama kiwango cha lugha kinachoshughulikia sauti ni muhimu sana katika uchanganuzi wa ushairi katika lugha ya Kiswahili. Mshairi hutumia irabu na konsonanti kuunda neno kama kipashio chenye maana. Maneno haya huunda virai, vishazi na sentensi ambazo zinatumika kuwasilisha maana hivyo kuendeleza dhamira. Kezilahabi ametumia urudiaji huu kwa kiasi fulani katika mashairi yake. Kwa mfano, katika shairi, 'Maisha' irabu na konsonanti mbalimbali zimerudiwa.

Maisha, yakikomaa, twachacharika twachachamaa
Furaha yatutambaa, twachachamka,twachanjamaa
Mifuko ikitujaa, twachachatika, twakingamaa
Kwa mwendo wa kishujaa, twachanjarika twakangamaa
Oyaa! Ongeza mwendo maisha ni basi la wazima!
Lakini,
Ulimwengu, kizaazaa, umekaa, kibaabaa
Na maisha, yapaapaa, yamejaa, hadaadaa
Binadamu, twataataa, kwa fadhaa, twakaakaa
Na twenenda, kichaachaa, kwa njaa, kigaagaa!
Sasa,
Maisha, nyondenyonde, kila saa, twaduwaaduwaa
Miguu nyakanyaka, tukikaa, 'meshupaapaa
Na kura, nyong'onyong'o 'mechakaa, 'mesinyaasinyaa
Miili, nyang'anyang'a, twazubaa, twashangaashangaa
Hae! Dunia tambara bovu asimamaye huanguka! (uk.32)

Shairi hili ni mfano mmoja wenye urudiaji mwingi wa irabu na konsonanti. Kwa mifano, irabu zote, *a, e, i, o* na *u* zimerudiwa ila irabu 'a' imerudiwa zaidi. Baadhi ya konsonanti zilizoradidiwa ni kama vile: *z, b, p, t, k, ch* na *g.* Takribani mashairi yote katika diwani ya *Dhifa* yana urudiaji huu. Hata hivyo, shairi hili teule lina mtindo na mpangilio wa kipekee wa kuleta hisia za mpokeaji kuhusu mitazamo ya maisha.

## 3.3 Urudiaji wa silabi

Silabi huweza kurudiwa mwanzoni au mwishoni mwa mstari wa shairi lolote. Urudiaji huu aghalabu unapotumiwa na mshairi, huwa analenga kuleta wizani mbali na kusisitiza suala ambalo linazungumziwa. Mshairi ametumia mfumo wa vina katika mashairi machache, ambapo amerudia silabi kwa mtindo ambao unasababisha mapigo ya sauti. Urudiaji wa silabi huweza kutumiwa kwa njia inayotabirika au isiyotabirika kwa kutegemea aina ya shairi. Silabi zinazoradidiwa katika mashairi ya kisasa hazina mtindo wa kutabirika. Silabi moja inaweza kurudiwa mwanzoni au mwishoni mwa mistari miwili au zaidi bila kufuatana kwa muundo maalum. Hii ni tofauti na shairi la kimapokeo ambapo silabi ile ile inarudiwa mwishoni mwa kila mstari katika ubeti. Mifano katika diwani hii inaonesha namna silabi zinavyorudiwa kwa nia ya kuleta mapigo fulani ya sauti.

Kwa mfano, katika shairi, 'Muungano', silabi, 'wa' imerudiwa katika mianzo ya mistari mitatu ya kwanza ya kifungu cha pili kisha silabi nyingine tofauti ikatumiwa mwanzoni mwa mistari inayofuata. Vilevile silabi 'tu' katika kifungu cha tatu imerudiwa ili kusisitiza uhusika katika wingi.

> Watemao wateme kiuficho kama wageni
> Wamezao wafumbe macho
> Watingishe vichwa, juu chini
> Kushoto kulia, mbele twendeni!...
>
> Tujadili, tukejeli, tucheke, tugeuze maneno
> Turekebishe, tuchambue
> Baada ya yote
> Tupumzike chini ya sitiari huru tata. (uk.56)

Katika shairi, 'Makaburini', urudiaji wa silabi, 'twa' pia inabainika katika kifungu cha pili. Silabi hii inaonyesha uhusika wa watu wengi ambao wanafanya kazi katika 'Bar' za matajiri. Mshairi anadhihirisha namna wanyonge wanavyotumiwa na matajiri kuzalisha mali ilhali wao hawafaidiki ipasavyo. Mbali na kuleta wizani, mshairi ameitumia silabi hiyo ili kusisitiza kwamba suala linalozungumziwa linahusu watu wengi, hivyo basi pana haja ya uhusika jumui sio wa mtu binafsi.

> Twauza Bar.
> Twanawisha mikono wateja
> Walokwisha kula mbuzi, ng'ombe, kitimoto,
> Vyote hivi na Bar vilikuwa vyenu. Twasikia tu,
> Twachoma utajiri kuzalisha utajiri. (uk.57)

Shairi lenye mada, 'PA!' ni mfano mwingine mzuri ambao unaonyesha urudiaji wa silabi. Shairi hili ni la kihisia kutokana na matumizi ya alama ya hisi katika kila silabi, 'pa'. Mshairi anazirudia hisia zake kwa sauti ya kishindo ili kudhihirisha dhamira yake katika diwani hii. Mshairi anatoa hisia zake kuhusu unafiki ambao umewagubika wananchi na viongozi wao. Katika mashairi mengi, mshairi anaelezea namna wananchi wanavyowachagua viongozi ili kuwahudumia lakini punde tu baada ya kushika hatamu za uongozi, wanasahau kutimiza ahadi walizotolea wananchi. Wananyakua mali na kuzitumia rasilimali za nchi kujinufaisha wenyewe. Hata hivyo, jambo linalosikitisha ni kwamba, badala ya kuwakemea viongozi hawa, wananchi wenyewe wanapumbazwa na kudanganywa kiasi cha kuwashangilia hata wanapojaza 'matumbo' yao na kulifilisi taifa.

> PA!
>
> Pa! Pa! Pa!
>
> ( Kimya)
>
> Pa! (uk.60)

### 3.4 Urudiaji neno

Kezilahabi amerudia baadhi ya maneno akiwa na lengo la kusisitiza ujumbe katika shairi husika. Mshairi ametumia njia mbili kuu za urudiaji wa maneno. Kwanza, ameyatumia maneno yale yale katika mistari mingine. Pili, ametumia visawe vya maneno katika mistari mingine ili kutoa maana ile ile na kwa njia fulani kujaliza au kukokoteza maana anayokusudia kuwasilisha. Hii ina maana kuwa amerudia neno fulani kwa kulipatia neno hili uwakilishaji mwingine ambao una maana sawa na neno lililotangulia. Mshairi ametumia njia hizi mbili za urudiaji neno kwa mtindo wake huku akiuendeleza katika mistari, vifungu na kutoka shairi moja haji jingine.

Kwa mfano, katika shairi la kwanza, 'Kwa Walimu Wote', neno 'mwalimu' limerudiwa katika vifungu vitatu kutokana na hali kwamba mshairi analenga kuufikisha ujumbe hasa kwa walimu, ambao ni hadhira yake. Mshairi anamzindua mwalimu aweze kutafakari na kuelewa hali wanazopitia katika kutekeleza majukumu yao. Mbali na kumkumbusha maisha yake akiwa mtoto, akiwa kijana, akiwa mtu mzima na akiwa mwalimu, mshairi anamweleza mwalimu kuhusu hali yake atakapostaafu.

Anamhimiza mwalimu kuwa angali anafundisha ana uwezo wa kupigania mshahara mzuri kutokana na majukumu mengi anayofanya shuleni. Mshauri anawazindua walimu wajitokeze kwa ujasiri na umoja ili kuboresha mustakabali wao na kuunga mkono serikali ambayo itatambua na kuthamini uzito wa kazi wanazofanya. Anaeleza kwamba njia ya kipekee ya kufanya hivyo ni kutumia kura yake kuwachagua viongozi watakaojali masilahi yao. Anasisitiza kwamba jina, mwalimu, daima litabakia kama kitambulisho chake popote aendapo. Watoto watamwita, 'Ticha' popote apitapo. Katika kifungu cha kwanza mstari wa mwisho, mshairi ametumia neno 'Ticha' kama kibadala cha mwalimu kama sehemu ya ukiushi katika kiwango cha kileksia. Mshairi amelitumia neno, 'Ticha' kimakusudi ili kudhihirisha kwamba mwalimu hutambulika na jamii nzima akiwepo mtoto ambaye hutumia neno hilo aghalabu kumwita mwalimu.

> Utakuwa kichekesho cha watoto
> Watakaokuita, Ticha! Popote uendapo.( kif. 2)

Mistari hii mitatu hapa chini inabainisha urudiaji wa neno 'mwalimu' unaotokea katika vifungu vitatu tofauti:

Nilipokuwa mwalimu nikaitwa Bure...( kif.1)
Kumbuka mwalimu utakapostaafu...(kif. 3)
Sikilizeni walimu...(kif.8), (uk.1)

Katika shairi 'Jibwa', neno jibwa limerudiwa katika vifungu vyote isipokuwa kifungu kimoja tu. Mshairi amelitumia neno jibwa kijazanda kuonyesha mtu asiye na maadili, mwizi sugu na mlafi wa kupindukia anayetumia hila zake kuhangaisha watu katika mazingira. Anasisitiza kwamba mtu wa aina hii anapaswa kupewa adhabu kali, si kwa kumrushia cheche za matusi bali kwa kuuliwa kwa kupigwa bunduki, shoka na kufugwa shingo. Mshairi anasisitiza kwamba jibwa hili ni laana kwa wananchi na anapaswa kukomeshwa, lipigwe hadi life.

Kwa mujibu wa shairi, mtunzi anateka mawazo ya mpokeaji aweze kuelewa jazanda iliyopo katika shairi zima. Mshairi amelitumia neno jibwa kama kiwakilishi cha viongozi walafi, wenye kiburi na wenye unyama ambao baada ya kuchukua hatamu ya uongozi hujali tu masilahi yao. Mshairi anawatahadharisha wananchi dhidi ya viongozi hawa na kuwahimiza 'kutowafuga' asilani bali wawaondoe ili kulinda rasilimali za nchi ambayo anataja kuwa ni 'jikoni'. Mifano ifuatayo inajitokeza katika mistari tofauti tofauti katika vifungo tofauti ambavyo vina neno jibwa linalorudiwa na kusisitizwa.

Jibwa likitoka jikoni...
Jibwa likianza kula mayai...
Jibwa jizi fisi...
Jibwa liloshika hatamu...
Dawa ya jibwa shoka...
Jibwa jizi laana...
Jibwa jizi mwalijua...(uk.5)

Katika shairi, 'Alalaye' mshairi ametumia visawe vya maneno ili kuepusha kurudia kwingi kwa neno lile lile. Maneno kama vile: wafikiri, wadhani na wahisi ambayo yametumika katika kifungu cha pili mistari ya pili, nne na sita yanatoa maana moja. Kwa mujibu wa mshairi, maneno haya matatu yana maana ya 'fikiri'. Badala ya kuliradidi neno hili, mtunzi ameamua kuteua visawe vyake almuradi maana ihifadhiwe na kupunguza uziada ambao ungeweza kutokea endapo angetumia neno lile lile. Urudiaji huu wa neno au msamiati si wa moja kwa moja kwani neno linarudiwa kupitia kwa visawe vyake ikichukuliwa kwamba kuvitumia visawe vya neno ni sawa na kulirudia neno lenyewe kwa njia ya kipekee.

Tumeona ngozi ya ng'ombe imewambwa
Wafikiri hatujuia nyama ilikokwenda
Tumeona mifupa ya kuku jalalani
Wadhani hatujui nani kafaidi
Tumeona vyombo vikisafishwa jikoni
Wahisi hatujui nani kala
Wanasema asiyekuwepo lake halipo...(uk.26)

### 3.5 Urudiaji wa kimaumbo

Umbo ni sehemu muhimu sana katika ushairi kwani hudhihirisha mwonekano wa utungo fulani kwa kutumia vipengele tofauti tofauti kama vile kiunganishi, mofimu au mzizi wa kitenzi utumiwao katika unyambuaji, fahiwa na kibwagizo. Maumbo haya hutumiwa na mshairi si kwa madhumuni ya kuunda shairi pekee bali pia kwa mtindo unaomwezesha mshairi kuwasilisha maana kwani utungo wowote lazima uwe na umbo lake. Katika diwani ya *Dhifa*, Kezilahabi ametumia baadhi ya vipengele hivi hasa umbo la kibwagizo na kiunganishi 'na'. Kwa mfano, katika shairi, 'Mafuriko', mshairi anaeleza kuhusu athari za mafuriko iliyoshuhudiwa mwaka huo na ambayo itabaki katika kumbukuku za binadamu kuweza kuwasimulia wajukuu wao. Mshairi anaeleza namna ambavyo mhusika anaandika na kutangaza kote athari za mafuriko yaliyotokea ili kutahadharisha wengine kuhusu mafuriko yoyote ambayo yanaweza kutokea baadaye. Katika kifungu cha pili na tatu, umbo lenye kirai 'mafuriko ya mwaka huu' limerudiwa ili kusisitiza athari za mafuriko yaliyotokea mwaka huo.

Mafuriko ya mwaka huu
Yatishia nyumba kongwe...
Mafuriko ya mwaka huu!
Mti mkongwe umelalia upande...
Mafuriko ya mwaka huu!
Wengi wataumbuka.(uk.4)

Katika shairi, 'Mke wa Waziri', mshairi ameliradidi umbo lenye kirai, 'wewe Monika' na 'unajua kuchekesha'. Mshairi anaeleza namna wanawake wanavyomkashifu mke wa waziri ambaye, tangu alipotoka kwao na kuolewa na waziri anawadharau na kujigamba pasipo kuelewa maisha yake ya awali. Wanawake hawa wanazungumzia maisha ya awali ya waziri huku wakirejelea utotoni na kuyalinganisha na hali yake ya sasa ambapo anajitapa na kuwapuuza

watu. Wanawake hawa wanamwashiria mke wa waziri na waziri mwenyewe na kuwaajabia sana. Mshairi ameteua neno 'chekesha' akisema kwamba waziri na mkewe wanajua 'kuchekesha' akimaanisha kuwa ni watu wanaoshangaza sana. Msisitizo upo hasa kwa Monika, ambaye ni mke wa waziri.

> Wewe Monika…
> Ulitoka kwetu bila ushanga kiunoni…
> Unajua kuchekesha
>
> Sikiliza Monika…
> Wewe Monika
> Twende ufukweni kuogelea
> Tuone hiyo cheni ya dhahabu
> Mnajua kuchekesha
>
> Monika sikiliza…
> We Monika!...
> Wapi zile nywele za pilipili?
> We Monika! (uk.36)

Katika shairi, 'Kuwako', mshairi ametumia kiunganishi 'na' kuongezea msisitizo katika wazo linalotangulia. Aghalabu kauli mbili zinapounganishwa huwa zina uhusiano wa karibu sana wa ujumbe unaowasilishwa. Kuziunganisha kauli mbili ni kuzisisitiza kauli hizo na kuzipa uzito sawa kwa mtindo wa kipekee. Katika utungo huu, mshairi anazungumzia hali ya kuwapo kwa binadamu akieleza namna ambavyo mtoto hujipata kwenye chupa ya mama, ambayo mshairi anataja kuwa 'rutuba ya uhai'. Mshairi ameteua maneno kwa njia ya kipekee akilenga kuuficha ujumbe kuhusu mchakato mzima wa ukuaji wa mtoto katika fuko la uzazi. Mshairi ametumia kiunganishi 'na' kuweka pamoja kauli zenye wazo moja linalowasilishwa. Kwa mfano:

> … Aliponisahau nilijipenyeza kwenye nyufa
> Nyembamba katika ngoma ya pumbao
> <u>Na</u> kama kiluilui kidogo sana nikaogelea…
> Hadi nilipogonga ukuta mwororo
> <u>Na</u> kuingia ndani kuwa kiumbe…
> Halafu nikaanza kufaidi utamu
> <u>Na</u> uhalisia wa kuweko
>
> Maelfu hutolewa nje ya uwanja.
> <u>Na</u> hawarudi tena.(uk.10)

Shairi hili ni la kisimulizi ambapo mshairi anasimulia mchakato mzima wa ukuaji wa mtoto hatua kwa hatua hadi anapozaliwa na kupewa jina. Baada ya kuzaliwa na kupatikana katika mazingira mapya, mshairi anaelezea namna binadamu anavyoathirika na mazingira hayo na kujihusisha na mambo yasiyompendeza Mungu aliyemuumba. Mshairi amelitunga shairi hili kwa kuliweka katika muktadha wa masimulizi ambao ni muhimu sana katika mawasiliano ya binadamu. Mtindo huu wa uwasilishaji hunasa hisia za mpokeaji na kuleta burudani ya kipekee ambayo humfanya mpokeaji huyo kumakinikia ujumbe unaowasilishwa. Kwa kutumia urudiaji wa 'na' mshairi, kimakusudi amefululiza matukio hivyo kujitwika jukumu la kuwasilisha maana.

## 3.6 Urudiaji wa kimuundo

Huu ni urudiaji ambapo muundo fulani umerudiwa. Urudiaji wa kimuundo unathibitishwa kutokana na matumizi ya usambamba katika ushairi ambapo muundo fulani wa virai, vishazi na sentensi hurudiwa. Aina zote za usambamba huwa zina muundo fulani unaorudiwa. Kezilahabi ameutumia mtindo huu wa urudiaji kuwasilisha maana. Katika diwani ya *Dhifa,* maana mbalimbali zimetiliwa mkazo kupitia aina tofauti za usambamba.

### 3.6.1 Usambamba wa kimuundo

Usambamba huu unahusu urudiaji wa ruwaza fulani ya kimuundo. Usambamba huu hutilia mkazo urudiaji wa muundo ambao ni sawa. Unahusisha urudiaji wa kategoria sawa ya maneno katika mistari ya kifungu kwa kusudi la kuleta msisitizo wa suala linalozungumziwa. Katika shairi, 'Dhifa,' Mshairi anazungumzia viongozi wanaonyakua na kupora mali ya serikali bila kujali wananchi. Tunapoangazia kifungu cha tatu, mshairi anawataja watu mbalimbali wanaohusika katika uporaji huu. Mwanzoni mwa kila mstari wa kifungu hicho, nomino, ambayo ni mojawapo ya kategoria za maneno, imerudiwa kwa ruwaza fulani ambapo majina ya watu mbalimbali yametajwa kama vile mawaziri, wabunge, waandishi na watangazaji. Wakereketwa na watangazaji wa habari ambao wanapaswa kuyaangazia masuala haya yanayowakera wananchi, wamenyamaza na hawashughuliki kamwe. Mshairi anasisitiza kuwepo kwa haja ya washikadau mbalimbali kukemea viongozi wanaofilisi nchi.

Mawaziri wenye kula
Wabunge wapewa magari
Waandishi walosajiliwa
Watangazaji wenye yale yale
Wakereketwa wasokereka
Kimya wamekaa. (uk.27)

### 3.6.2 Usambamba wa kisintaksia

Kwa mujibu wa Preminger na Brogan (1993: 877) , usambamba huu hutokea pale ambapo vipashio vya kisintaksia vinavyorudiwa hujitokeza pale pale pembeni mwa neno. Vipashio hivyo huwa kama nafasi zenye jukumu la kisintaksia, ambazo zinaachwa baada ya kuondolewa kimakusudi kwa kirai au kishazi ambacho katika usomaji, mpokeaji hukitia. Mshairi ameutumia urudiaji wa muundo wa kisintaksia katika kusisitiza maana na kupunguza uziada ambao ungeweza kutokea katika utungo wake. Kwa mfano, katika shairi, 'Kwa Walimu Wote', mshairi anaangazia na kuitabiri hali ya mwalimu, itakavyokuwa atakapostaafu na kurudi nyumbani. Kwa kutumia usambamba wa kisintaksia, mshairi, katika kifungu cha tatu, anaelezea taswira itakayokuwapo katika nyumba yake. Anasema, 'mijusi watataga mayai ndani ya viatu vyako vilivyokwisha visigino na ndani ya sidiria chakavu zilizoshikiwa kamba kwa pini.' Usambamba huu unadhihirika kutokana na matumizi ya sentensi, 'mijusi watataga mayai'...Sentensi hii inategemewa na sehemu mbili. Kwanza, 'viatu vyako vilivyokwisha visigino' na pili, 'sidiria chakavu zilizoshikiwa kamba kwa pini.' Ibainike kwamba, hata pale ambapo sentensi, 'mijusi watataga mayai' imeondolewa, msomaji bado anaitia katika usomaji wake. Hii ina maana kwamba sentensi hiyo imerudiwa kwa kutumia mtindo wa kisintaksia ili kutilia mkazo maana. Aidha, mistari ya sita na saba ya kifungu kicho hicho pia inadhihirisha usambamba huu. Sentensi, 'mende watazaliana ndani ya chupa tupu' ikiondolewa, mpokeaji anaitia katika usomaji wake.

Kumbuka mwalimu utakapostaafu.
Mijusi watataga mayai ndani ya viatu
Vyako vilivyokwisha visigino
Na ndani ya sidiria chakavu
Zilizoshikiwa kamba kwa pini.
Mende watazaliana ndani ya chupa tupu
Za marashi na za bia. (uk.1)

Katika shairi, 'Mafuriko', mshairi anatoa hisia zake kuhusu mafuriko, ambayo yametishia maisha kiasi kwamba watu wengi wamehama. Anaeleza namna upepo mkali unavyovuma na kutishia kuzibomoa nyumba zao zilizokwisha kulala pande. Analalama kwamba upepo huo uvumapo, wao hawalali. Katika kusisitiza madhara haya makubwa ya mafuriko, mshairi ametumia usambamba wa kisintaksia kwa njia ya kipekee. Katika kifungu cha pili mstari wa

kumi, kumi na moja na kumi na mbili, mshairi ametumia kishazi, 'kila kukicha twatazama'...Kishazi hiki kimeradidiwa kwa muundo wa kisintaksia. Mshairi anasema kwamba kila kukicha wanatazama mambo matatu, ambayo ni mizizi, mkao na kuta hafifu za nyumba. Ukamilifu wa sentensi hii unategemea kishazi hicho ambacho kinarudiwa kwa mtindo wa kipekee. Kinachobainika hapa ni kwamba, mpokeaji wa shairi hili anapokisoma kifungu hiki, anakitia kishazi hicho, hata ikiwa kimeondolewa. Ijapokuwa kishazi hicho hakionekani kurudiwa katika maandishi, msomaji anakitia katika usomaji wake hivyo kudhihirisha kwamba kishazi chenyewe kipo.

> ...Upepo mkali uvumapo hatulali.
> Kila kukicha twatazama mizizi yake
> Na mkao wake, na kuta hafifu za nyumba.
> Lazima ukatwe kuanzia matawi hadi shina
> Mafuriko ya mwaka huu yaashiria...(uk.4)

Hali kadhalika, tukiangazia shairi, 'Mpiga Zeze' mshairi, kwa njia ya masimulizi, anatoa nasaha na kutambua namna watu wanavyokabiliana na maisha na mazingira wanamoishi. Uteuzi wake wa maneno unadhihirisha usambamba wa kisintaksia hasa katika mstari wa ishirini na moja na ishirini na mbili. Kwa kuzingatia sentensi, 'ukamchukua mama mjamzito aliyebeba zigo kichwani, mtoto mgongoni,' inabainika kwamba mshairi amerudia kishazi, 'aliyebeba'. Kishazi hiki hakionekani mwanzoni mwa kirai, 'mtoto mgongoni'. Hii ina maana kwamba hata kikiondolewa msomaji bado anaweza kukitambua anaposoma.

> ...Mto Nabili ulifurika kwa mvua ya juzi
> Ukamchukua mama mjamzito
> Aliyebeba zigo kichwani, mtoto mgongoni...(uk.8)

### 3.6.3 Usambamba wa kivisawe

Hii ni aina ya usambamba ambapo, wazo moja linalojitokeza katika mstari fulani hurudiwa kwenye mstari mwingine kwa kubadilisha mtindo. Kimsingi, katika ushairi, jambo moja linaweza kuelezwa kwa maneno mengine ikawa kwamba wazo lile lile ndilo linalosisitizwa kwa mtindo tofauti. Usawe tunaozungumzia katika utafiti huu si wa kiwango cha neno kwa neno ila kirai au kishazi ambacho kina maana sawa na neno lililotajwa. Mshairi ametumia mtindo huu wa uwasilishaji maana katika diwani ya *Dhifa* kupitia kwa baadhi ya mashairi. Kwa mfano, tunaporejelea shairi, 'Madomo Mapana', mshairi, katika mstari wa ishirini na nane wa kifungu

cha kwanza, anawakemea viongozi mafisi na kuwahimiza wawaachie walimu waijenge nchi. Mshairi ametumia maneno, 'kukuna kichwa' na kufikiri ambayo yana maana sawa. Viongozi wanahimizwa kwamba ni kazi bure kufikiria kwamba wanajali mustakabali wa nchi ilhali mambo wanayojikunia vichwa ni namna ya kuifilisi nchi, jambo linalodhihirisha unafiki mkubwa.

...Bure kuweka mkono usoni,
Bure kukuna kichwa.
Kama hamwezi kufikiri. (uk. 7)

### 3.6.4 Usambamba wa kitanakuzi

Usambamba huu unahusu matumizi ya mawazo mawili ambayo yanakinzana au yaliyo na maana kinyume. Preminger na Brogan (1993:878) wanautaja kama urudiaji wenye jozi za maneno yanayokinzana. Msingi wa usambamba huu ni kauli kinzani ambapo wazo linaloelezwa katika mstari wa kwanza linapingana na lile linalojitokeza katika mstari wa pili. Mshairi huweza kuwasilisha maana anayokusudia kwa kutumia mtindo wa kutoa kauli zinazopingana, yaani kwa matumizi ya mbinu ya tanakuzi. Kauli hizi zinapotumiwa katika shairi hujenga ukinzani wa maana. Katika diwani ya *Dhifa*, mshairi ametumia mtindo huu wa urudiaji akilinganisha wazo kwa kutoa kauli kinyume. Katika shairi, 'Alalaye', mshairi anawahimiza watu wawe macho ili waweze kuelewa na kumakinikia mambo yanayofanyika katika mazingira yao. Watambue, wataje na wakemee ubinafsi ambao umekita mizizi miongoni mwa watu wanaotaka wafaidi bila kuhusisha wengine. Kifungu cha pili cha shairi hili kina muundo unaokinzana na mwingine ambapo suala linalosisitizwa kwa mtindo huu wa urudiaji ni uwepo na ushirikishwaji kikamilifu masuala yanayowahusu wananchi ili wote waweze kufaidi. Upande mmoja unapotaka wananchi washirikishwe, upande mwingine unapinga na kutoa kauli kinyume.

Wahisi hatujui nani kala
Wanasema asiyekuwapo lake halipo
Alalaye usimwamshe.
Tunasema:
Kila mwananchi alikuwepo na yupo
Lake lazima liwepo
Alalaye huamka mapema. (uk.26)

Katika shairi, 'Dhifa', Kezilahabi anazungumzia rasilimali za nchi ambazo zinasherehekewa, kunyakuliwa na kunyonywa na viongozi na watu wenye ushawishi mkubwa serikalini bila hata

kujali wananchi. Katika kifungu cha pili, mshairi anasema kwamba, hata katika kusherehekea kwao hawawezi kutambua kamasi puani hadi pale ambapo nzi anaamua kutua. Huu ni mtindo wa kijazanda ambapo suala la kutotambua kamasi puani likimaanisha kwamba viongozi wanahusisha fikira zao zaidi katika unyakuzi wa mali ya nchi kiasi cha kutozubaishwa na chochote. Aidha katika kifungu cha tatu, mawaziri na wabunge wanajigawa mali ilhali waandishi na watangazaji wa habari hawaangazii mambo hayo. Vilevile, wakereketwa ambao wanapaswa kuzungumzia na kuyakemea mambo haya wamebaki kimya na kuonekana kama watu wasiosumbuliwa na mambo yanayofanyika.

Kamasi jeupe lachungulia
Waonao hawaoni...
Watangazaji wenye yale yale
Wakareketwa wasokereka...(uk.27)

Katika shairi, 'Tena na Tena' mtunzi ametumia mtindo wa kipekee kusisitiza kuhusu hali ya mapenzi kati ya watu wawili akimithilisha hali hii na wanyama ambao hukwenda wawili wawili. Mshairi anahimiza watu wafikirie zaidi kuhusu umuhimu wa mapenzi na ndoa. Anatoa mfano wa panzi ambaye huruka na mpenziwe na chatu ambaye mpenziwe akifa yeye hujinyima kula na hatimaye hufa. Kauli zinazopingana zinajitokeza wakati mshairi anapofananisha maisha ya watu wawili katika kifungu cha kwanza na cha pili akitumia kiambishi kikanushi 'si'.

...Au mwezini kutua
Maisha ya wawili ni kama

...Harufu asijali
Maisha ya wawili si kama. (uk.45)

### 3.6.5 Usambamba wa kisemantiki

Usambamba huu pia huitwa usambamba wa kimaana kwani semantiki ni kiwango kimojawapo cha lugha kinachojishughulisha na maana. Hapa, muundo unaorudiwa huwa na maana ile ile kiasi kwamba maana inayojitokeza katika mstari mmoja ndiyo inayorudiwa na kukuzwa katika mstari mwingine kwa kubadilishana maneno. Katika ushairi, mwandishi huteua maneno na kutumia miundo mbalimbali ambayo humsaidia kuwasilisha maana inavyostahili. Miundo miwili au zaidi huweza kuwa na maana zinazofanana hivyo kutilia mkazo wazo hilo kwa mpokeaji.

Kezilahabi, katika ushairi wake, anasisitiza baadhi ya masuala kwa usambamba wa kimaana. Kwa mfano, katika shairi, 'Ukweli-Koko,' mshairi anatanguliza kwa kueleza kwamba lengo lake katika shairi hili ni kusema ukweli wala si uongo akipuuza chuki zozote dhidi yake kwa kusema ukweli.

Nimekuja kusema uongo
Sikuja kusema ukweli...(uk.50)

Kutokana na mfano huu, sentensi hizi mbili zina maana sawa. Sentensi ya pili inazungumzia jambo lile lile ambalo linazungumziwa katika sentensi ya kwanza. Maana inayojitokeza katika mstari wa kwanza unakuzwa katika mstari wa pili. Mtu ambaye ameamua kuzungumzia uongo bila shaka anadhihirisha kwamba lengo lake si kusema ukweli. Mshairi amerudia maana ile kwa madhumuni ya kuleta msisitizo kuhusu jambo analopania kusema.

Katika shairi, 'Zimwi', mshairi analalamikia madhara yanayosababishwa na zimwi kijijini. Zimwi limemeza watoto wote kijijini huku likiwaacha wazazi wakilala kwa uchungu waliopata. Katika shairi hili mtunzi ametumia sentensi mbili ambazo zina maana sawa. Ijapokuwa baadhi ya maneno aliyotumia hayana muundo sawa, mshairi ameyateua kwa namna inayoleta usawa wa kimaana.

Zimwi limemeza watoto wote kijijini...
Zimwi litujualo limetula likakwisha...(uk.40)

Sentensi hizi mbili zinajitokeza mwanzoni mwa kifungu cha kwanza na cha pili mtawalia. Kauli hizi mbili zinawakilisha sauti yenye kilio cha wazazi kuhusu hasara walizopata kutokana na kuuliwa kwa watoto wao na kumalizwa wote kijijini.

Katika shairi, 'Marahaba', mshairi anazungumzia hali inayowapata maskini wakiwa katika mikono ya matajiri. Katika kifungu cha sita mstari wa tano na sita, mshairi ametumia virai viwili ambavyo vina maana sawa. Mshairi anapozungumza kitamathali ameteua virai, 'vikombe vya majonzi' na 'ukoko wa mateso' ambayo yanadhihirisha hali ya huzuni.

...Ambako twakaribishwa
Kunywa vikombe vya majonzi
Na kula ukoko wa mateso

Kati ya vilio vya maskini
Na ngumi za matajiri. (uk.11)

### 3.6.6 Usambamba wa kidhamira

Kazi yoyote ya fasihi huwa na dhamira inayozungumziwa. Usambamba wa kidhamira unahusisha urudiaji wa wazo kuu kwa kutumia muundo fulani. Mshairi huteua maneno na kufinyanga lugha kwa njia ambayo inamwezesha kuwasilisha wazo lenyewe ili mpokeaji aweze kuuelewa ujumbe vyema. Aidha, mshairi anaporadidi dhamira, hutilia mkazo wazo na kulifanya lijitokeze kwa uzito unaostahili. Katika diwani ya *Dhifa,* mshairi ameutumia usambamba huu kuikuza dhamira. Katika shairi, 'Kwa Walimu Wote', mshairi anaeleza kuhusu mabadiliko katika maisha ya mwalimu tangu anapoanza kazi ya ualimu hadi anapostaafu. Wazo hili linarudiwa kimuundo kiasi kwamba vifungu vinne vya kwanza vinazungumzia hali ambayo mwalimu hujipata anapostaafu ilhali vifungu vinavyofuata vinaeleza kuhusu hali ya mazingira yake ya kazi na namna anavyoweza kuyaboresha kwa kupigania haki yake kwa kuwachagua viongozi wanaoweza kujali masilahi yao ipasavyo. Anasisitiza kwamba mabadiliko yatawezekana tu endapo walimu watajitokeza kwa umoja kutumia kura zao.

Huu utakuwa wimbo wako
Utakapostaafu urudipo nyumbani…
Utakuwa kichekecho cha watoto
Watakaokuita, Ticha! popote uendapo

Kumbuka mwalimu utakapostaafu
Mijusi watataga mayai ndani ya viatu…

Na manyigu watajenga ndani ya kofia
Zilizosahaulika kutani…(uk.1)

Katika shairi, 'Jibwa' mshairi anazungumzia jibwa kijazanda. Wazo kuu analoeleza ni kuhusu viongozi walafi, wakora na wadanganyifu wanaotumia hila zao kujifaidi wenyewe bila kuyajali masilahi ya wananchi wengine. Vifungu vyote vya shairi hili vinarudia na kusisitiza namna viongozi wanavyokosa maadili na kuifanya nchi kudorora kiuchumi kutokana na matumizi mabaya ya rasilimali.

Jibwa likitoka jikoni
Ulimi lajilamba…
Jibwa likianza kula mayai

Jua wizi limefuzu…

Jibwa liloshika hatamu
Adabu yake kiburi…

Jibwa liloshika hatamu
Litatumia kila hili

Dawa ya jibwa shika
Subiri litapolala…(uk.5)

Katika shairi, 'Mke wa Waziri' wazo linalorudiwa na mshairi linahusu mabadiliko ya tabia ya mke wa waziri anayeitwa Monika. Mshairi anavuta kumbukumbu kwa kurejelea maisha yake ya awali na kueleza namna alivyokuwa katika kiwango cha chini. Baada ya kuolewa na waziri maisha yake yanabadilika. Mshairi, kupitia kwa wahusika wanaolalamika kuhusu tabia ya Monika, anashangaa na kuduwazwa sana na mabadilko haya. Wazo hili linarudiwarudiwa katika shairi zima hivyo kuleta dhana na msisitizo wa dhamira hiyo.

Wewe Monika
Ulitoka kwetu bila ushanga kiunoni
Kama kumbukumbu asi mbawa…

Sikiliza Monika
Sisi tumezoea vituko vya wakubwa…

Monika sikiliza
Sisi wanawake wa shamba…(uk.13)

### 3.6.7 Usambamba wa kiwizani

Msingi wa usambamba huu ni mpangilio maalum wa mizani unaounda urefu sawa katika kila mstari ili kusababisha mapigo ya sauti. Usambamba huu hutokea pale ambapo mpangilio maalum wa mizani, unaoleta mapigo ndio unaorudiwa katika shairi. Uzuri wa kazi ya ushairi huweza kujengwa kutokana na matumizi ya sauti ambazo zinasababisha mapigo. Sauti moja inaporadidiwa mwishoni mwa kifungu kwa kufuata ruwaza fulani mahususi, hujenga wizani maalum. Katika diwani ya *Dhifa*, Kezilahabi ametumia usambamba wa kiwizani akilenga kunasa hisia na kuathiri mawazo ya mpokeaji kwa namna inavyomfanya amakinikie ujumbe unaowasilishwa. Katika shairi, 'Wimbo wa Unyago' kifungu cha pili, mshairi ametumia muundo maaalum unaoleta wizani huku akitoa wasia kwa vijana.

...Asifuye macho yako
Ataka kuyafumba;
Asifuye miguu yako
Ataka usitembee ;
Asifuye meno yako
Ataka ucheke kijinga.( uk.17)

Katika shairi, 'Alalaye' mshairi anahimiza kuhusu haja ya watu kuwa makinifu katika mambo yanayofanyika katika mazingira yao ili waweze kufaidi. Faida humjia mtu anayeamua kushughulikia mambo yanayofaa na ambayo yanasaidia kutimiza mahitaji ya watu wanaoisha katika mazingira ambamo mambo hayo yanatokea. Kutokana na maneno ambayo mshairi ameteua kwa mtindo wake mwenyewe, mpokeaji anausiwa dhidi ya kuwa zumbukuku asiyefahamu mambo yanayofanyika hata machoni pake. Hali hii inasisitizwa katika mistari sita ya kifungu cha pili ambacho kinajenga mapigo fulani maalum. Katika kifungu hiki, mapigo yanajitokeza tunaposoma au kukariri mstari baada ya mstari.

Tumeona ngozi ya ng'ombe imewambwa
Wafikiri hatujui nyama ilikokwenda
Tumeona mifupa ya kuku jalalani
Wadhani hatujui nani kafaidi
Tumeona vyombo vikisafishwa jikoni
Wahisi hatujui nani kala. (uk.26)

Kupitia kwa shairi 'Bonde', Kezilahabi anatoa ushairi wa kisimulizi anaporejelea zamani palipokuwa na giza, nalo jua likafuata ili kung'arisha nchi. Mshairi anazungumza kijazanda akielezea kuhusu namna watu walivyoishi zamani bila matumaini yoyote na baadaye nchi ikawa na mabadiliko kutokana na juhudi na fikira za wananchi. Hatimaye matumaini yakaanza kuwajia wananchi. Mistari mitatu ya kifungu cha tatu inadhihirisha hali hii kwa kujenga wizani maalum.

...Pakawa na giza
Pakawa na mwanga
Pakawa na fikra. (uk.29)

### 3.7 Urudiaji wa kibalagha

Sanaa ya balagha, ambayo ni jinsi ya kusema na kueleza jambo, inaweza kufanikishwa kupitia kwa urudiaji, kama njia mojawapo inayotumiwa kuwasilisha ujumbe fulani. Kwa mujibu wa

Wamitila (2008: 494), urudiaji wa kibalagha ni urudiaji ambao unahusishwa na balagha. Hii ina maana kwamba kuna mbinu zinazohusishwa na urudiaji wa kibalagha. Ijapokuwa mbinu hizo ni nyingi, tumejikita katika chache tu zilizotumiwa na mshairi katika diwani ya *Dhifa*.

### 3.7.1 Anafora

Hii ni mbinu ya urudiaji wa kibalagha ambayo inahusu urudiaji wa neno au kifungu cha maneno mwanzoni mwa mistari katika kifungu cha shairi. Kipengele hiki cha urudiaji hutumiwa na washairi kama mtindo wa kipekee wa kubainisha kazi zao kwa lengo la kutilia mkazo kauli fulani. Kezilahabi ni mmoja katika washairi ambao hutumia anafora kuwasilisha maana kikamilifu. Kwa mfano, katika shairi 'Wakati Fulani' kirai, wakati fulani kimerudiwa mwanzonni mwa mistari ya kifungu cha tatu. Mshairi anasisitiza kwamba mambo hufanyika kwa kutegemea wakati. Mshairi anazama katika akili ya msomaji na kuonyesha namna binadamu anavyobadilika kiwakati kwa kutegemea mambo anayotaka kutekeleza. Hali hii inadhihirisha kwamba matamanio ya binadamu hutofautiana na kubadilika wakati baada ya wakati.

Wakati fulani twasubiri kuche...
Wakati fulani twamsaka paa gizani
Wakati fulani twataka kumshika mbogo
Wakati fulani kwa machozi twatamani...(uk.15)

Katika shairi, 'Kwa Walimu Wote' mshairi amerudia kitenzi, 'nilipokuwa' mwanzoni mwa mistari ya kifungu cha kwanza. Anarejelea nyuma awamu ambazo mwalimu amepitia kabla ya kuweza kuitwa mwalimu, kutoka utotoni hadi ujanani, akawa mtu mzima na hatimye kuitwa mwalimu Bure.

...Nilipokuwa mtoto niliitwa Chacha...
Nilipokuwa kijana niliitwa Chaupole
Nilipokuwa mtu mzima niliitwa Manywele
Nilipokuwa mwalimu nikaitwa Bure. (uk.1)

### 3.7.2 Epifora

Huu ni urudiaji ambapo neno au kishazi hurudiwa mwishoni mwa mistari ya kifungu cha shairi fulani. Mtindo huu unadhihirika katika shairi, 'Wimbo wa Unyago.' Mshairi ametumia neno 'haifai' na kulirudia mwishoni mwa mistari ya sita na saba ya kifungu cha tatu. Mtunzi

anaikashifu hulka ya umbea na tabia ya kuzungumza kuhusu watu bila ya kuyachuja maneno wanayosema. Anaiona kama hulka ambayo haifai katika jamii. Mshairi anasisitiza kwamba mwanamke yeyote anayeamua kumchafulia jina mumewe hadharani na kumsawiri kama mtu asiyefaa, bila shaka anapaswa kufahamu kuwa hata naye pia hafai katika nyumba hiyo.

...Asemaye mumeo hafai
Nyumbani kwake pia hafai...(uk.17)

### 3.7.3 Anadiplosia

Huu ni urudiaji ambapo neno au kifungu cha maneno mwishoni mwa mstari fulani hutumiwa mwanzoni mwa mstari unaofuata ili kuleta msisitizo wa jambo linalozungumziwa. Kwa mfano, katika shairi 'Harusi,' mshairi ameradidi neno, 'tufapo' mwishoni mwa mstari wa kumi na sita na kulirudia mwanzoni mwa mstari unaofuata. Anasisitiza kuhusu kifo ambacho anakimithilisha na harusi ya mwisho ambayo kila mmoja atapitia hivyo basi binadamu anapaswa kuwa tayari kwani wakati wake utafika. Kulingana na shairi, hofu aliyo nayo binadamu humfanya atamani sana maisha yasonge kwa mwendo wa kinyonga na konokono ili siku ya kifo isiweze kufika haraka.

...Tufe tufapo
Tufapo tumekufa...(uk.39)

Shairi,'Niliona', lina urudiaji wa aina hii ambapo neno, 'niliona' limetumiwa mwishoni mwa mstari wa saba wa kifungu cha kwanza na kurudiwa katika mwanzo wa mstari unaofuata wa kifungu cha pili. Mshairi anasisitiza kuhusu madhara yanayowapata watu hasa wanapokosa kutumia akili zao vyema kufikiria. Anathibitisha kuona ishara za madhara ya majuto zinazotokana na kukosa kufikiria.

...Aliyejidhihirisha kwa ishara, niliona
Niliona yakitagaatagaa...(uk.33)

Katika shairi, 'Wimbo wa Unyago' neno 'olewa' ambalo limejitokeza mwishoni mwa mstari wa tano limerudiwa mwanzoni mwa mstari unaofuata wa kifungu cha kwanza. Mshairi anatoa wosia kwa vijana akiwahimiza kuishi maisha yanayotukuka, nao wasichana kufanya maamuzi ya busara wanapoamua kuolewa kwani ni chaguo la kila msichana.

...Olewa msichana olewa
Olewa chaguo lako...(uk.17)

### 3.7.4 Epanalepsia

Cuddon ( 2013 : 239 ) anaeleza kwamba urudiaji huu wa kibalagha ni mtindo unahusu urudiaji wa neno au kishazi baada ya maneno mengine kujitokeza katikati yao. Hii ina maana kwamba maneno mengine hujitokeza katikati ya neno linalorudiwa. Kishazi au neno la kwanza katika mstari hurudiwa mwishoni mwa mstari huo huo. Kwa mfano, katika shairi,' Jibwa' mshairi ametumia mtindo huu wa urudiaji akisisitiza neno 'piga'. Anawahimiza wananchi kutumia njia wanazoweza kuwazuia viongozi walaghai na walafi wanaoiba na kupora mali ya serikali bila kuwajali wananchi waliowachagua. Urudiaji huu unajitokeza katika vifungu tofautitofauti vya shairi hili.

Piga limekwiba piga (kif. 1)
Piga kichwa piga (kif. 5)
Piga kwa bunduki, piga (kif.7), (uk.5)

Katika kifungu cha tatu cha shairi, 'Mtakaso', jina, Chapu linatajwa na kuradidiwa katika mistari ya kwanza na tatu mtawalia. Mshairi anasisitiza kuhusu mhusika Chapu, ambaye anatajwa na mtu anayenyatia nyuma yake. Kila baada ya hatua mbili anapotembea anasikia jina lake likitajwa lakini anapogeuka na kutazama nyuma, kimya kinatawala. Msisitizo upo kwa mhusika huyu Chapu kutokana na namna anavyoandamwa, hali inayomfanya azongwe na mawazo.

'Chapu!' Nyumangu ' Chapu!'
Nani aninyatia! Hatua mbili natembea.
'Chapu chapu!' Nyumangu 'Chapu Chapu!'
Nani! Natazama nyuma:
Kiza. Kimya. (uk.19)

Shairi, 'Wimbo wa Unyago' nalo lina urudiaji huu. Katika kifungu cha kwanza, vitenzi, 'ishi' na 'olewa' vimerudiwa pembezoni mwa nomino kijana na msichana mtawalia. Jambo muhimu ambalo mshairi anasisitiza kwa kijana msichana ni kwamba anapaswa kuishi maisha kwa kujichagulia na kujiamulia mwenyewe mtu wa kumwoa pasipo kujifunga katika minyororo ya kikabila. Uhuru wa kujichagulia uwe kama mwanga unaomsaidia kijana kubaini mwenza bila kuongozwa na ukabila kwani ukabila ni utumwa.

Ishi kijana ishi, ishi maisha yako…
Olewa msichana olewa
Olewa chaguo lako…(uk.17)

## 3.8 Hitimisho

Katika sura hii tumeangazia viwango mbalimbali vya urudiaji na namna vinavyodhihirika katika diwani ya *Dhifa* kwa kutoa mifano ya mashairi husika. Tumejadili kwa kutoa mifano mwafaka namna ambavyo Kezilahabi ameutumia urudiaji wa aina mbalimbali kuwasilisha maana kikamilifu na kuendeleza dhamira yake. Hata hivyo urudiaji tuliozungumzia hapa unajitokeza katika mashairi kwa viwango vinavyotofautiana kutoka shairi moja hadi jingine. Kuna baadhi ya urudiaji ambao unajitokeza katika mashairi mengi ilhali urudiaji mwingine unajitokeza kwa uchache. Kwa mfano, hakuna mifano toshelezi ambayo inaweza kujitokeza katika diwani kudhihirisha usambamba wa kifahiwa. Kimsingi, mshairi amefaulu pakubwa kutumia urudiaji kama mtindo wa kipekee katika kuwasilisha maana.

# SURA YA NNE

# URUDIAJI KATIKA DIWANI YA *VI FARU WEUSI*

## 4.1 Utangulizi

Katika sura hii tumebainisha namna mshairi, Muhammed Khatib alivyotumia urudiaji kuwasilisha maana na kuendeleza dhamira yake. Tutatoa mifano mwafaka inayodhihirisha aina mbalimbali za urudiaji zinazojitokeza katika diwani. Viwango ambavyo tumeangazia katika sura ya tatu ndivyo tutakavyobainisha na kueleza namna vilivyotumika katika uwasilishaji wa maana.

## 4.2 Urudiaji wa irabu na konsonanti

Irabu na konsonanti ni sauti ambazo zinamlazimu mwandishi yeyote kuzitumia katika kazi yake kwani ndiyo msingi wa maneno yatumiwayo katika sentensi zozote. Urudiaji wa sauti hizi umetawala pakubwa mashairi ya diwani hii. Kwa mfano, katika shairi, 'Twiga', ambapo mshairi anamfananisha kiongozi na twiga, ametumia mtindo wa kurudia irabu na konsonanti kwa njia inayoleta ujumi, hasa katika maneno ya mwisho ya mistari mitatu ya kifungu cha kwanza. Uteuzi wake wa maneno unabainika kwa namna alivyozipanga irabu. Baadhi ya irabu na konsonanti zilizoradidiwa ni kama vile: *a, i, e, k,* na *l.* Huu ni mtindo wa kimakusudi wenye lengo la kuleta wizani unaoambatana na maana.

> Masikio yako, yamepaa,
> Tukwambiayo, huyasikii,
> Sauti,
> Tunaipaza, haikufikii,
> Kelele,
> Tunazipiga, hazikushituwi,
> Shida zetu, huzijuwi, tabu zetu, huzielewi,
> Dhiki yetu, hutambuwi.
> Lini utatusikiliza?...(uk.9)

Katika shairi, 'Vitambi,' mshairi ameangazia hulka ya unyakuzi wa rasilimali za nchi unaofanywa na viongozi walio madarakani. Ametilia mkazo wazo hili kwa ujumi wa kipekee ambapo irabu na konsonanti zimeradidiwa katika baadhi ya maneno aliyotumia. Sauti

zilizorudiwa ni kama vile: *a, o, u, i, ch, j* na *k.* Kifungu cha kwanza cha shairi hili linabainisha urudiaji huu hasa katika mistari mitatu ya mwisho.

Vitambi,
Vimekuwa makaburi,
Makaburi ya mizoga,
Mizoga ya wanyama,
Wanyama pia na kuku,
Kuku, jogoo, makoo,
Vitambi,
Vitambi ni sera ya wachinjachinja! (uk.18)

## 4.3 Urudiaji wa silabi

Silabi zinaporadidiwa na mshairi, huipa kazi ujumi hasa katika uwasilishaji. Hii ni kwa sababu ya mapigo ya sauti yanayoambatana na silabi hizo. Mfumo wa vina huweza hujengeka kutokana na kurudiwa kwa silabi katika sehemu za mstari. Silabi hizi zinaweza kuwa kati au mwisho wa mstari kwa kutegemea aina ya shairi. Aidha, silabi zinaweza kurudiwa popote pale katika mistari ya shairi. Silabi, kama ilivyo irabu na konsonanti ni sehemu muhimu ya kiisimu inayotumiwa kuunda maneno yanayotumiwa katika utungo wowote. Hivyo basi mshairi anapoamua kutumia mtindo wa kiziradidi katika kazi yake, mpokeaji hupata fursa ya kutekwa hisia kwa njia ambayo inapendeza anapoisoma. Katika kudhihirisha urudiaji huu wa silabi, mshairi ametumia mfumo wa vina ambapo silabi nyinginezo zinarudiwa mwishoni mwa mistari kwa lengo la kuleta wizani. Kwa mfano, tunaporejelea shairi, 'Waafrika', mshairi amejitwika jukumu la kunasa hisia ya mpokeaji kwa kuradidi silabi mbalimbali katika vifungu kadhaa. Silabi kama vile: *wa, ma, li, ru* na *kwa* katika kifungu cha kwanza na cha pili ni baadhi tu ya silabi ambao zimerudiwa katika shairi hili. Mshairi anapozungumzia matatizo mbalimbali waliyopitia Waafrika chini ya wakoloni, anazua hisia na kuajabia unyonge na unyama uliotokea.

Waafrika,
Waliwindwa, kama wanyama,
Walisagwa, kwa wima wima,
Walisombwa, bila huruma,
UNYONGE.
Unyonge ulioje!
Walisakwa, mabarubaru,
Walishikwa bila uhuru,
Na kuteswa pasi udhuru,
UNYAMA…(uk.73)

Katika shairi, 'Mkunazini,' mshairi anapiga mwangwi suala lile lile analozungumzia katika shairi, Waafrika', tulilokwisha kutaja. Katika kifungu cha kwanza anaeleza kuhusu soko la binadamu akiajabia na kusisitiza kwa kutumia maneno yenye uhusiano wa kifahiwa, namna wananchi walivyonadiwa, walivyozabuniwa na walivyonunuliwa. Anaangazia namna wanawake kwa wanaume walivyopigwa na kuachwa na makovu kisha kusafirishwa bila hiari kupitia nyikani na bahari. Katika vifungu viwili vya mwanzo, mshairi amebainisha urudiaji wa silabi mbalimbali zinazoleta mapigo ya sauti hivyo kuathiri hisia ya mpokeaji.

Soko la binadamu,
La kunadiwa,
Kuzabuniwa,
Kununuliwa,.
Kovu limeacha,
Yenye uovu,
Na uonevu.
Unyonge ulioje?

Ni wake kwa waume,
Waliosagwa,
Waliozugwa,
*Pia kupigwa,*
Nao kwa maelfu,
Bila hiyari,
Wakasafiri,
Nyika na bahari,
Unyama ulioje?...(uk.63)

## 4.4 Urudiaji neno

Shairi, 'Twiga' linadhihirisha urudiaji wa maneno kwa njia ya kipekee. Mshairi ametumia visawe vya maneno ili kusisitiza wazo moja. Kwa mfano, katika kifungu cha kwanza mstari wa saba na wa nane, maneno kama vile: shida, tabu na dhiki yametumiwa pamoja. Neno moja ni kisawe cha jingine hivyo kuleta maana sawa ambayo inatiliwa mkazo katika shairi. Mshairi anamlimbikizia 'twiga' kidole cha lawama kwa kuwatenga watu na kuwaacha wakihangaika, kuteseka na kukosa raha. Mwandishi ametumia neno twiga kijazanda kumaanisha kiongozi ambaye amekaa mbali sana na wananchi kiasi kwamba hawawezi kumfikia na kumweleza shida zinazowakabili. Kukaa mbali huku ndiko kunakomithilishwa na urefu wa twiga ambaye hata kelele za watu hazimfikii kwa sababu masikio yake yako mbali. Vilevile katika kifungu cha pili

wananchi wanamwona kiongozi huyo kama mtu anayewaringia. Neno maringo linasisitizwa kwa kurudiwa na kisawe chake, madaha.

> ...Kelele,
> tunazipiga, hazikushituwi.
> Shida zetu, huzijuwi, tabu zetu, huelewi
> Dhiki yetu, hutambuwi
> Lini utatusikiliza?
>
> Huo mwendo wako, wa maringo,
> Utembeavyo, wingi maringo.
> Madaha,
> Wingi wa pozi, hunesa shingo. (uk.9)

Katika shairi, 'Niamini' mshairi ametumia kitenzi, 'Niamini' akizungumza moja kwa moja na mpokeaji wa ujumbe akimhimiza amwamini kwamba anampenda na hamtaki mwengine kamwe. Neno hili, niamini limerudiwa na kutawala kila kifungu cha shairi kwa lengo la kusisitiza upeo wa mapenzi yao ya dhati yasiyoyumbayumba wala kutetereka.

> Niamini,
> Niamini, niamini, niamini, Muhibaki,
> Niamini,
>
> Niamini,
> Niamini, muhibaki, simtaki,
> Mwengine.
>
> Niamini,
> Simtaki, simtaki, na sitoki
> 'Meridhika
>
> Niamini,
> Na sitoki, na sitoki, sibanduki,
> Nimefika.
>
> Niamini,
> Sibanduki, sibanduki, sigeuki,
> Daima. (uk.25)

Katika shairi, 'Vitambi', mtunzi anawalalamikia viongozi wanaoyajali matumbo yao. Mali na rasilimali za serikali zinawafaidi wachache sana huku wananchi wa kawaida wakiteseka. Katika

kifungu cha nne, maneno kama vile: chichiri, hongo na rushwa yametumiwa kama visawe. Katika mstari wa tatu, maana ya neno chichiri imetiliwa mkazo kwa kutumia maneno mengine yenye maana sawa nalo. Mshairi anawasuta viongozi mafisadi wanaotegemea hongo ili kutoa huduma. Msisitizo upo katika utoaji chichiri ambao kihisia mshairi analalamika kuwa ufisadi huu unawafaidi wachache tu.

...Vitambi,
Vimeshehenizwa riba,
Riba na nyingi chichiri,
Chichiri, hongo na rushwa,
Rushwa pia unyonyaji,
Unyonyaji kitabaka.
Vitambi,
Wachache kufaidika! (uk.18)

## 4.5 Urudiaji wa kimaumbo

Katika shairi la kihisia, 'Damu! Damu! Damu!', mshairi analilia wadudu mabalimbali wanaowasumbua usiku na mchana kwa kunyonya damu zao. Katika kuwasilisha ujumbe huu, mshairi ametumia umbo la kipekee lenye kibwagizo cha kibunifu ambapo anamalizia neno, 'damu' kwa hisia katika mwisho wa kila kifungu. Kila kifungu cha shairi kina mistari miwili ya mwisho inayofanana. Muundo huu ndio unaorudiwa katika kila kifungu ili kutilia mkazo damu inayonyonywa na wadudu hawa. Urudiaji huu wa kimaumbo unajitokeza kwa wingi sana katika mashairi mengi ya diwani hii hivyo kudhihirisha mtindo wa kipekee wa mshairi katika uwasilishaji wa maana.

Usiku ulalapo,
Hatusalimiki.
Hufika vitandani,
Ndani mifumbatini,
Na pia michagoni,
Vifaru vya kunguni,
Kutunyonya damu zetu,
Damu!

Mchana majini,
Hatunusuriki.
Pekupeku mwendoni,
Wakulima shambani,
Wafugaji mbugani,

Kepu kuja miguuni,
Kutunyonya damu zetu,
Damu!...(uk.20)

Urudiaji wa kimaumbo pia huweza kubainika kutokana na matumizi ya virai au vishazi vilivyo na urefu sawa. Urefu huu hutokana na idadi ya silabi zinazotumika na mshairi kimakusudi ili kuweza kudhihirisha umbo fulani maalum. Urudiaji huu unajitokeza katika shairi, 'Waso Kauli'. Katika shairi hili, mistari yote ambayo inaunda shairi zima ina urefu sawa. Hii ni kwa sababu silabi zinazounda virai na vishazi hivyo vyote, kutoka kifungu cha kwanza hadi cha mwisho, ni tano. Hili ni umbo la kipekee ambalo mshairi amelitumia kusisitiza wazo kwamba watu ambao wanachukuliwa kwamba hawana usemi katika maendeleo ya nchi kwa sababu moja au nyingine pia wana jukumu la maana hivyo wanapaswa kupewa nafasi. Mshairi anazindua hadhira kuhusu uwepo wa watu wa aina mbalimbali anaowataja kama, 'waso kauli' ambao ni mabubu, vipofu, vigugumizi, wenye vithembe na wenye vitata wanaopaswa kuhusishwa katika masuala ya taifa.

Waso kauli,
Hawasemeki,
Kwa wingi wao.
Kwa wingi wao,
Hawasemeki,
Wasokauli.

Waso sauti,
Hawasikiki,
Sauti zao.
Sauti zao,
Hawasikiki,
Wasosauti...(uk.12)

Matumizi ya kiunganishi 'na' ni mtindo mwingine unaotumiwa na mshairi kuwasilisha maana. Mtindo huu pia unadhihirisha urudiaji wa kimaumbo. Kiunganishi hiki 'na' kinapotumika kuunganisha kauli mbili, hali inayojitokeza ni mkazo unaopewa kauli zenyewe. Katika shairi, 'Visivyosema' mshairi anaangazia nguvu na uwezo mkubwa vilivyo navyo, viti au viumbe visivyo na uwezo wa kusema au kunena. Kutokana na maneno anayoteua, ni bayana kwamba ijapokuwa viumbe hivyo havineni, vina uwezo na kulalamika hata bila binadamu kutambua. Kwa mfano katika kifungu cha nne, 'na' imetumika kuunganisha na kusisitiza viumbe

visivyosema lakini vina uwezo wa kutoa ishara ya hujuma dhidi yao. Umbo jingine lenye kiunganishi 'na' pia linarudiwa katika kifungu cha sita ambapo mshairi anasisitiza kuhusu ngurumo na radi kuwa na athari zake vile vile hata bila kusema.

...Visivyosema,
Ndege na wanyama,
Bara na mrima,
Wa mboga na nyama.
Nao hulalama,
Bila ya kusema,
Kupata hujuma,
Hutoa sauti...

...Visivyosema,
Ngurumo na radi,
Wingu hushitadi,
Na baridi kutaradadi,
Na kuwa shadidi
Hapo hujasudi,
Huwa zajinadi,
Pasipo hodi,
Hutoa sauti. (uk.32)

## 4.6 Urudiaji wa kimuundo

Dhana ya usambamba ndiyo inayotumika kuelezea urudiaji huu. Urudiaji wa kimuundo hutokea pale ambapo muundo fulani wa kishazi, kirai au sentensi umerudiwa katika shairi. Tumejikita katika baadhi ya aina za usambamba zinazojitokeza katika diwani ya *Vifaru Weusi*.

### 4.6.1Usambamba wa kimuundo

Usambamba huu hutokea pale ambapo muundo wenye ruwaza sawa ya maneno hurudiwa katika mistari ya kifungu cha shairi. Kwa mfano, katika shairi, 'Waafrika' mshairi anaangazia hali ya maisha ya Waafrika chini ya mikono ya mkoloni. Anaangazia namna Waafrika waliteswa na kudhulumiwa huku wengi wao, hasa wenye nguvu wakichukuliwa na kusafirishwa ili kuwatumia katika mashamba yao ughaibuni. Kwa mfano, katika kifungu cha kumi na tatu, mshairi anaeleza namna watu shupavu na wenye nguvu walivyotengwa na Waafrika wengine wasio na nguvu, hali ambayo mshairi anaitaja kama usaliti mkubwa. Katika mstari wa pili, tatu na nne mshairi ameendeleza ruwaza sawa ya kimuundo kwa kutumia kivumishi cha kipekee,' wenye' na kivumishi cha sifa, 'shupavu'. Hali kadhalika, mshairi ametumia usambamba wa kimuundo

katika kifungu cha kumi na sita anapozungumzia safari ndefu ambayo Waafrika walipitia wakienda ughaibuni kufanya kazi katika mashamba ya wakoloni. Mshairi ametumia nomino halisi na za mahali katika ruwaza sawa.

Usaliti ulioje!
Wenye nguvu ligombaniwa,
Washupavu, kang'ang'aniwa,
Wenye mbavu, kuzabuniwa,
USALITI...

Uthakili ulioje!
Baharini, safari ndefu,
Marekani, wakasarifu,
Arabuni, ikenda safu,
Na Bukini, ikawa sufufu...(uk.73)

Aidha, mshairi katika, 'Kitubio' anaangazia jinsi jamii ilivyojawa na taasubi za kiume. Anasisitiza mtazamo wa jamii kwamba kazi kubwa ya mwanamke inapaswa kuonekana nyumbani. Kwa mujibu wa mshairi, mwanamke anasawiriwa kama mfanya kazi wa nyumbani na ambaye jukumu lake haswa ni kushiriki kikamilifu katika shughuli za nyumba. Anatarajiwa kuwa kama dobi, topasi, yaya, mpishi, mtekamaji, mchanjakuni, mkulima na kuwa mchungaji wa mbugani. Katika mstari wa mwisho wa kila kifungu, mshairi anatoa hisia inayomfanya aonekane kumwonea huruma. Anaposema, 'tuombe kitubio', anahisi kwamba mwanamke amedhalilishwa na kukosewa hivyo basi jamii inastahili kuomba msamaha. Katika kuendeleza usambamba wa kimuundo, mshairi ametumia nomino zinazowataja wafanyakazi mbalimbali kwa njia inayoonesha mpangilio wa ruwaza sawa ya kimuundo hasa katika kifungu cha kwanza na cha pili.

Mwanamke, si
Dobi wa nguo kufuwa?
Topasi wa majaaliwa?
Yaya kwa 'naozaliwa?
Mpishi wa kupakuwa?
Kiota cha kutotowa?
Tuombe kitubio.

Mwanamke, si
Mtekamaji kisimani?
Mchanja kuni shambani?

Mkulima wa kondeni?
Mchungaji wa mbugani?
Kibarua wa mjini?
Tuombe kitubio...(uk.38)

### 4.6.2 Usambamba wa kisintaksia

Usambamba huu unahusu urudiaji wa muundo wa kisintaksia ambapo vipashio vya kisintaksia ndivyo vinavyorudiwa. Katika shairi, 'Wanamitumba' mshairi anakashifu tabia ya kuiga mambo na vitu vya kigeni na kuziacha mila na desturi. Anaeleza namna tulivyoacha mitindo ya maisha na hali za maisha yetu na kuzama kabisa katika mienendo ya kigeni. Mshairi anatuona kama 'wanamitumba' yaani watu wanaopokea tu pasipo kutathmini wala kufikiria ubora wa mambo au vitu tunavyopewa kutoka 'nje' bali tunakumbatia na kuvitumia bila kujali athari zao. Katika kifungu cha kwanza mstari wa kwanza wa shairi hili, usambamba wa kisintaksia unadhihirika. Mshairi anasema kwamba tumekuwa wanamitumba, kwa mitindo na kwa kuimba. Sentensi hii ina kishazi, 'tumekuwa wanamitumba' ambacho kinasisitizwa. Tunaweza kuiandika sentensi hii upwa bila kiunganishi 'na' zikawa, 'tumekuwa wanamitumba kwa mitindo' na 'tumekuwa wanamitindo kwa kuimba'. Hii ina maana kwamba badala ya mshairi kutumia kishazi hiki mara mbili, ameamua kukiondoa katika maandishi kwani hata ikiwa kimeondolewa, mpokeaji bado atakitambua na kukitia katika usomaji wake. Msisitizo utabakia ule ule wa uanamitumba, wa kuiga, si tu mitindo ya maisha bali pia namna wanavyotunga na kuimba nyimbo zao, hali ambayo mshairi anaiona kama ujinga usiomithilishwa.

Tumekuwa wanamitumba, kwa mitindo na kwa kuimba,
Desturi zetu zilo njema,
Pia mila zenye neema,
Zote tumeziacha nyuma,
Na kujenga uhasama.
Utobwe ulioje! (uk.69)

Katika shairi, Nira na Shemere' mshairi anaangazia makundi mawili ya watu ambao wanaishi maisha yanayotofautiana kabisa. Anabainisha kwamba kuna kundi la watu wachache 'wanaoshiba' hasa viongozi wanaotumia rasilimali za nchi kujinufaisha. Kwa upande mwingine kuna kundi lenye asilimia kubwa sana ya watu maskini wanaoteseka, wanaodhoofika na wasioweza kuwa na 'vitambi'. Aidha, wana njaa na hawawezi hata kwenda mbweu kama wanavyofanya wenye kushiba. Kifungu cha nne mstari wa tano, sita, saba na nane mshairi

ametumia muundo wa kisintaksia. Kutokana na matumizi ya kiunganishi, wala, tunatambua kwamba kishazi, 'tumedhoofika na kukorongoka bila ya…' kimerudiwa kwa mtindo wa kipekee. Ibainike kwamba kishazi hiki ndicho kinachotegemewa na nomino, 'vitambi' na msemo, 'kwenda mbweu'. Ijapokuwa kishazi chenyewe hakionekani kurudiwa katika maandishi, mpokeaji hukitia anapolisoma shairi hili. Hii ina maana kuwa, hata pale ambapo kishazi hicho kimeondolewa, bado kinabainika na msomaji katika usomaji wake.

Nira na shemere,
Wachache hushiba,
Pasi habahaba,
Wengine ni tiba,
Tumedhoofika,
Na kukorongoka,
Bila ya vitambi,
Wala kwenda mbweu. (uk.78)

Shairi, 'Nimi' limetungwa kwa kuzingatia mbinu ya uhuishi. Mshairi anaangazia simu ( simu ya kiganja) kwa kuipa uwezo wa kuzungumza na kujipa sifa. Simu inajigamba kwa kueleza namna binadamu anavyoienzi muda wowote na popote aendapo. Katika kifungu cha tatu, simu inaeleza namna inavyohusika katika kupanga njama. Inasikia njama ambazo ni dhahiri na zile fiche. Mstari wa kwanza hadi wa nne, inadhihirisha usambamba wa kisintaksia. Sentensi, 'nimi husikia njama za dhahiri na za siri' inaweza kuandikwa kwa njia mbili. Kwanza, tunaweza kuwa na, 'nimi husikia njama za dhahiri' na 'nimi husikia njama za siri.'meradidiwa. Hata hivyo, sentensi, 'nimi husikia njama' haijarudiwa katika maandishi. Hii ina maana kwamba, hata ikiwa imeondolewa katika shairi, sentensi hiyo hutiwa na mpokeaji katika usomaji wake. Huu ni mtindo wa kipekee ambao mshairi amechagua kimakusudi kutumia kutilia mkazo ujumbe anaowasilisha.

Nimi,
Husikia njama.
Za dhahiri,
Na za siri,
Nimeshabaini,
Wao wanadhani,
Hawajulikani,
'Mechelewa. (uk.15)

### 4.6.3 Usambamba wa kivisawe

Usambamba huu hudhihirika wakati ambapo mshairi amerudia na kukuza wazo moja katika mstari mwingine kwa kubadilisha maneno. Msingi wa usambamba huu ni kwamba maneno anayotumia katika mstari wa kwanza siyo yale anayotumia katika mstari wa pili muradi wazo liwe lie lile. Shairi, 'Ndwele' ni mojawapo ya mashairi katika diwani ya *Vifaru Weusi* yanayozungumzia mapenzi. Mshairi amezama na kugubikwa zaidi katika mapenzi kiasi cha mapenzi hayo kumsababishia ndwele. Ameathirika na huba na hawezi kuishi bila mapenzi kwani yeye hukosa hata chakula na usingizi. Mshairi anadhihirisha kwamba ukosefu wa mapenzi unamwuguza na dawa ambayo ina uwezo wa kuutibu ugonjwa wake ni mapenzi pekee. Katika kifungu cha kwanza mstari wa kwanza na wa pili mshairi anasema 'ndwele ya mahaba imenisibu' nao mstari wa mwisho anasema, 'yanipa tabu'. Kinachobainika hapa ni kwamba kitenzi, 'imenisibu' ni kisawe cha kishazi, 'yanipa tabu'. Kwa kuyateua maneno haya kwa mtindo wake, mshairi anatilia mkazo matatizo na tabu anayopata kutokana na ukosefu wa mapenzi. Anaugua kimapenzi, hali inayojitokeza kama msiba mkubwa kwake.

Ndwele ya mahaba,
Imenisibu,
Sili nikashiba,
Wewe sababu,
Ni nyonda ya huba,
Yanipa tabu...(uk.6)

Katika shairi, Twiga' mshairi anamlalamikia twiga ambaye amekaa mbali sana nao na hawezi hata kuwasikiliza kutokana na sikio lake lililo mbali. Akizungumza kijazanda, mshairi anamkashifu na kumsuta kiongozi anayekaa mbali na wanachi baada ya kuchaguliwa. Hasikilizi wala kuelewa matatizo ya wananchi waliomchagua. Mshairi anaitazama hali hii kama maringo kwa wanachi. Katika kifungu cha pili, anazungumzia maneno, 'madaha' na 'wingi wa pozi'. Neno, madaha ambalo lina maana ya 'kuwa na maringo' ni kisawe cha kishazi, wingi wa pozi, kama kilivyotumika katika kifungu chenyewe. Kimsingi, mshairi analenga kutilia mkazo maringo ya kiongozi huyu huku akiyahusisha na tabia ya dharau kwa wananchi waliomchagua wakitarajia kuhudumiwa kwa heshima na dhati ya moyo.

Huo mwendo wako, wa maringo,
Utembeavyo, wingi wa maringo,

Madaha,
Wingi wa pozi, hunesa shingo.
Wapenda,
Mwendo wa pole, na kutetemeka,
Sisi huku, kila siku, pekupeku, kama kuku,
Si mwenzetu, njoo huku.
Lini utateremka?...(uk.9)

Katika shairi, 'Hadi lini?' mshairi anastaajabishwa na hali ya vita inayokithiri miongoni mwa wananchi. Akitumia urudiaji maalum wa kiumbo, anajiuliza swali hili hili mwishoni mwa kila kifungu. Hali kadhalika, ameteua maneno yake kwa mtindo ambao unaonesha usambamba wa kivisawe. Katika kifungu cha tatu, mshairi anazungumzia, 'tunapambana' na 'twakuwa vitani'. Kwa mujibu wa mshairi, kule kupambana ni kushiriki katika vita, hali ambayo inadhihirisha usawe wa kauli hizo mbili. Mshairi anatilia mkazo uwepo wa vita na kujiuliza mwisho wake.

Mpaka lini?
Twakuwa vitani,
Tunapambana,
Vita virefu,
Vita vinachosha.
Hadi lini? (uk.30)

### 4.6.4 Usambamba wa kifahiwa

Maneno yanapokuwa na uhusiano wa kifahiwa, huwa kuna neno fulani kuu ambalo maana yake inategemewa na maneno mengine. Katika uhusiano huu, maana ya maneno mengine hujengeka kutokana na neno kuu ambalo ndilo msingi. Katika shairi, 'Uhasama' mshairi amezua hali kinzani anapozungumzia, baridi na joto, mvua na jua, usiku na mchana na mbingu na ardhi. Katika kila mstari wa pili wa vifungu vitano, mshairi ametumia maneno kama vile: hazipatani, hazikutani, havionani, havigusani na havijuani ili kuelezea uhasama uliopo. Mshairi anapotumia neno kuu, 'hazipatani' anamaanisha, hali ya kutoingiliana kwa vyovyote vile. Maneno yanayofuata katika vifungu vingine yana uhusiano wa kifahiwa na neno hilo hivyo kutilia mkazo maana.

Baridi na joto,
Hazipatani.

Mvua na jua,

Hazikutani.

Usiku na mchana,
Havionani.

Mbingu na ardhi,
Hazigusani.
Uhai na kifo,
Hazijuani.

Ni uhasama,
Mpaka lini? (uk.26)

Katika shairi, 'Masurupwete' mshairi anaongea na hadhira yake akiwauliza wanachoficha wanapoyavaa masurupwete, nguo ndefu zinazojaa katika maungo yao kiasi cha mwili kutoonekana. Mshairi anashangazwa na watu wanaovaa masurupwenye (bwelasuti) na mashumburere (kofia pana) akihofia kwamba kuna kitu au jambo wanaloficha. Usambamba wa kifahiwa unajitokeza kutokana na muundo maalum uliotumiwa na mshairi katika kila mstari wa tano wa kila kifungu cha shairi. Katika maswali ambayo mshairi anajiuliza, ametumia maneno yaliyo na uhusiano wa kifahiwa kama vile: 'Kinachozibwa nini?', 'Mnachoficha nini?' na 'Kifunikwacho nini?' Kitenzi, ziba kina uhusiano na vitenzi ficha na funika ambapo wazo linalisisitiwa ni hali ya kutoweka mambo waziwazi.

Masurupwete!
Mnaovaa mwilini,
Yakajaa maungoni,
Mwili hauonekani,
Kinachozibwa nini?
Nundu na vitambi vyenu?

Masurupwenye!
Mnaovaa viunoni,
Toka juu hadi chini,
Miguu haionekani,
Mnachoficha nini?
Ngiri na matende yenu?

Mashumburere!
Mvaayo vichwani,
Hushindiliwa pomoni,

Peponi,
Hakutakiwi,
Motoni
Kwakimbiliwa.
Vitamu,
Havitakiwi,
Vichungu,
Vyagombaniwa.

Asali,
Haionjwi,
Shubiri,
Yashabikiwa.

Minofu,
Haitakiwi
Mifupa,
Yang'ong'olewa.

Amani,
Haipendezwi
Ghasia,
Zakumbatiwa.

Vizima,
Havitumiwi
Vya nyufa,
Vinaenziwa...(uk.32)

Shairi, 'Uhasama' ambalo tumekwishataja katika kazi hii pia linadhihirisha usambamba wa kitanakuzi. Katika shairi hili, mshairi anaangazia mambo yanayokinzana kutoka kifungu cha kwanza hadi cha tano. Anazungumzia baridi na joto, mvua na jua, usiku na mchana, mbingu na ardhi, uhai na kifo akisisitiza namna mambo yanavyotofautiana maishaini.

### 4.6.5 Usambamba wa kisemantiki

Huu ni usambamba wenye muundo wa kukuza maana kwa kuirudia maana hiyo katika mistari ya kifungu cha shairi. Kwa mfano, katika kifungu cha pili cha shairi, 'Ndwele' mshairi anaangazia hali yake ya kimapenzi akisisitiza jinsi maisha yanavyomwia magumu kutokana na kukosa mpenzi wake. Anaeleza namna ambavyo anakosa usingizi, anavyokonda na kuwa mgonjwa. Katika mistari mitatu ya kifungu cha pili, mshairi ameteua, kwa mtindo wa kipekee, vishazi vitatu ambavyo vinazungumzia jambo moja. Kwa mfano, anaposema, 'sipati naumu', kucha

n'nakesha', 'lepe kwangu sumu' maana inayojitokeza hapa ni moja tu, ambayo ni ukosefu wa usingizi kutokana na penzi linalomtesa na kumwuguza.

Sipati naumu,
Kucha n'nakesha.
Lepe kwangu sumu,
Yanikondesha.
Mimi mahamumu,
Magumu maisha. (uk.34)

Katika shairi, 'Wasokauli' mshairi anaangazia nafasi za watu ambao wana ulemavu mbalimbali akisisitiza kwamba wao pia wanapaswa kuhusishwa katika masuala ya nchi. Katika vifungu vyote vya shairi, mtindo sawa wa kisemantiki ndio unaotawala. Kila kifungu kina sentensi yenye maneno yanayobadilishana nafasi kwa kutoa maana ile ile. Kwa mfano, mshairi katika kifungu cha kwanza anasema, 'waso kauli hawasemeki kwa wingi wao' na 'kwa vingi wao waso kauli hawasemeki'. Jambo linalozungumziwa ni lile lile tu ila ametumia mtindo wa kubadilisha nafasi za maneno yenyewe. Mshairi ametumia mtindo huu katika vifungu vyote hivyo kudhihirisha usambamba wa kisemantiki.

Waso kauli,
Hawasemeki,
Kwa wingi wao,
Kwa wingi wao,
Hawasemeki,
Waso kauli.

Waso sauti,
Hawasikiki,
Sauti zao,
Sauti zao,
Hawasikiki,
Wasosauti...(uk.12)

Katika, 'Tende na Zaituni', mshairi ametumia mtindo ule ule alioutumia katika, 'Wasokauli' ili kuwasilisha maana. Mstari wa tano na wa kwanza wa kifungu cha kwanza na cha pili mtawalia, mshairi ametumia kishazi, 'walao hujisahau' na 'hujisahau walao'. Kwa kubadilisha nafasi ya maneno mshairi anatilia mkazo jambo lile lile, kwamba yeyote anayepata nafasi ya kula matunda matamu yaotayo jangwani bila shaka hujisahau hasa wale wanaoyala kwa mara ya kwanza.

Mtazamo huu ni ule wa kisiasa ambapo viongozi wanaochaguliwa kwa mara ya kwanza kuwakilisha wananchi hujitajirisha na kufurahia mali ya serikali pasi na kuwakumbuka waliowapigia kura.

> Matunda ya Arabuni,
> Yanayoota jangwani, matamu yasokifani,
> Yenye hadhi na thamani,
> Walao hujisahau,
> Hasa wale limbukeni.
>
> Hujisahau walao,
> Wakahajiri makwao, kuacha asili yao…(uk.36)

### 4.6.7 Usambamba wa kidhamira

Usabamba wa aina hii hutokea pale ambapo lengo kuu la mshairi linaradidiwa katika shairi. Ni urudiaji ambao dhamira ile ile ndiyo inayorudiwa ili kuisisitiza kwa mpokeaji. Kwa mfano, Shairi, 'Uzezeta' ni moja katika mashairi katika diwani hii ambayo yanasisitiza ujumbe kwa kuiangazia dhamira ile ile katika vifungu vyote vya shairi. Mshairi anadhamiria kuangazia madhara ya dawa za kulevya kwa kuelezea namna mbalimbali ambazo dawa hizi zinatumika na watu kiasi cha kuwafanya waraibu. Katika kifungu cha kwanza, mshairi anasema kwamba dawa zinazoingizwa mwilini kwa sindano na vidonge humsababisha mtu kuwa zuzu, huwa mwendawazimu, hukosa usingizi na kukosa hamu ya chakula. Kifungu cha pili kinabainisha namna waraibu wa dawa hizi hutumia vipumbazi ambavyo huwapumbaza na kuwaharibu akili. Aghalabu huwa wenye kushangaa, kuduwaa na kuzubaa kila wakati.

Isitoshe, katika kifungu cha tatu, mshairi anawatambua wale wanaotumia vichangamshi wanaodhani kwamba dawa hizo huwapa furaha na kujiona 'wamefika' na kamwe hakuna mashaka. Waraibu hawa hawafahamu kwamba dawa hizi huwazuzua tu. Aidha, majani ya miraa ambayo huwakeshesha, yamezungumziwa katika kifungu cha nne. Kwa mujibu wa mshari, wanaoyatumia majani haya hupandwa na furaha ya kidhahania tu kama ile ya watumiaji pombe. Wao hujiona mafarisi wenye vyeo na nafasi wasijue kwamba wanajiletea mawazo ya kihayawani. Kimsingi, mshairi ameutumia usambamba wa kidhamira kwa kuiradidi dhamira ile ile kupitia vifungu hivi vinne kwa njia ya kipekee kuleta msisitizo kuhusu namna dawa za kulevya zinavyoathiri watu katika jamii.

Sindano pia vidonge,
Ni vileta usingizi,
Mlaji huwa kama renge,
Humuotesha na njozi,
Hata akipewa tonge,
Kuila huwa hawezi,
Chakula hakitamani, yumo tu usingizini,
Muda wote yu ndotoni,
Kumbe vile ni zezeta!..(uk.48)

Katika shairi, 'Mbwamwitu' mshairi anaangazia matatizo, mateso na maafa yanayosababishwa na mbwamwitu dhidi ya wanyama wengine wanyonge. Katika kila kifungu cha shairi hili, mshairi anaelezea namna mbwa mwitu anavyowararua wanyama wenzake, wanavyovinyofoa viungo vya wanyama, wanavyong'atua maini na matumbo ya wenzao, wanavyomegua matumbo na wanavyojifuta damu nyingi midomoni baada ya kuwararua wanyama. Shairi hili ni la kijazanda ambapo mshairi anamithilisha mbwa mwitu na matajiri viongozi wanaodhalilisha na kuwanyanyasa wanyonge ili waendelee kunufaika huku wanyonge wakizidi kulia na kuumia. Baada ya kunyakua mali, wao hutumia hila na ujanja kuwapumbaza wananchi ili wasiweze kujua jambo linalotendeka. Anapiga mfano wa taifa la mnyonge mnyongeni lenye watu wa tabaka la juu wanaowatumia vibaya wa tabaka la chini kwa kuwanyima haki zao na kuwatumia kujitajirisha. Dhamira ya mshairi ni kuelezea, kwa kuficha makali ya ujumbe, namna viongozi serikalini wanavyowanyanyasa wananchi ili kujinufaisha wenyewe. Hili ndilo wazo linaloradidiwa kutoka kifungu cha kwanza hadi cha mwisho hivyo kudhihirisha usambamba wa kidhamira.

Nawaona mbwamwitu,
Wanavyorarua,
Miili ya wanyama wenzao,
Bila ya huruma.

Nawaona mbwa mwitu,
Wanavyonyonyofoa,
Viungo vya wanyama wenzao,
Vizima vizima...(uk.77)

### 4.6.8 Usambamba wa kiwizani

Msingi wa usambamba wa aina hii ni mpangilio maalum wa mizani kwa njia inayosababisha mapigo na kuleta ujumi wa ushairi. Mpokeaji anapolisoma shairi, 'Mzimu' mapigo ya sauti yanayounda virai na vishazi yanabainika. Hii ni kutokana na matumizi ya idadi ya mizani sawa katika vipande vyake. Ujumi wa uwasilishaji unaopatikana katika shairi hili, unaambatana na ujumbe kifungu baada ya kifungu. Kwa mfano, katika kifungu cha kwanza, mshairi anaelezea namna wahandisi na wanasheria walivyo katika kukurukakara za kuziacha kazi zao walizosomea ili kuingia 'pangoni'. Mshairi ametumia neno pangoni kuashiria ulingo wa kisiasa wenye msukosuko ambapo wataalamu wanapigania nafasi za uongozi huku kila mmoja akijipendekeza kwa wananchi na kuacha taaluma aliyosomea. Wanapigana vikumbo ishara kwamba nafasi hizo za kazi ni chache na zinastahili kupiganiwa kiasi cha mwenye nguvu kupishwa. Mshairi ametumia mtindo huu kwa mpangilio unaopendeza sana na unaonasa hisia za mpokeaji kutoka kifungu cha kwanza hadi cha mwisho.

Nawaona wahandisi, pia na wanasheria,
Wapiga kwata kwa kasi, bila hata kutulia,
Wazikimbia nafasi, kazi walizosomea,
Vikumbo wapigana,
Na huku washindana,
Kuingia pangoni,
Mzimuni…(uk.40)

Hali kadhalika, shairi, 'Sili' linapiga mwangwi shairi, 'Ndwele' ambalo pia linazungumzia mapenzi yanayomfanya mshairi kukosa chakula na usingizi. Hata hivyo shairi hilo halina urudiaji tunaozungumzia hapa. Katika shairi, 'Sili', mshairi anaangazia hali yake ya kimapenzi akieleza namna anavyokosa chakula na hata akipata chakula hicho, hali akashiba kwa sababu ya fikira za huba. Shairi hili lenye kifungu kimoja tu linadhihirisha mpangilio maalum wa mizani inayotoshana katika mistari yote, hivyo kusababisha mapigo ya sauti yenye ujumi wa kipekee.

Sili nikashiba,
Nikikukumbuka,
Hula habahaba,
Kwa kushikashika,
Sababu ya huba,
Kwangu imeshika. (uk.23)

Katika shairi, 'Si Wahusika', mshairi anazungumzia tabia ya watu kujipa umaarufu wasiostahili. Anaangazia kundi la watu wanaobeba silaha na kuvalia magwanda kama ishara ya kushiriki vita vya kumwangamiza adui. Ajabu ni kwamba wanaporejea kutoka vitani, wanajipaka damu ya mnyama waliomsaka ili kuwapumbaza watu kuwa wamepambana na adui na kuwaua. Wanaomba na kucheza kwa furaha kuashiria kwamba wamemweza adui bali ni shere tu wanazochezea watu ili waonekane shujaa, wapate heshima na wajipe sifa wasizostahili. Kwa mfano, katika kifungu cha kwanza, mshairi anatoa taswira ya uono ili kuashiria namna walivyotoka vitani. Wanajiwekea pinde begani, mikuki kuifunga kiunoni, visu vyenye ncha kali na panga huku wakiwa na magwanda yao kuonyesha kwamba wametoka kushiriki mapambano ambayo hakika si wahusika hata kidogo. Mshairi ametumia mtindo wa kipekee wa ruwaza sawa ya kimuundo. Katika mistari ya vifungu vyote, mshairi ametumia idadi sawa ya mizani kwa namna inayoleta mapigo ya sauti.

Pinde zimo begani,
Mikuki mikononi,
Shembea kiunono,
Na vitara alani,
Magwanda maungoni,
Wanatoka vitani…(uk.86)

## 4.7 Urudiaji wa kibalagha

Urudiaji wa kibalagha unahusishwa na balagha ambayo ni sanaa ya usemaji. Kuna mbinu nyingi ambazo huzingatiwa katika urudiaji wa aina hii. Hata hivyo katika uchanganuzi wetu, tumeangazia na kuzichanganua mbinu chache tu ili kubainisha namna mshairi alivyozitumia katika uwasilishaji wa maana.

### 4.7.1 Anafora

Urudiaji wa neno au kifungu cha maneno mwanzoni mwa kila mstari wa kifungu cha shairi ni mtindo wa kipekee unaotoa msisitizo wa kauli inayozungumziwa. Mwadishi ametumia mtindo huu katika baadhi ya mashairi ili kuwasilisha maana. Kwa mfano, katika shairi, 'Niamini', mshairi anarejelea neno lile lile mwanzoni mwa kila mstari wa kifungu cha kwanza. Mshairi anaangazia hali ya kimapenzi ambapo anamhakikishia mpenzi wake kuhusu uhusiano wao. Anamtakata mpenzi wake aweze kumwamini kwa vyovyote vile kwamba anampenda na kamwe

hawezi kubanduka kutoka kwenye penzi hilo. Kwa kuliradidi neno, niamini, mshairi anakusudia kutilia mkazo mapenzi hayo.

> Niamini,
> Niamini, niamini, Muhibaki,
> Niamini. (uk.25)

Katika shairi, 'Tende na Zaituni', mshairi anadhihirisha matumizi ya neno, 'sio' lenye dhana ya ukanusho mwanzoni mwa mistari mitatu ya kifungu cha nne. Mshairi anazungumzia uongozi kijazanda akielezea namna nafasi hizo za uongozi zilivyojaa faida nyingi. Anasisitiza kuhusu wingi wa rasilimali zinazowekwa chini ya ulinzi wao, kiasi kwamba wale wanaochaguliwa, hasa kwa mara ya kwanza hula na kuwasahau wananchi waliowachagua.

> Tende pia zaituni,
> Zimeiva sio changa, zimeingia mchanga,
> Sio mpunga wa kutwanga,
> Sio mtama wa kuchunga,
> Sio njugu za kukaranga. (uk.36)

### 4.7.2 Anadiplosia

Urudiaji huu hudhihirika pale ambapo neno au kifungu cha maneno kinachotumika mwishoni mwa mstari hurudiwa katika mwanzo wa mstari huo. Mshairi ametumia mtindo huu wa urudiaji katika baadhi ya mashairi yake. Miongoni mwa mashairi hayo, 'Tufani' ndilo linalodhihirisha upeo wa mtindo huu. Mshairi ameteua na kuyapanga maneno kikamilifu kutoka kifungu cha kwanza hadi cha mwisho. Maneno ambayo yametumika mwishoni mwa kila mstari ndiyo yanayorudiwa mwanzoni mwa mistari inayofuata. Mshairi ameutumia mtindo huu katika vifungu vyote vitano. Katika shairi lake, tufani nzito inaangamiza abiria wa jinsia zote, wakubwa kwa wadogo. Kutokana na mvua nyingi yenye radi na upepo mkali unaotikisa chombo baharini, abiria wanalilia maisha yao. Hali hii inazua wasiwasi na mshtuko miongoni mwa nahodha na mabaharia ambao sasa wanagundua kwamba wao si hodari.

> Dhoruba pia tufani,
>   Tufani na kikukusi,
> Chombo kimo mkondoni,
>   Mkondoni kina kisi,
> Wimbi nje wimbi ndani,
>   Wimbi ndani lenye fosi.

Na mvua zinanyesha,
Zinanyesha utusitusi,
Radi nazo zatingisha,
Zatingisha kirisasi,
Giza nene linatisha,
Linatisha ni jeusi...(uk.71)

Katika shairi, 'Vitambi' mshairi anazungumzia hulka ya viongozi kwa njia fiche sana. Anaelezea namna uongozi ulivyobadilika kuwa njia ya kujilimbikizia mali na kujinufaisha bila kuwatumikia wananchi na nchi kwa jumla. Badala ya kufanya shughuli zinazoinua uchumi na kujenga taifa wanajihusisha na unyakuzi wa rasilimali za nchi na kuufanya kuwa kama 'sera' zao. Mshairi amedhihirisha mtindo wa anadiplosia katika kila kifungu cha shairi hili. Maneno yaliyotumiwa mwishoni mwa kila mstari ndiyo yanayoradidiwa katika mianzo ya mistari inayofuata.

Vitambi,
Vimekuwa makaburi,
Makaburi ya mizoga,
Mizoga yao wanyama,
Wanyama pia na kuku,
Kumu, jogoo, makoo,
Vitambi,
Vitambi ni sera ya chinjachinja!
Vitambi,
Vimekuwa ni maghala,
Maghala ya marobota,
Marobota ya nafaka,
Nafaka nao uwanga,
Vitambi,
Ni matumbo yao fadhila!..(uk.18)

### 4.7.3 Epifora

Katika urudiaji huu, neno au kifungu cha maneno huradidiwa kwenye sehemu ya mwisho ya mstari. Kwa mfano, kifungu cha pili cha shairi, 'Twiga' kinadhihirisha mtindo wa epifora. Mshairi ametumia neno, maringo mwishoni mwa mistari miwili ya kwanza ambapo anasisitiza

mwendo wa pozi na madaha ya twiga. Mshairi anamtazama mnyama twiga kama kiongozi anayewakwepa wananchi waliomchagua. Kulingana naye, kukaa mbali na wananchi ni njia ya kuwaringia wananchi wenyewe ambao wanamtarajia karibu.

> Huo mwendo wako wa maringo,
> Utembeavyo, wingi maringo,
> Madaha,
> Wingi wa pozi, hunesa shingo...(uk.9)

## 4.8 Hitimisho

Katika sura hii, tumebainisha namna urudiaji unavyojitokeza katika diwani ya *Vifaru Weusi.* Tumetoa mifano katika kila aina ya urudiaji ili kudhihirisha namna mshairi alivyotumia mtindo huu katika kuwasilisha maana. Idadi ya mifano tuliyotoa katika kila aina inatofautiana kutoka shairi moja hadi jingine kutokana na uzito wa kila aina ya kiwango cha uwasilishaji uliotumiwa na mshairi. Kwa mfano, vipengele vya urudiaji wa kibalagha kama vile mrejeleokuwili na epanalepsia havijajitokeza. Hata hivyo, hii haimaanishi kwamba Muhammed Khatib hajapiga ndipo haja yake ya kimtindo kuwasilisha maana. Kwa hakika, mshairi amedhihirisha uhuru wa mshairi na uwezo mkubwa wa kimtindo kuwasilisha maana.

# SURA YA TANO

# DHIMA NA ATHARI ZA URUDIAJI KATIKA DIWANI ZA *DHIFA* NA *VIFARU WEUSI*

## 5.1 Utangulizi

Mshairi anapotumia urudiaji kama mtindo wa uwasilishaji wa maana, huwa anapania kuleta athari fulani kwa mpokeaji wa ujumbe. Athari hii ni muhimu sana katika kuyaendeleza maudhui na kuikuza dhamira ya mshairi. Katika sura ya tatu na nne, tumeangazia aina mbalimbali za urudiaji zinazojitokeza katika diwani ya *Dhifa* na *Vifaru Weusi* mtawalia na kutoa mifano mwafaka ili kubainisha mtindo wa mshairi. Katika sura hii, tumejikita katika dhima na athari zinazosababishwa na urudiaji hasusan uendelezaji wa maana na ujumi unaodhihirishwa na washairi katika diwani hizi mbili.

## 5.2 Usisitizaji wa maana

Urudiaji ni mtindo muhimu sana katika usisitizaji wa maana katika shairi. Maclin ( 1996: 293) anapotoa maelezo kuhusu maana ya urudiaji, anayataja masuala mawili ambayo ni muhimu sana. Kwanza, anaeleza kwamba neno, kishazi au muundo wowote wa sentensi unapotumiwa zaidi ya mara moja katika shairi, husababisha msisitizo: pili huzua athari ya kipekee kwa mpokeaji wa kazi yenyewe. Ushawishi wa mpokeaji ni athari kubwa sana ambayo mshairi hulenga anaporudia maneno au vifungu vya maneno katika shairi. Bradford (1997: 2) anaposema kwamba msomaji hutumia lugha kwa mtindo unaomwezesha kumshawishi mlengwa wake. Croft na mwenzake (2000: 57) wanaikariri dhana ya ushawishi kwa kuuweka katika muktadha wa urudiaji, wakisema kwamba mtindo wa urudiaji wa maneno yenye maana sawa aghalabu hutumiwa huleta msisitizo na ushawishi katika shairi. Jambo linalodhihirika hapa ni kwamba, urudiaji wa maneno huleta nguvu na uzito katika wazo kuu linalozungumziwa. Mshairi anapoamua kuwasilisha wazo kwa hadhira, hutumia mtindo wa kipekee ambao unaomwezesha kuathiri mawazo na hisia. Maneno yanayoradidiwa katika shairi hutilia mkazo wazo kwa njia inayoweza kumshawishi mpokeaji kuhusu suala zima linaloangaziwa.

Kwa mujibu wa Wamitila (2008: 499) usisitizaji ni sifa ya urudiaji ambayo inajitokeza pale ambapo maneno fulani yanarudiwa hasa yale maneno ambayo yana uwezo wa kuibua hisia fulani

kwa mlengwa. Mshairi huweza kuradidi maneno kwa njia inayoibua hisia za mpokeaji hivyo kusisitiza ujumbe unaowasilishwa ipasavyo. Katika diwani za *Dhifa* na *Vifaru Weusi,* washairi wameangazia masuala mbalimbali ambayo wameyasisitiza kwa kuyaradidi maneno na vifungu vya maneno kihisia.

Kwa mfano, katika shairi, 'Mtakaso', Kezilahabi anaangazia jinsi mawazo yanavyomtawala mhusika. Katika kifungu cha kwanza, anaeleza namna mhusika anavyotembea akiyumbayumba kama mlevi huku akisikia sauti za watoto wakimsengenya: 'Ndiye! Siye! Ndiye! Siye!'. Aidha, hisia ya wasiwasi inajitokeza katika kifungu cha tatu ambapo mhusika anaitwa mara nyingi kwa jina lake lakini pindi anapogeuka nyuma kumtazama anayemwita, kimya kinatawala na haonekani kabisa. Msisitizo upo katika mhusika huyu ambaye anahitaji mtakaso. Hii ndiyo maana katika kifungu cha nne, mwenye sauti ile anajitambua akisema 'Usiogope! Ndimi mlinziwo.' Mshairi anasisitiza hali inayomgubika mhusika akidhihirisha hisia za woga.

> ...Nyumangu sauti za watoto zasengenya:
> Ndiye! Siye! Ndiye! Siye!
> Natazama nyuma: kiza, kimya.
> Mto mpana u mbele yangu.
>
> ''Chapu!'' Nyumangu "Chapu!"
> Nani aninyatia! Hatua mbili natembea.
> "Chapu Chapu!" Nyumangu " Chapu Chapu!"
> Nani! Natazama nyuma:
> Kiza. Kimya. (uk.19)

Urudiaji uliopo katika shairi hili unaelezwa kihisia ambapo msisitizo unaelekezwa katika uhitaji wa mtakaso kutokana na hali ya mhusika. Uelezaji huu wa kihisia una athari kubwa kwa mpokeaji wa ujumbe. Katika usomaji wa shairi hili, mpokeaji anaingiwa na hisia za woga kiasi cha kuhisi kama kwamba yeye ndiye mhusika anayezungumziwa. Usisitizaji huu ambao unatokana na urudiaji wa uelezaji kihisia, kama anavyouita Wamitila (2008: 500) unadhihirisha dhima mojawapo ya urudiaji kama mtindo wa mshairi.

Mifano mingine ya mashairi yanayodhihirisha dhima hii katika diwani ya *Dhifa* ni kama vile: Mafuriko, Puuu!, Hati, Mkolole, Mke wa Waziri na Pa! Hali kadhalika, katika diwani ya *Vifaru Weusi* tunapata mashairi kama vile: Mke wa waziri, Masurupwete, Vitambi, Waafrika, Damu! Damu! Damu!, Iwapi?, Watembeza Mabakuli na Wanamitumba.

## 5.3 Uelewekaji wa ujumbe

Dhamira ya mshairi hueleweka kutokana na uteuzi wake wa maneno na mtindo anaotumia kuwasilisha ujumbe. Aghalabu, ujumbe wowote unaowasilishwa katika ushairi au kazi yoyote ya fasihi sharti ueleweke wazi ndipo lengo kuu la mshairi liweze kutimika. Uelewekaji huu hutegemea muwala wa kazi husika. Kwa mujibu wa Jeffries na mwenzake (2010: 85) njia kuu inayotumika kukuza uwiano katika matini ya fasihi ni urudiaji, ambayo inahusisha matumizi ya maneno na miundo sawa ya virai, vishazi na sentensi. Kutokana na maelezo yake, maneno na vifungu vya maneno vinaporadidiwa kwa mtindo na mpangilio fulani huchangia pakubwa katika uelewekaji kwa kujenga muwala na uhusiano wa sehemu tofautitofauti za matini. Urudiaji unapotokea hatua kwa hatua kwa uwiano, kumsaidia mpokeaji kuelewa ujumbe ipasavyo. Uwiano wa matini katika shairi ndio unaohakikisha kwamba ujumbe umeeleweka vyema na mpokeaji.

Washairi, Kezilahabi na Mohammed Khatib wamechangia pakubwa katika kuleta uwiano katika mashairi yao ili kuhakikisha kwamba dhamira zao zimeeleweka. Hii inatokana na mtindo wa urudiaji wa maneno na vifungu vya maneno, wenye utaratibu mzuri na ambao unajitokeza kila baada ya hatua. Urudiaji ni mojawapo ya mitindo ya uandishi ambao umetumiwa na washairi hawa kuleta uwiano katika mashairi yao. Takribani mashairi yote katika diwani hizi yanabainisha dhima ya uelewekaji unaotokana na urudiaji. Kwa mfano, tunapotazama shairi, 'Kwa Walimu Wote' katika diwani ya *Dhifa*, tunashuhudia muwala mzuri sana unaosababishwa na urudiaji wa kianafora ambapo mwanzoni mwa mistari minne ya kifungu cha kwanza, neno, 'nilipokuwa', limerudiwa. Aidha, urudiaji wa neno, 'niliitwa' katikati ya mistari mitatu umechangia pakubwa katika kukuza uwiani huo. Hapa, mshairi anampeleka mpokeaji katika utaratibu wa matukio ya maisha ya mwalimu tangu awe mtoto hadi akawa mtu mzima, mwalimu hasa, kwa jina Bure.

> Sikilizeni wimbo huu:
> Nilipokuwa mtoto niliitwa Chacha
> Kwa matamshi yangu ya sasa
> Nilipokuwa kijana niliitwa Chaupele
> Nilipokuwa mtu mzima niliitwa Manywele
> Nilipokuwa mwalimu nikaitwa Bure. (uk.1)

Tunapotazama diwani ya *Vifaru Weusi,* shairi, 'Vifaru Weusi' linadhihirisha wazi muwala tunaozungumzia kupitia kwa usambamba wa kifahiwa unaojitokeza katika kifungu cha pili. Maneno, wanateswa, wananyanyaswa na dhalilishwa yana uhusiano wa kifahiwa na jinsi yalivyotumiwa katika shairi hilo yamejenga uwiano unaochangia katika kueleweka kuzuri kwa ujumbe.

Vinyama vidogo,
Viswala na digidigi,
Si ngiri wala si fisi,
Hawana nafasi,
Wote wanateswa,
Na wananyanyaswa,
Na kudhalilishwa,
Ndani ya nyika,
Kwetu Afrika,
Hakuishiki,
Ni adhabu. (uk.1)

## 5.4 Upigaji mwangwi

Kwa mujibu wa Wamitila (2008: 500) urudiaji unapotokea katika kazi ya kifasihi au matini yoyote, unaweza kuwa na dhima ya kupiga mwangwi kazi nyingine hivyo kuchangia katika uelewekaji wa ujumbe. Katika fasihi, kazi moja inapopiga mwangwi kazi nyingine, ina maana kwamba masuala yanayozungumziwa katika matini hayo mawili yanaingiliana pakubwa. Dhamira inayoangaziwa katika matini fulani ndiyo ile ile inayojitokeza katika matini mengine hivyo kutajwa kuwa mwingilianomatini ambao hutumiwa na waandishi wa kazi za fasihi. Katika ushairi, upigaji mwangwi huchangia pakubwa katika kueleweka kwa dhamira kwa kuwa shairi moja linapopiga mwangwi jingine, wazo kuu hurudiwa. Kwa mfano, katika Diwani ya *Vifaru Weusi,* mshairi anadhihirisha dhima ya upigaji mwangwi kupitia mashairi mawili: 'Mkunazini' na 'Waafrika.' Shairi, Waafrika ni mwangwi wa kidhamira wa 'Mkunazini' ambalo linazungumzia dhuluma walizopitia Waafrika chini ya utawala wa Wazungu. Mbali na kuundiwa soko la binadamu ambapo Waafrika walinadiwa, kuzabuniwa na kununuliwa ili kufanya kazi katika mashamba yao, walipigwa na kufanyiwa unyama. Walilazimishwa kufanya kazi na waliokaidi maagizo walipigwa kwa mijeledi. Zaidi ya hayo, walichukuliwa maelfu, hasa wale wenye nguvu wakasafirishwa bila hiari, kupitia nyikani na baharini hadi ughaibuni.

Dhuluma ambazo mshairi anaangazia katika shairi, 'Mkunazini', ndizo zile zile anazozungumzia katika shairi, 'Waafrika'. Inabainika kwamba lengo hasa la mshairi ni kumtaka mpokeaji kuelewa dhuluma na unyanyasaji uliofanyiwa Waafrika wangali katika mikono ya Wazungu kabla ya uhuru. Kuangaziwa kwa hali hii waliyojipata Waafrika kunasaidia mpokeaji kuona umuhimu wa kuwa na taifa huru hivyo kukuza uzalendo na umoja. Mwingiliano huu wa matini una uwezo wa kuhakikisha kwamba hadhira imaeelewa vyema suala linaloangaziwa katika mashairi haya mawili. Kwa kuwa shairi moja ni mwangwi wa jingine kidhamira, inadhihiridha kwamba wazo hilo kuu limerudiwa hivyo kuleta msisitizo unaochangia pakubwa katika uelewekaji. Kimsingi, kupiga mwangwi shairi, ni dhima muhimu sana ya urudiaji kama mtindo wa uandishi wa matini ya fasihi.

## 5.5 Kujenga wizani

Kwa mujibu wa Wales (2011:371), wizani ni tukio la kifonetiki hasa linalotokana na mpangilio sawa wa kifonemiki. Fonetiki ni kiwango cha lugha ambacho kinashughulikia sauti za lugha. Hata hivyo tunapojikita katika sauti za lugha fulani mahususi, kiwango cha kifonolojia hurejelewa. Hii ndiyo maana Wales anazungumzia mpangilio wa kifonemiki kwa kuwa tunaangazia sauti katika ushairi. Hivyo, katika ushairi, wizani unahusisha sauti zinazoundwa kwa mpangilio sawa wenye mapigo. Urudiaji ni mtindo wa uandishi ambao huchangia pakubwa katika kuathiri hadhira. Katika ushairi, silabi hupangwa katika mfumo maalum wa vina, ambao katika uwasilishaji, husababisha mapigo ya sauti ambayo huwa na athari kwa mpokeaji. Wizani ni mapigo ya sauti yanayotokana na urudiaji wa silabi katika shairi. Silabi huundwa kutokana na sauti ambazo zinaporadidiwa kwa muundo maalum, huleta ujumi. Silabi huweza kurudiwa katika sehemu tofautitofauti za vifungu vya shairi.

Wizani katika shairi ni dhima inayosababishwa na urudiaji wa silabi, uwe katika mfumo wa vina na mizani au muundo wowote unaotumiwa na mshairi. Katika diwani hizi, washairi wamedhihirisha mtindo wa urudiaji wa kisauti ambao unaathiri hisia za mpokeaji. Urudiaji wa silabi ndio unaohakikisha uwepo wa wizani katika shairi. Dhima hii ya urudiaji inabainika katika mashairi mengi kwenye diwani hizi. Kwa mfano, tunapoangazia shairi, 'Mafuriko' katika diwani ya *Dhifa*, tunashuhudia urudiaji wa silabi unaosababisha wizani kwa mpokeaji. Katika kifungu cha kwanza, mshairi ameradidi silabi, *ya,* anapotumia kihusishi cha mahali, *juu ya,* na silabi, *ni,* ambayo imerudiwa katika vielezi vya mahali kama vile: *vyooni, maofisini* na

*madarasani.* Aidha, shairi Jibwa linadhihirisha mapigo haya ya sauti kutokana na kurudiwa kwa silabi, *mu*, katika maneno, *utamu* na *hatamu*. Mashairi mengineyo katika diwani hii pia yanabainisha wizani. Hata hivyo, viwango vya urudiaji wa silabi hizi ndivyo vinavyotofautiana kutoka shairi moja hadi jingine.

> ...Juu ya mistari ya pundamilia,
> Na masikio makubwa ya tembo,
> Juu ya kuta vyooni, maofisini, madarasani,
> Juu ya paa za nyumba, kuta za ikulu
> Na juu ya khanga na tisheti... (uk.4)

Kwa upande mwingine, diwani ya *Vifaru Weusi* inadhihirisha pakubwa wizani ikilinganishwa na diwani ya *Dhifa.* Silabi nyingi katika mashairi tofautitofauti zimeradidiwa kwa wingi kupitia mfumo wa vina na miundo mingineyo. Kwa mfano, tukirejelea shairi, 'Madhabahu', silabi *na*, katika kifungu cha kwanza, inatokea baada ya kipindi fulani cha mizani: kila baada ya mizani mitatu, *huwindana, husakana, huvutana.* Hivyo ndivyo ilivyo katika kifungu cha tatu na nne ambapo silabi, *zwa* na *mu* zimeradidiwa mtawalia.

> Madhabahu takatifu,
> Huwindana,
> Husakana,
> Huvutana,
> Na pia kuumbwana...(uk.4)

Huu ni mfano mmoja tu kati ya mifano mingi sana inayoshuhudiwa katika diwani hii. Takribani mashairi yote katika diwani ya *Vifaru Weusi* yana mapigo ya sauti ambayo yanabainisha uwepo wa wizani. Kimsingi, washairi, Kezilahabi na Mohammed Khatibu, katika tungo zao, wamedhihirisha wizani ambao ni dhima mojawapo ya urudiaji unaotokana na kurudiwarudiwa kwa silabi.

## 5.6 Dhima ya ukumbukaji

Masuala yanayoangaziwa katika kazi ya fasihi yanaweza kubaki katika kumbukumbu ya mpokeaji kwa muda mrefu. Hali hii hutokea pale ambapo masuala hayo yanaradidiwa. Kwa kawaida, jambo linalorudiwarudiwa huhifadhiwa ubongoni haraka kuliko lile linalotajwa mara

moja tu. Mara nyingi washairi hutumia urudiaji kama mbinu ya kipekee inayohakikisha kwamba maana imekumbukwa hivyo kuendeleza dhamira. Maana huweza kukumbukwa katika shairi ikiwa maneno na vifungu vya sentensi vimeradiwarudiwa. Katika ushairi, uruduaji huendelezwa kwa njia maalum ambayo inawezesha msisitizo, uelewekaji na ukumbukaji. Mpokeaji ana uwezo mkubwa wa kukumbuka maana katika shairi hasa ikiwa wazo hilo linaradidiwa.

Mshairi anapotumia maneno au vifungu vya maneno na kuvirudiarudia kwa mtindo fulani, huweza kunasa na kugusa hisia za msomaji mbali na kuyachokora mahasa ya ndani ya mpokeaji huyo. Athari hizi zinaweza kukumbukwa hata miaka mingi baadaye kutokana na msisitizo unaotiliwa na urudiaji. Katika diwani tunazochunguza, kuna baadhi ya mashairi ambayo dhamira zao haziwezi kusahaulika upesi kwa sababu ya maneno na vifungu ambavyo vinarudiwarudiwa. Mshairi anapotumia kibwagizo katika shairi, huweza kukariri hisia zenye athari isiyosahaulika.

Kwa mfano, katika diwani ya *Vifaru Weusi,* shairi, 'Vitambi' linazungumzia ulafi wa viongozi wanaojitakia rasilamali za nchi ili kujinufaisha wenyewe. Mshairi amerudia neno vitambi mwanzoni mwa kila kifungu cha shairi ili kumwonesha msomaji taswira ya uono ya kiongozi mlafi. Mpokeaji wa shairi hili ana uwezo wa kuikumbuka dhamira inayozungumziwa. Mashairi mengi sana katika diwani hii yanadhihirisha dhima hii ya ukumbukaji wa masuala yanayoangaziwa hasa yale ambayo yana urudiaji wa kimaumbo. Mifano mingine ya mashairi yanayohakikisha kumbukumbu kupitia kwa urudiaji wa kimaumbo ni kama vile: Isiponyesha, Wasokauli, Nimi, Mbeleko, Damu! Damu! Damu!, Kivuli, Iwapi? na mengineyo. Vilevile, tunapoangazia shairi, 'Maisha' katika diwani ya *Dhifa*, mpangilio wa sauti za irabu na konsonanti unamwacha mpokeaji akiwa na hisia kuhusu hali ya maisha, ambayo anaweza kukumbuka kwa muda mrefu. Mbali na kudhihirisha wizani, mshairi ana lengo la kutaka mpokeaji apata hisia kuhusu maisha na namna anavyopaswa kuyakabili.Tazama kifungu cha pili cha shairi, 'Maisha.'

Lakini,
Ulimwengu kizaaazaa, umekaa, kibaabaa
Na maisha, yapaapaa, yamejaa, hadaadaa
Binadamu, twataataa, kwa fadhaa, twakaakaa
Na twenende, kichaachaa, kwa njaa, kigaagaa! (uk.32)

## 5.7 Suala la ujumi

Kwa mujibu wa Wales (2011: 09) ujumi ni utambuaji wa uzuri wa kitu. Ni tawi la falsafa ambalo linajishughulisha na uelezaji wa uzuri wa jambo. Kulingana naye, mtindo wa lugha unaotumiwa katika ushairi una uwezo wa kubainisha ujumi kama dhima ya kishairi. Anautazama ushairi kama sanaa inayotumia lugha kuleta ujumi katika matini. Cuddon (2013: 11) naye anayasisitiza mawazo ya Baumgarten akisema kwamba ujumi ni dhana ya kifalsafa ambayo inahusu utambuaji wa jambo kwa hisia za akili. Anaeleza kuwa ujumi ni uzuri unaojitokeza katika kazi ya sanaa. Binadamu huwa na hisia za akili ambazo humsaidia kutambua uzuri au ubaya wa kitu au jambo fulani linaliwasilishwa. Wataalamu hawa wanakubaliana katika wazo kwamba suala la ujumi ni tokeo la kifalsafa ambalo linahusisha akili. Ni uzuri unaotambuliwa na hisia za akili ya mpokeaji wa shairi fulani.

Kazi yoyote ya fasihi aghalabu huwasilishwa na msanii kwa kumlenga mpokeaji au hadhira. Msanii hujenga uelewekaji wa ujumbe na athari ya mpokeaji kuhusu ujumbe wenyewe unaowasilishwa kwa kutegemea mtindo wake wa lugha. Katika ushairi, uteuzi na mpangilio wa maneno huchangia pakubwa katika kuleta uzuri wa kazi. Aghalabu, ufundi wa kuunda ushairi humwezesha mpokeaji kutambua uzuri wake. Mpokeaji huweza kushawishika katika akili yake akawa na mtazamo chanya kwamba kazi fulani ni nzuri. Hivyo, sanaa ina uwezo wa kubainisha uzuri wa kazi ya fasihi. Njia mojawapo ya kuunda uzuri wa shairi ni kupitia kwa mtindo wa urudiaji. Ukamilifu wa hisia za akili unaosababisha mtazamo chanya wa kazi ya fasihi, kupitia kwa sanaa ndio unaoleta ujumi. Kimsingi, ujumi ni uzuri wa kazi ya fasihi unaotambulika kutokana na hisia za akili ya hadhira. Washairi, Kezilahabi na Mohammed Khatib, wametumia mtindo wa urudiaji kuleta ujumi katika mashairi yao. Katika diwani hizi, ujumi unajitokea kupitia kwa mipangilio ya maneno na vifungu vya maneno vilivyorudiwarudiwa kwa miundo fulani. Kwa mfano, tunapoangazia shairi 'Mtakaso' katika diwani ya *Dhifa,* mshairi anatambua wasiwasi na hofu ya mhusika kwa ujumi. Kwanza, katika kifungu cha kwanza mhusika huyu anapotembea, watoto wanamsengenya huku wakibishana, 'Ndiye!Siye!Ndiye!Siye!' kisha anapotazama nyuma, kimya kinatawala. Pili, katika kifungu cha tatu, anasikia tena sauti ikimwita kwa jina lake halisi, 'Chupa' ambalo linarudiwarudiwa kwa hisia ya mshangao. Anapotazama nyuma tena, kimya kinatawala.

''Chapu!'' Nyumangu "Chapu!"
Nani aninyatia! Hatua mbili natembea.

"Chapu Chapu!" Nyumangu " Chapu Chapu!"
Nani! Natazama nyuma:
Kiza. Kimya. (uk.19)

Kifungu cha pili cha shairi, 'Alalaye', mshairi ametumia usambamba wa kifahiwa kwa mpangilio unaodhihirisha ujumi. Mbali na kutumia maneno yenye uhusiano wa kifahiwa, yaani *wadhani, wafikiri na wahisi,* mshairi ametumia sentensi yenye usambamba wa kimaana ili kusisitiza maana. Maana ile ile imerudiwa kwa kubadilisha mtindo wa maneno katika mstari wa pili, nne na wa sita. Mistari hii mitatu yenye maana sawa inapokezana kwa njia inayoleta ujumi wa shairi lenyewe.

Tumeona ngozi ya ng'ombe imewambwa,
Wafikiri hatujui nyama ilikoenda,
Tumeona mifupa ya kuku jalalani,
Wadhani hatujui nani kafaidi,
Tumaona vyombo vikisafishwa,
Wahusu hatujui nani kala. (uk.26)

Mashairi mengi katika diwani ya *Vifaru Weusi* yana mtindo wa urudiaji wa kimaumbo hasa kutokana na vibwagizo vya kiubunifu ambavyo mshairi ametumia. Kibwagizo cha kiubunifu ni kibwagizo kifupi. Muundo wa shairi ambao una kibwagizo kifupi huonyesha ubunifu wa kiwango kikubwa ikilinganishwa na vibwagizo vingine. Shairi ambalo limeundwa kwa ubunufu mzuri aghalabu huwa na ujumi kwani ujumi ni dhana ya kiakili inayotokana na ufundi au sanaa. Katika shairi ambalo lina kibwagizo cha kiubunifu, kibwagizo chenyewe huweza kuwa ni neno moja au mawili ambayo yanaradidiwa kwa muundo fulani unaoleta ujumi. Mashairi yanayothibitisha ujumi katika diwani hii ni kama vile: Isiponyesha, Wasokauli, Mbeleko, Damu! Damu! Damu!, Iwapi?, Mzimu, Mlipindua?, Waafrika na mengineyo. Shairi, 'Waafrika' ni la kipekee kwa kuwa mstari wa mwisho unaorudiwa umeandikwa kwa herufi kubwa hivyo kuleta ujumi wa kazi yenyewe, hali inayosaidia katika ukumbukaji. Kimsingi, diwani hizi mbili zimedhihirisha ujumi kama jukumu kubwa la urudiaji ambalo linachangia pakubwa katika ukumbukaji wa kinachowasilishwa na mshairi.

## 5.8 Suala la uziada

Leech (1969: 57) anaeleza kwamba lugha inaweza kutumika katika sanaa kwa njia inayokiuka matumizi ya kawaida ya maneno katika jamii. Hii ina maana kwamba ukiushi ni mtindo wa kipekee ambao msanii hutumia kuwasilisha ujumbe kwa njia tofauti na inavyozoeleka katika maongezi ya kawaida. Ukiushi huo unaweza kujitokeza kupitia kwa uziada. Leech na Short (2007: 44) nao wanauona uziada kama njia inayohakikisha msukumo wa ukiushi katika ushairi. Msukumo huu huweza kujitokeza katika viwango mbalimbali vya lugha kama vile: kifonetiki, kisintaksia na kisemantiki ambapo viwango hivyo vinakuzwa zaidi hivyo kujitokeza sana. Kwa mujibu wa Wales (2011: 166) uziada ni mbinu ya ukiushi wa maongezi ya kawaida ambayo ina msukumo wa ishara za lugha ili ziweze kutambulika zaidi ya nyingine. Ishara za lugha ambazo Wales anazungumzia ni sauti, maneno, virai, vishazi na maneno ambayo yanatumika katika lugha. Ishara hizi huweza kusisitizwa kwa kuradidiwa kwa mitindo mbalimbali katika shairi. Mshairi huzipa ishara hizi, msukumo wa kuweza kukuzwa ili zitambulike zaidi na mpokeaji. Kwa upande mwingine, Cuddon (2013:284) anaeleza kwamba uziada ni mbinu ya kijieleza ambapo maneno na vifungu vya maneno hukuzwa kwa njia ambayo inaweza kutambulika na kujitokeza sana. Kulingana naye, uziada ni mbinu ya kishairi ambayo ni muhimu sana katika kufanya jambo lionekane zaidi na mpokeaji. Maelezo haya ya wataalamu yanaafikiana katika wazo kwamba uziada ni mbinu ya kishairi ambayo hukuza zaidi ishara za lugha kwa njia inayojitokeza sana kwa mpokeaji.

Katika ushairi, urudiaji unaweza kutokea kwa njia ambayo mpokeaji huhisi kwamba kuna uziada. Neno au kifungu fulani cha maneno kinaweza kujitokeza zaidi ya vinginevyo hivyo kufanya vifungu hivyo kuonekana sana na mpokeaji. Lengo la mshairi katika kuchimuza maneno ni kuhakikisha kwamba mpokeaji ameyatambua na kuyatia mawazo katika maneno yayo hayo ambayo anarudia. Mshairi huyapa maneno hayo uzito wa kipekee kwa kutaka mpokeaji ayatambua maneno hayo tu na si mengine kwa sababu ya mchango mkubwa wa maneno hayo katika kuendeleza dhamira. Mshairi anapotumia uziada katika shairi, huondoa utata unaoweza kuzuka katika kazi na kumsaidia mpokeaji kukuza uelewekaji wa suala linalozungumziwa.

Urudiaji ndio mtindo wa kipekee ambao mshairi huweza kutumia kuleta uziada katika shairi. Muhammed Khatib ameuendeleza uziada katika shairi, 'Niamini' ambapo anaangazia uhusiano wa kimapenzi. Anamtaka mpenziwe, 'Muhibaki' aweze kumwamini kwamba anampenda na

hawezi kamwe kumwacha kwa ajili ya mwengine. Anasisitiza kwamba ameridhika na penzi hilo na daima habanduki, hageuki, hatoki wala habadili nia kuhusu uhusiano wao. Mshairi ametumia neno, niamini, akilenga kuhakikisha kwamba mpokeaji amelitazame na kulitambua zaidi ya mengine kwa kuwa neno hilo ndilo msingi wa dhamira ya shairi hili. Kifungu cha kwanza, ambacho kimeundwa kwa maneno matano, neno, niamini linajitokeza mara nne. Hii ina maana kuwa neno hilo ndilo linalochimuzwa ili kulisisitiza zaidi. Katika vifungu vinginevyo, neno lenyewe limeradidiwa kimaumbo ambapo neno, niamini linajitikeza mwanzoni mwa kila kifungu.

Niamini,
Niamini, niamini, Muhibaki,
Niamini.
Niamini,
Muhibaki, muhibaki, simtaki,
Mwingine…(uk.25)

Mbali na kuyakuza maneno, ukiushi pia hujitokeza katika kiwango cha kifonetiki ambapo sauti moja inajitokeza zaidi ya nyingine. Ukiushi huu wa kisauti, una mchango mkubwa katika kuendeleza wizani. Kwa mfano, kwa kutazama shairi, 'Maisha' katika diwani ya *Dhifa*, tunashuhudia irabu, *a*, iliyorudiwarudiwa kwenye maneno yote ishirini isipokuwa neno moja tu, 'ulimwengu' ambalo linatanguliza kifungu cha pili. Sauti hiyo imechimuzwa zaidi kiasi kwamba, hata kwa kutazama tu, mpokeaji ana uwezo wa kuitambua namna inavyojitokeza maradufu. Uziada wa aina hii huathiri hisia za mpokeaji hasa katika uwasilishaji wa shairi lenyewe.

Ulimwengu, kizaazaa, umekaa, kibaabaa,
Na maisha yapaapaa, yamejaa, hadaadaa,
Binadamu, twataataa, kwa fadhaa, twakaakaa,
Na twenenda, kichaachaa, kwa njaa, kigaagaa!...(uk.32)

Uziada kama mojawapo ya majukumu yanayoendelezwa na urudiaji, ni muhimu sana katika shairi kwa kuwa humsukuma mpokeaji katika kutambua zaidi, sauti, maneno au vifungu vya maneno ambavyo vinakuzwa zaidi ya vinginevyo. Hali hii huhakikisha umakinifu katika maneno yenye msingi wa dhamira katika kazi husika. Kezilahabi na Muhammed Khatib, wamebainisha

uziada huu japo katika mshairi machache ambayo yanatosha kudhihirisha urudiaji kama mtindo unaoweza kutumika kuleta uziada katika matini.

## 5.9 Hitimisho

Sura hii imechunguza dhima ya urudiaji katika mashairi ya diwani za *Dhifa* na *Vifaru Weusi*. Urudiaji kama mbinu ya kimtindo, umetumiwa na washairi kuwasilisha maana kwa namna inavyoathiri hisia za mpokeaji. Swali ambalo tumejiuliza katika sura hii tukajaribu kulijibu ni, je, urudiaji una majukumu gani kwa mpokeaji wa mashairi ya kisasa? Urudiaji unapotumiwa na mshairi kuwasilisha maana, huhakikisha uelewekaji, usisitizaji na ukumbukaji wa masuala yanayoangaziwa katika shairi. Mbali na hayo, urudiaji huhakikisha kwamba maana ambayo inayowasilishwa imejitokeza kwa ujumi na wizani unaomfanya mpokeaji kuathirika kihisia. Hii ina maana kwamba urudiaji una mchango mkubwa sana katika kuwasilisha maana na kuendeleza dhamira ya mshairi.

# SURA YA SITA

# HITIMISHO

## 6.1 Utangulizi

Katika sura hii, tumehitimisha utafiti wetu kuhusu urudiaji na uwasilishaji wa maana katika diwani za *Dhifa* na *Vifaru Weusi.* Tumeangazia matokeo ya utafiti huu, umuhimu wake na kutoa mapendekezo ya utafiti zaidi kuhusu mtindo katika diwani hizi teule.

### 6.2 Muhtasari wa utafiti

Utafiti huu unahusu urudiaji kama mbinu ya kisanaa ambayo mshairi yeyote anaweza kutumia katika kuwasilisha maana na kuendeleza dhamira anayokusudia. Tumeongozwa na malengo manne makuu ambayo ni kueleza aina mbalimbali za urudiaji katika ushairi, kubainisha matumizi ya urudiaji katika diwani ya *Dhifa* na *Vifaru* Weusi na kubainisha dhima na athari za urudiaji katika diwani hizi mbili. Tumeujenga utafiti wetu chini ya mihimili ya nadharia ya umitindo ambayo inaelekeza umuhimu wa namna mshairi anavyoweza kutumia lugha kuwasilisha ujumbe katika mashairi ya kisasa. Nadharia hii inashikilia umuhimu wa kutumia lugha kwa upekee ili ujumbe uweze kumfikia mpokeaji kwa njia ya msisitizo. Tumetambua mbinu ya urudiaji na kuangazia aina mbalimbali za urudiaji na namna zinavyojitokeza katika diwani husika. Kuna aina tofautitofauti za urudiaji ambazo tumechunguza kwa kuzigawa katika matapo manne ambayo ni: urudiaji sahili, urudiaji wa kimaumbo, urudiaji wa miundo na urudiaji wa kibalagha. Katika urudiaji sahili tumeangazia msamiati au maneno yanayorudiwa na namna yanavyorudiwa, urudiaji wa irabu, konsonanti na silabi ambazo zina mchango mkubwa katika kuleta wizani.Tumeangazia urudiaji wa kimaumbo ambapo tumechunguza kibwagizo cha kiubunifu na kubainisha kiunganishi 'na' kama ilivyotumika katika mashairi.

Urudiaji wa kimuundo ni aina nyingine ambayo tumechunguza ili kutambua namna miundo ya virai, vishazi na sentensi inavyoweza kutumika na mshairi kusisitiza maana. Katika kuendeleza urudiaji huu wa kimuundo, tumezungumzia usambamba kama urudiaji wa kipekee ambao unahusisha miundo mbalimbali ya vifungu vya maneno vinavyoradidiwa. Usambamba wa kimuundo, kisintaksia, kifahiwa, kimaana au kidhamira, kitanakuzi, kivisawe na usambamba wa kidhamira ndio tuliobainisha katika utafiti wetu. Ijapokuwa kuna aina nyingi za usambamba,

utafiti wetu umejishughulisha na aina hizi chache ambazo kwa maoni yetu zinatosha kuthibitisha urudiaji wa kimuundo uliotumiwa na washairi wa diwani husika. Aidha, katika utafiti huu, tumeangazia urudiaji wa kibalagha, yaani ule unaohusishwa na balagha kama vile: epanalepsia, anadiplosia, anafora na epifora. Hizi ni baadhi ya mbinu za kibalagha zinazoweza kuchunguzwa katika matini. Hata hivyo, kuna aina nyinginezo ambazo hatujazungumzia katika utafiti huu. Tumeziwekea msingi, aina hizi za urudiaji kwa kuzitolea maelezo kabla ya kuzibainisha katika diwani.

Utafiti huu umechunguza namna viwango vya urudiaji vinavyojitokeza katika *Dhifa.* Tumebainisha aina za urudiaji katika kiwango cha kifonetiki, kisintaksia na kisemantiki kwa kutoa mifano mwafaka. Maana katika mashairi mbalimbali ya diwani hii, zimesisitizwa ili kuhakikisha uelewekaji na ukumbukaji wa masuala yanayozungumziwa. Katika uchunguzi wetu, tumebainisha kwamba aina hizi za urudiaji zimejitokeza kwa viwango tofauti tofauti. Hii inatokana na idadi ya mifano ambayo tumetoa katika kila aina tuliyochunguza. Tumeangazia tu aina za urudiaji zilizotumiwa na mshairi hasa katika usambamba na urudiaji wa kibalagha. Katika diwani ya *Vifaru Weusi,* aina za urudiaji ambazo tumechunguza ni zile zile tulizoziwekea msingi katika sura ya pili na hata kuziangazia katika sura ya tatu. Katika sura za tatu na nne, tumefanya uchunguzi wa kinadharia kuhusu mashairi ya diwani mbili ili kudhihirisha namna washairi walivyotumia urudiaji kama mbinu ya kimtindo kuendeleza dhamira. Tumebainisha namna urudiaji wa irabu na konsonanti unavyojitokeza kutokana na mipangilio ya abjadi katika kiwango cha grafolojia. Hali hii inatiliwa mkazo na wazo la Leech (1969: 39) anayesema kwamba athari za kisauti huweza kudhihirika katika akili ya msomaji anaposoma ushairi kwa sauti au kimoyomoyo. Mkabala huu umekuwa muhimu katika kutambua wizani kama jukumu mojawapo la urudiaji.

Urudiaji huwa na dhima na athari zake kwa mpokeaji wa shairi. Kwa kuwa mshairi humlenga mpokeaji, hutumia mtindo wa lugha unaomwezesha kuelewa dhamira ipasavyo. Msisitizo wa maana hutokea pale ambapo maana yenyewe imeradidiwa katika shairi hivyo kuhakikisha kwamba ujumbe unaowasilishwa umeeleweka na kukumbukwa na mpokeaji. Urudiaji una majukumu mbalimbali ambayo tumeangazia na kuyabainisha katika diwani ya *Dhifa* na *Vifaru Weusi.* Dhima ambazo tumeangazia katika sura ya sita ni kama vile: usisitizaji, ukumbukaji, uelewekaji, ujumi, upigaji mwangwi wa dhamira, wizani na uziada. Kimsingi, urudiaji una

mchango mkubwa sana katika usisitizaji wa maana kwani ni rahisi sana kutia katika kumbukumbu, masuala yanayorudiwarudiwa. Hali kadhalika, athari za kihisia zinazomfanya mpokeaji kushawishika kwamba baadhi ya mashairi tuliyochunguza yana ujumi wa kipekee hutokana na urudiaji.

## 6.3 Mapendekezo

Utafiti huu umejikita katika urudiaji, kama suala mojawapo la kimtindo ambalo mshairi hutumia kuwasilisha maana na kuendeleza dhamira. Tumeangazia na kuchunguza aina mbalimbali za urudiaji zinazojitokeza katika diwani za *Dhifa* na *Vifaru Weusi* na kubainisha viwango vya sauti, neno na vifungu vya maneno. Dhana hii ya urudiaji inapaswa kufanyiwa utafiti zaidi ili kudhihirisha kwa mapana, urudiaji wa kibalagha katika diwani hizi. Hii ni kwa sababu urudiaji ni mtindo muhimu sana katika mawasiliano kupitia kwa matini na usemaji. Hata hivyo kuna aina nyinginezo za urudiaji wa kibalagha ambazo hatujaangazia katika utafiti wetu. Kwa kuwa tumeangazia urudiaji, ambao ni mtindo mmoja tu unaotumika na mshairi kuwasilisha maana, tunapendekeza utafiti zaidi ufanywe ili kubainisha mitindo mingine ambayo washairi wa diwani hizi wametumia kuendeleza dhamira.

# MAREJELEO


Bradford, R. (1997) *Stylistics*. London: Routledge.

Crystal, D. & D. Davy, (1969) *Investigating English Style*. London: Longman Group.

Cuddon, J. (2013) *A Dictionary of Literary Terms and Literary Theory.* USA: Wiley-Blackwell.

Croft, S. na Myers, R. (2000) *Exploring Language and Literature*. London: Oxford University Press.

Galperin, I. R. (1971) *Stylistics*. Moscow: Higher School Publishing House.

Jeffries, L na Mclntyre, D (2010) *Stylistics*. New York: Cambridge University Press.

Kezilahabi, E. (2008) *Dhifa.* Nairobi: Vide-Muwa Publishers.

Khatib, M.S. (2016 ) *Vifaru Weusi.* Nairobi: Vide-Muwa Publishers.

Leech, G.N. (1969) *A Linguistic Guide to English Poetry*. London: Longman Group Limited.

Leech, G. (1981) Semantics*, The study of meaning.* Bingay: Richard Clay Limited.

Leech, G. Short, M ( 2007) *Style in Fiction*. London: Pearson Education Limited.

Manjavidze, T (2013) *Stylistics Repetition, Its Peculiarities and Types in Modern* English. European Scientific *Journal Special Edition*: European Scientific Institute 1857-7881 (print) e-ISSN 1857-7431.

Mclin, A (1996) *Reference Guide to English. A Handbook of English as a Second Language.* Washington D. C: United State Information Agency.

Migrant.net>pass>pdf>Reading>poetry (2012) 'Reading on The Move: Poetry: Rhyme, Repetition and Rhythm'. National PASS Centre. Migrant Education Program Consortium.

Mnenuke, A.(2010) ' *Dhima ya Urudiaji katika Mawasiliano ya Kiswahili: Uimarishaji na Udhoofishaji wa maana.*' Jarida la Taasisi ya Taaluma ya Kiswahili Toleo La 74: 32-44.

Msokile, M. (1993) *Misingi ya Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: English Press Limited.

Mueller, M. (2015) ' The use of Repetition in Betti Alver's Poetry: A Stylistic analysis. Master's Thesis, University of Tartu, Chuo Kikuu Cha Nairobi. (Haijahapishwa).

Mwania, J (2007) 'Usambamba katika ushairi huru'. Tasnifu ya M.A Kenyatta, Chuo kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Mweri, J. (2010) *Utangulizi wa Isimu.* Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Ndumbu (2013) 'Matumizi ya takriri na istiari katika Utenzi wa Ras'lghuli'. Tasnifu ya MA Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Preminger, A and Brogan, T. (1993) *The new princeston encyclopedia of poetry and poetics.* New Jersey: Princeton University Press.

Simpson, P. (2004) *Stylistics. A Resource Book for Students.* New York: Routledge.

Venance, F (2013) 'Uhakiki wa Ushairi, Diwani ya Fungate ya Uhuru'. Venancefuraha.blogspot.com.

Wales, K (2011) *A Dictionary of Stylistics*. Third Edition. London; Routledge.

Wamitila, K.W. (2003) *Kamusi ya Fasihi Istilahi na Nadharia.* Nairobi: Focus Publications Limited.

Wamitila, K. W. (2008) *Kanzi ya Fasihi. Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi: Vide-Muwa Publishers.

Yeats na wenzake (1979) *The language of Modern Poetry*. Great Britain: Andre Deutsch Limited.